

**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

---

National Development Plan

One-Year Development Plan

---

1987

# Mpango wa Maendeleo wa Mwaka, 1986 - 1987

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Fedha

---

<https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/777>

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



**MPANGO WA MAENDELEO  
WA MWAKA 1986/87**

Juni, 1986

*Kimetolewa na* WIZARA YA FEDHA, MIPANGO NA UCHUMI  
DAR ES SALAAM—TANZANIA

1986

KIDKEPIGWA CHAPA NA MPIGACHAPA WA SERIKALI  
DAR ES SALAAM—TANZANIA

*Bei Sh. 60/-*

THE UNIVERSITY OF CHICAGO  
DEPARTMENT OF CHEMISTRY  
5400 S. UNIVERSITY AVENUE  
CHICAGO, ILL. 60637

THE UNIVERSITY OF CHICAGO  
DEPARTMENT OF CHEMISTRY

*MPANGO WA MAENDELEO  
WA MWAKA 1986/87*



# MPANGO WA MAENDELEO WA MWAKA 1986/87

## YALIYOMO

	<i>Ukurasa</i>
UTANGULIZI ... ..	v
<b>SURA YA KWANZA:</b>	
Hali ya Uchumi kwa Ujumla ... ..	1
<b>SURA YA PILI:</b>	
Utekelezaji wa Mpango wa 1985/86 ... ..	3
<b>SURA YA TATU:</b>	
A. Mpango wa Kufufua Uchumi 1986/87—1988/89 ... ..	4
B. Mpango wa Fedha na Karadha ... ..	5
C. Mpango wa Fedha za Kigeni wa Mwaka 1986/87 ... ..	8
<b>SURA YA NNE:</b>	
Mipango ya Sekta Mbali mbali ... ..	12
Muhtasari na Mpango ... ..	12
1. Kilimo ... ..	13
2. Mifugo ... ..	16
3. Viwanda ... ..	18
4. Maliasili ... ..	19
5. Madini ... ..	20
6. Biashara na Utalii ... ..	21
7. Ardhi ... ..	21
8. Ujenzi ... ..	22
9. Nishati ... ..	23
10. Usafirishaji na Mawasiliano ... ..	24
11. Maji ... ..	27
12. Elimu ... ..	28
13. Afya na Ustawi wa Jamii ... ..	29
14. Maendeleo ya Jamii na Utawala ... ..	30
15. Kazi ... ..	30
<b>SURA YA TANO:</b>	
Mpango wa Maendeleo wa Mikoa Mwaka 1986/87 ... ..	32
<b>SURA YA SITA:</b>	
Sayansi na Tekinologia ... ..	35
<b>SURA YA SABA:</b>	
Sekta ya Watu Binafsi ... ..	37
	<i>Nyongeza "A"</i>
	<i>Ukurasa</i>
Fedha za Maendeleo kwa Mwaka 1986/87— ... ..	39
<i>Fungu Wizarat Idara</i>	
30 Ofisi ya Rais ... ..	40
31 Ofisi ya Makamu wa Rais ... ..	40
32 Kazi na Maendeleo ya Utumishi ... ..	40
34 Nje ... ..	43
37 Ofisi ya Waziri Mkuu (PMO) ... ..	43
38 Ngome ... ..	44
39 Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ... ..	44
40 Mahakama ... ..	45
41 Sheria ... ..	45
43 Kilimo na Mifugo ... ..	45
44 Viwanda na Biashara ... ..	53
46 Elimu ... ..	62

<i>Fungu</i>	<i>Wizarati/dara</i>	<i>Ukurasa</i>
47	Mawasiliano na Ujenzi ... ..	65
48	Ardhi, Maji, Nyumba na Maendeleo Mijini ... ..	71
49	Nishati na Madini ... ..	74
50	Fedha, Uchumi na Mipango ... ..	76
51	Mambo ya Ndani ... ..	79
52	Afya na Ustawi wa Jamii ... ..	82
53	Maendeleo ya Jamii, Utamaduni na Michezo ... ..	83
54	Radio ... ..	85
55	Makao Makuu ... ..	85
57	Ulinzi ... ..	87
60	Maliasili na Utalii... ..	87
61	Serikali za Mitaa na Maendeleo ya Ushirika ... ..	90

*Nyongeza "B"*

**Mpango wa Mikoa—Fedha za Maendeleo kwa Mwaka 1986/87**

<i>Fungu</i>	<i>Mkoa</i>	<i>Ukurasa</i>
70	Arusha ... ..	200
71	Pwani ... ..	201
72	Dodoma ... ..	202
73	Iringa ... ..	203
74	Kigoma ... ..	205
75	Kilimanjaro ... ..	206
76	Lindi ... ..	207
77	Mara ... ..	208
78	Mbeya ... ..	209
79	Morogoro... ..	210
80	Mtwara ... ..	212
81	Mwanza ... ..	213
82	Ruvuma ... ..	215
83	Shinyanga... ..	216
84	Singida ... ..	217
85	Tabora ... ..	218
86	Tanga ... ..	219
87	Kagera ... ..	220
89	Rukwa ... ..	221

KIELELEZO CHA VIFUPISHO

DANIDA	...	...	...	Danish International Development Agency.
UNDP	...	...	...	United Nations Development Programme.
UNICEF	...	...	...	United Nations International Children and Education Fund.
U.K.	...	...	...	United Kingdom.
W/BANK/BDU/NIA	...	...	...	World Bank.
SIDA	...	...	...	Swedish International Development Agency.
USAID	...	...	...	United States Agency for International Development.
IDA	...	...	...	International Development Agency.
FRG	...	...	...	Federal Republic of Germany.
UNFPA	...	...	...	United Nations Funds for Population Activities.
STABEX	...	...	...	Stabilization and Export Earning Scheme of Lome Convention.
EEC	...	...	...	European Economic Community.
NETHER...	...	...	...	Netherlands.
UNESCO	...	...	...	United Nations Educational Scientific and Cultural Organization.
UNHCR	...	...	...	United Nations High Commission for Refugees.
IBRD	...	...	...	International Bank for Reconstruction and Development.
NORAD	...	...	...	Norwegian Agency for International Development.
THB	...	...	...	Tanzania Housing Bank.
TRDB	...	...	...	Tanzania Rural Development Bank.
TIB	...	...	...	Tanzania Investment Bank.
EDF	...	...	...	European Development Fund.
TDFL	...	...	...	Tanganyika Development Finance Company Limited.
NBC	...	...	...	National Bank of Commerce.
WHO	...	...	...	World Health Organization.
BADEA	...	...	...	Arab Bank of Economic Development in Africa.
CIDA	...	...	...	Canadian International Development Agency.
B/FUND	...	...	...	Beverage Development Fund.
S/C	...	...	...	Supplier's Credit.
TG/FD	...	...	...	Textiles and Garments Funds.
WFHDF	...	...	...	Worker's and Farmers' Housing Development Fund.
WFP	...	...	...	World Food Programme.
SSPF	...	...	...	Sugar and Sugar Products Fund.
FAO	...	...	...	Food and Agricultural Organization.
ICPE	...	...	...	International Centre for Public Enterprises Yugoslavia.
BT	...	...	...	Bank of Tanzania.
CIF	...	...	...	Cost, Insurance and Freight.
SAREC	...	...	...	Swedish Agency for Research Co-operation with Developing Countries.
HPI	...	...	...	Heifer Project International.
EIB	...	...	...	European Investment Bank.
ABDI/SBI	...	...	...	Industrial Development Bank of India/State Bank of India.
RIDEP	...	...	...	Rural Intergrated Development Programme.
T.B.L.	...	...	...	Tanzania Breweries Limited.
NPC	...	...	...	National Printing Company.
ABD	...	...	...	African Development Bank.
ILO	...	...	...	International Labour Organization.
N.E.C.	...	...	...	National Engineering Company.
DAFCO	...	...	...	Dairy Farms Company.
TANRIS	...	...	...	Tanzania Research Information Service.
IDM	...	...	...	Institute of Development Management (Mzumbe).
TPB	...	...	...	Tanzania Pyrethrum Board.
TSA	...	...	...	Tanzania Sisal Authority.
TAT	...	...	...	Tobacco Authority of Tanzania.
TCA	...	...	...	Tanzania Cotton Authority.
TTA	...	...	...	Tanzania Tea Authority.
CATA	...	...	...	Cashewnut Authority.
CAT	...	...	...	Coffee Authority of Tanzania.
SAP	...	...	...	Structural Adjustment Programme
CP	...	...	...	Consumer Price Index.
GNP	...	...	...	Gross National Product.
IMF	...	...	...	International monetary Fund.
SADCC	...	...	...	Southern African Development Co-ordination Conference.
PTA	...	...	...	Preferential Trade Area.
TALIRO	...	...	...	Tanzania Livestock Research Organization.
NARCO	...	...	...	National Ranching Company.
THS	...	...	...	Tanzania Hides and Skins Company.
NAPCO	...	...	...	National Poultry Company.
TAFIRI	...	...	...	Tanzania Fisheries Research Institute.
STAMICO	...	...	...	State Mining Corporation.
NASACO	...	...	...	National Shipping Company.



BIT	...	...	...	...	Board of Internal Trade.
AISCO	...	...	...	...	Agricultural and Industrial Supplies Company.
TTC	...	...	...	...	Tanzania Tourist Corporation.
VIP	...	...	...	...	Ventilated Improved Pit Latrines.
TRM	...	...	...	...	Trunk Roads Maintenance.
NDC	...	...	...	...	National Development Corporation.
TFC	...	...	...	...	Tanzania Fertilizer Company.
TBS	...	...	...	...	Tanzania Bureau of Standards.
CAMARTEC	...	...	...	...	Centre for Agro Mechanization and Rural Technology.
TIRDO	...	...	...	...	Tanzania Industrial Research Organization.
TISCO	...	...	...	...	Tanzania Industrial Studies Consulting Organization.
TEMDO	...	...	...	...	Tanzania Engineering and Mechanical Designing Organization.
TBCL	...	...	...	...	Tanzania Bags Company Ltd.
BML	...	...	...	...	Blanket Manufacturers Ltd.
UGL	...	...	...	...	Ubungo Garments Ltd.
ALAF	...	...	...	...	Aluminium Africa Ltd.

## UTANGULIZI

1. Mpango wa Maendeleo wa 1986/87 umeandaliwa katika mazingira ya hali ngumu ya uchumi iliyokuwepo mwaka 1985/86 na miaka kadhaa iliyopita. Kwa msingi huu, mpango unazingatia umuhimu wa koeendeleza juhudi za kufufua uchumi na, kiutekelezaji, ni wa mwanzo katika mpango maalum wa kufufua uchumi wenye upeo wa miaka mitatu kuanzia 1986/87 hadi 1988/89.

Kwa msingi wa yaliyoelezwa hapo juu, Mpango wa 1986/87 utaendelea kutekeleza miradi inayoendelea kwa kuweka umuhimu wa kwanza kwa miradi inayotarajiwa kukamilika katika mwaka huo huo wa 1986/87. Mpango hauanzishi miradi mipya ita pale tu inapoonekana kuwa miradi mipya ni muhimu katika juhudi ya kufufua uchumi.

Kwa lengo hilo hilo la kufufua uchumi, Mpango wa 1986/87 unasisitiza zaidi uwekezaji rasilimali katika sekta za uzalishaji mali moja kwa moja. Katika lengo hili la jumla, mkazo mkubwa umewekwa katika sekta ya kilimo kwa maana ya kilimo cha mazao, mifugo, hifadhi ya ardhi pamoja na barabara na madaraja vijijini. Sekta hii imepangiwa kutumia asilimia 30.6 ya fedha zote za Mpango. Mpango pia unatoa umuhimu kwa sekta ya viwanda ili kuwezesha kuzalisha bidhaa zaidi ambazo ni motisha kwa wakulima na wazalishaji wengine. Vile vile huduma za kiuchumi hasa ardhi na ujenzi, mawasiliano na uchukuzi na nishati ambazo zinatoa huduma za moja kwa moja kwa sekta zinazozalisha mali zimepewa umuhimu katika Mpango.

Katika bajeti ya Serikali, Mpango wa Maendeleo wa 1986/87 unatarajiwa kugharimu Shs. 6,985 milioni ambayo ni ongezeko la asilimia 2.3 kulinganisha na makadirio ya mwaka 1985/86. Mchango wa sekta ya umma katika Mpango unakadiriwa kuwa Shs. 2,287 milioni ambazo zinajumlisha fedha ya mashirika ya umma yenyewe, mifuko maalum na mikopo toka mabenki. Hivyo Mpango wote wa Maendeleo wa mwaka 1986/87 unakadiriwa kugharimu Shs. 9,872 milioni. Mgawanyo wa makadirio baina ya fedha toka bajeti ya Serikali na mchango wa mashirika ya umma umeonyeshwa kwa kila mradi katika mafungu yanayohusika katika Mpango.

Sura ya kwanza ya Mpango inatoa muhtasari wa hali ya uchumi kwa jumla na maendeleo katika vigezo muhimu vya uchumi. Sura ya pili inatoa maelezo mafupi kuhusu utekelezaji wa Mpango wa 1985/86 ambayo ni moja ya mambo muhimu yaliyozingatia katika utayarishaji wa Mpango wa 1986/87. Sura ya tatu inatoa ufafanuzi kuhusu mambo mengine muhimu yaliyozingatia katika utayarishaji wa Mpango wa 1986/87. Sura inayofuata inatoa maelezo mafupi juu ya mipango ya sekta mbali mbali pamoja na orodha ya miradi ya Wizara na mashirika ya umma katika Nyongeza "A" na orodha ya miradi ya mikoa katika Nyongeza "B".

**C. D. Msuya,**  
*Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango*

UNIVERSITY

The University of Toronto is pleased to announce the appointment of Dr. [Name] as the new [Title]. Dr. [Name] has a B.Sc. in [Field] from the University of Toronto and a Ph.D. in [Field] from the University of [Country].

Dr. [Name] will be joining the [Department] in [Month]. He/She will be responsible for [Responsibilities]. Dr. [Name] is a member of the [Society] and has published [Number] papers in [Journal].

Dr. [Name] is a member of the [Society] and has published [Number] papers in [Journal]. He/She is also a member of the [Society] and has published [Number] papers in [Journal]. Dr. [Name] is a member of the [Society] and has published [Number] papers in [Journal].

Dr. [Name] is a member of the [Society] and has published [Number] papers in [Journal]. He/She is also a member of the [Society] and has published [Number] papers in [Journal]. Dr. [Name] is a member of the [Society] and has published [Number] papers in [Journal].

Dr. [Name] is a member of the [Society] and has published [Number] papers in [Journal]. He/She is also a member of the [Society] and has published [Number] papers in [Journal]. Dr. [Name] is a member of the [Society] and has published [Number] papers in [Journal].

C. D. [Name]  
[Title]

## SURA YA KWANZA HALI YA UCHUMI KWA JUMLA

1. Matumaini ya kuzinduka kwa uchumi yaliyokuwa makubwa katika mwaka 1984 kutokana na maendeleo mazuri katika bandhi ya vigezo (parameters) muhimu vya uchumi, hayakuweza kuendelea katika viwango hivyo katika mwaka 1985. Uzalishaji wa bidhaa na utoaji wa huduma kwa jumla ulishuka ikilinganishwa na mwaka 1984 na ingawaje katika sekta ya kilimo hali ya chakula iliendelea kuwa nzuri kutokana na hali nzuri ya bewa katika sehemu nyingi nchini, uzalishaji wa sekta ya kilimo kwa jumla ulishuka kutokana na uzalishaji mdogo wa mazao muhimu ya biashara. Kwa jumla, ongezeko dogo katika Pato la Taifa lililopatikana lilitokana na sekta ya huduma hasa uendeshaji wa Serikali. Hivyo uhaba wa bidhaa muhimu na huduma nyingine za kiuchumi na jamii uliendelea na bei ziliendelea kupanda kwa haraka.

### **Pato la Taifa:**

2. Takwimu za awali za mwaka 1985 na zilizorekebisha za mwaka 1984 zinaonyesha kuwa Pato la Taifa katika mwaka 1985 liliongezeka kwa asilimia 2.3 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 3.2 mwaka 1984 kwa bei za mwaka 1976. Japokuwa lipo ongezeko dogo, ongezeko hili silo la kuridhisha kwani pato la sekta karibu zote isipokuwa maji na umeme na huduma za uendeshaji Serikali lilishuka na iwapo ongezeko la mchango wa huduma hizo ukiondolewa, Pato la Taifa kwa jumla lilishuka kwa asilimia 2.0. Tukizingatia mwenendo huu na hali halisi ya maisha ya wananchi, ni dhahiri kuwa pato halisi la wastani la Mtanzania katika mwaka 1985 iliendelea kushuka na lilikuwa pungufu kwa karibu asilimia 11.0 ikilinganishwa na mwaka 1980.

### **Ukuzaji wa Rasilimali:**

3. Katika mwaka 1985, ukuzaji wa rasilimali uliongezeka kwa kiasi kikubwa cha Sh. 1218 milioni kwa bei za mwaka 1976 toka Sh. 4,900 milioni mwaka 1984 hadi Sh. 6,118 milioni mwaka 1985, ongezeko la asilimia 24.9 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 15.7 mwaka 1984. Ingawaje ujenzi wa majengo kwa jumla uliongezeka kidogo kwa asilimia 2.7 na ujenzi wa barabara na shughuli nyingine kushuka kwa asilimia 5.7 kutokana na uhaba wa zana na vifaa vya ujenzi huo, ununuzi wa vifaa, vikiwemo vya usafiri uliongezeka sana toka Sh. 2,574 milioni hadi Sh. 3,758 milioni mwaka 1985, ongezeko la Sh. 1,184 milioni au asilimia 50. Hii lilitokana hasa na kuendelea kulegeza masharti ya uingizaji wa magari ya aina ya pick-up na magari mengine yaliyoingizwa kwa misaada maalum ya kuimarisha Vyama vya Ushirika. Hapakuwapo mabadiliko makubwa katika sehemu nyingine za ukuzaji wa rasilimali.

### **Maendeleo katika Sekta mbali mbali:**

4. Kwa jumla, katika mwaka 1985, maendeleo katika sekta mbali mbali hayakuwa ya kuridhisha. Tofauti na mwaka 1984 ambapo sekta karibu zote isipokuwa viwanda zilikuwa na maongezeko katika mwaka 1985, mchango wa sekta zote isipokuwa Sekta ya maji na nishati na huduma za uendeshaji serikali katika Pato la Taifa ilipungua.

5. Katika mwaka 1985/86 sekta ya kilimo ilionyesha sura mbili tofauti. Mazao ya chakula na hasa mahindi yaliongezeka na kwa upande mwingine uzalishaji wa mazao muhimu ya biashara uliendelea kushuka. Kwa mfano hadi kufikia mwezi Februari 1986 Shirika la Taifa la Usagishaji lilikuwa limenumua jumla ya tani 259,000 za vyakula ikilinganishwa na tani 167,860 mwaka mzima wa 1984/85. Lakini kwa upande wa mazao ya biashara, ni tumbaku na pamba ndizo ziliongezeka. Kutokana na hali hiyo uzalishaji wa sekta nzima ya kilimo ulishuka kwa asilimia 1.6 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 2.6 mwaka 1984.

6. Sekta iliyokuwa na ongezeko kubwa kufiko yote (asilimia 23.1%) ni uendeshaji wa Serikali na huduma nyingine. Ongezeko hili lilitokana hasa na kuimarisha Serikali za Mitaa pamoja na malipo makubwa ya viinua mgongo kwa wafanyakazi zaidi ya waliostaafishwa mwaka 1985. Kwa kifupi, sekta ambazo mchango wake katika Pato la Taifa ulishuka zilikuwa kilimo (asilimia 1.6), madini (asilimia 6.9), viwanda (asilimia 6.4), ujenzi (asilimia 0.9), biashara (asilimia 6.3), fedha (asilimia 0.7), na zile ambazo mchango wake uliongezeka ni umeme na maji (asilimia 5.2) mawasiliano, uchukuzi na maghala (asilimia 0.6) na uendeshaji wa Serikali na huduma nyingine (asilimia 23.1).

### **Biashara na Hali ya Malipo na Nchi za Nje:**

7. Hali ya malipo na nchi za nje iliendelea kuwa mbaya katika mwaka 1985 kwani mauzo ya bidhaa zetu nchi za nje yaliendelea kushuka kutokana na mabadiliko ya mara kwa mara ya thamani ya shilingi hali hiyo hudhahirishwa zaidi kwa kutumia dola ya Marekani ambayo ndiyo sarafu iliyotumiwa katika sehemu hii.

8. Thamani ya mauzo ya bidhaa zetu nchi za nje ilifikia dola 315.6 milioni mwaka 1985 ikilinganishwa na dola 405.1 milioni mwaka 1984 na dola 412.0 milioni mwaka 1983. Katika kipindi hicho, uagizaji wa bidhaa uliendelea kuongezeka na thamani yake ilifikia dola 925.3 milioni ikilinganishwa na dola 762.0 milioni mwaka 1984.

9. Sababu kubwa ya kushuka kwa thamani ya mauzo yetu nchi za nje ni kushuka kwa kiasi (volume) cha bidhaa nyingi hasa mazao ya kilimo kwani katika mwaka 1985/86 ni tumbaku na pamba ndizo ziliongezeka. Uzalishaji wa mazao mengine yote ulishuka. Bei za baadhi ya bidhaa kama kahawa iliyoongezeka haikubadili mwenendo huo. Kwa upande wa kuagiza bidhaa toka nje palikuwepo ongezeko kutokana na kuwaruhusu watu binafsi kuendelea kutumia fedha zao kuagiza bidhaa bila kutegemea Benki Kuu. Bidhaa zilizoagizwa kwa njia hiyo zinakadiriwa kufikia thamani ya dola 120 milioni mwaka 1985. Japokuwa hatua hiyo imesaidia kupunguza kidogo uhaba wa baadhi ya bidhaa za walaji, matatizo ya uzalishaji katika sekta nyingine yaliendelea kutokana na uhaba wa malighafi na vifaa vingine muhimu. Inakadiriwa kwamba ili uchumi uanze kurejeshwa katika hali ya kawaida, kitahitajiwa kiasi kisichopungua dola 1,200 milioni kwa mwaka katika miaka mitatu ijayo ili kufufua uchumi na kiasi hicho itabidi kigawanywe katika sekta muhimu.

10. Kutokana na hali ngumu ya fedha za kigeni katika mwaka 1985, malimbikizo ya madeni yaliongezeka na kufikia Desemba 1985, kiasi hicho kilifikia dola 700 milioni. Kwa kutazama vigezo vingine muhimu, urari wa huduma ulikuwa na ziada ya dola 1.2 milioni ikilinganishwa na dola 26.0 milioni mwaka 1984. Urari wa uhamisho wa mali ulikuwa dola 122.5 milioni na urari wa malipo yote unaojumlisha urari wa bidhaa, huduma uhamisho wa mali na urari wa rasilimali ulikuwa na nakisi ya dola 190.0 milioni ikilinganishwa na dola 131.0 milioni mwaka 1983.

#### Mapato na Matumizi ya Serikali:

11. Kama ilivyokuwa katika mwaka 1984/85, mwenendo wa mapato na matumizi ya Serikali hautabadilika sana japokuwa pengo katika bajeti ya kawaida linategemewa kuwa kubwa zaidi. Mapato ya kawaida katika mwaka 1985/86 yanatarajiwa kufikia Sh. 21,975.1 milioni badala ya makadirio ya Sh. 19,912 milioni. Katika mwaka 1984/85 mapato yalikuwa Sh. 19,143 milioni. Matumizi ya kawaida yalipangwa kuwa Sh. 23,360.0 milioni lakini maturajio ifikapo mwisho wa Juni, 1986 ni kwamba kiasi cha Sh. 25,604.3 milioni kitakuwa kimetumika ambacho ni asilimia 9.3 zaidi ya makadirio. Katika mwaka 1984/85, Sh. 21,336.5 milioni zilitumika.

12. Mapato yanatarajiwa kuvuka makadirio kutokana hasa na ongezeko katika kodi ya mapato ambayo ilikadiriwa kuwa Sh. 4,260 milioni na maturajio ni Sh. 5,947.1 milioni, ongezeko la Sh. 1,687.1 milioni au asilimia 39.6. Hapatarajiwi kuwapa mabadiliko makubwa katika vianzo vingine. Kwa upande wa matumizi ya kawaida mategemeo ni kwamba yatavuka makadirio kutokana na udhibiti hafifu wa matumizi pamoja na upandaji wa bei za baadhi ya bidhaa na huduma muhimu.

13. Bajeti ya Maendeleo ilielekea kukabiliwa na matatizo ya upungufu wa fedha za kigeni kwani licha ya uhaba wa fedha hizo kwa miradi tunayogharimia sisi wenyewe, hata miradi inayogharimiwa kwa fedha kutoka nje ilikabiliwa na matatizo ya kutokupata fedha hizo kwa wakati uliotakiwa. Matatizo yake ni kwamba japokuwa maturajio ni kutumia Sh. 5,940 milioni ikilinganishwa na makadirio ya Sh. 6,828 milioni, fedha nyingi za hapa zimetumika kuliko makadirio wakati ambapo fedha kuroka nje zimetumika kidogo zaidi. Kwa mfano katika jumla ya Sh. 6,828 milioni zilizokadiriwa, Sh. 3,404 milioni zilikuwa fedha za hapa na maturajio ni kutumia Sh. 3,837 milioni wakati ambapo katika makadirio ya Sh. 3,428 milioni za fedha kutoka nje, ni Sh. 2,083 milioni ndizo zitakuwa zimetumika ifikapo Juni, 1986.

#### Ujazi wa Fedha na Bei:

14. Mwaka 1985/86, uwiano baina ya ukuaji halisi wa uchumi na ongezeko katika ujazi wa fedha ulielekea kuvurugika. Ingawa katika mwaka 1984 Pato halisi liliongezeka kwa asilimia 3.2 na mwaka 1985 kwa asilimia 2.3, ujazi wa fedha uliongezeka kwa asilimia 18.2 mwaka 1984/85 na unategemewa kuongezeka kwa asilimia 27.3 kati ya Juni, 1985 na Juni, 1986. Hali hiyo inaeleza kwa kiasi kikubwa ongezeko la haraka la bei kwani uzalishaji halisi umeendelea kuwa chini sana ukilinganisha na kiasi kikubwa cha ongezeko la fedha katika uchumi.

15. Ongezeko kubwa la ujazi wa fedha ulielekea kutokana na mikopo mikubwa toka mabenki kufidia pengo katika Bajeti ya Serikali. Mwaka 1985/86, maturajio ni kwamba ifikapo Juni, 1986 mikopo hiyo itakuwa imefikia Sh. 5,778.3 milioni ikilinganishwa na makadirio ya Sh. 5,200 milioni na vile vile kiwango cha Sh. 3,935.6 milioni mwaka 1984/85. Mikopo kwa sekta nyingine inatarajiwa kufikia Sh. 3,400 milioni kutokana na mahitaji makubwa ya karadha kwa ununuzi wa mazao na pia kwa mahitaji makubwa ya sekta nyingine na upandaji haraka wa bei. Makadirio yalikuwa Sh. 1,100 milioni. Kwa jumla karadha katika uchumi ilifikia Sh. 9,178.3 milioni na ikijumliwa na mabadiliko katika akiba ya fedha za kigeni, ujazi wa fedha kwa jumla uliongezeka kwa Sh. 5,795.7 milioni ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 27.3. Katika mwaka mzima wa 1984/85, ujazi wa fedha uliongezewa kwa asilimia 21.1.

16. Bei kwa jumla ziliendelea kuwa za juu katika mwaka 1985 ingawaje ile kasi ya kupanda ilipungua kidogo ikilinganishwa na mwaka 1984. Kwa kutumia fahirisi ya bei za wakazi wa mijini Tanzania Bara (CPI), katika kipindi cha kati ya Januari na Desemba, 1985 bei zilongezeka kwa asilimia 28.2 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 42.9 katika kipindi kama hicho mwaka 1984. Ongezeko kubwa la 1984 lilitokana na kuondolewa ruzuku na kupandisha baadhi ya viwango vya kodi ya mauzo. Bei za bidhaa nyingi hasa vyakula, nguo na vianzo vya nishati kama umeme, kuni n.k. ziliendelea kupanda kwa haraka mwaka 1985. Sababu muhimu za maongezeko haya zilikuwa uhaba wa bidhaa muhimu mijini hasa chakula kwa sababu ya kukosekana njia za kutosha za uchukuzi kutokana na uhaba mkubwa wa mafuta ya petroli hasa katika robo ya nne (Oktoba—Desemba) ya mwaka na pia kutokana na ongezeko la gharama za uzalishaji baada ya kuongeza viwango vya malipo ya umeme mapema mwaka 1985.

#### Hali ya Uchumi Duniani na Ushirikiano Kimataifa:

17. Hali ya uchumi duniani katika mwaka 1985 ilikuwa ya mchanganyiko. Kwa nchi zilizoendelea, Pato la Taifa (GNP) la nchi hizo kwa jumla liliongezeka kwa asilimia 3.2 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 4.6 mwaka 1985. Uzalishaji katika nchi zinazoendelea uliongezeka kidogo kwani Pato la Taifa (GDP) liliongezeka kwa asilimia 3.3 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 2.9 mwaka 1984. Bei ziliendelea kupanda kwa kasi kwa nchi zinazoendelea kinyume na nchi zilizoendelea ambako ongezeko la bei za walaji (CPI) kwa wastani liliendelea kupungua kufikia asilimia 4.2 mwaka 1985 ikilinganishwa na asilimia 5 mwaka 1984.

18. Ongezeko katika biashara kwa jumla lilikuwa dogo la asilimia 3.3 mwaka 1985 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 6.6 mwaka 1984. Sababu muhimu za ongezeko hili dogo zilikuwa kushuka kwa bei ya mafuta ya petroli na hivyo kupungua mapato ya nchi muhimu zinazotoa mafuta, kushuka kwa bei za bidhaa nyingi asilia (primary commodities) na kuendelea kupanda kwa bei za bidhaa za viwanda zinazoagizwa toka nchi za nje. Hali hii iliongeza malimbikizo ya madeni kwa nchi zinazoendelea na kupunguza uwezo wao wa kuagiza bidhaa kwa maendeleo ya uchumi wao. Madeni ya nchi zinazoendelea yalikuwa kufikia dola 970 bilioni katika mwaka 1985 na katika jumla hiyo madeni ya Afrika ni dola 170 bilioni.

19. Hatua za Mashirika ya Fedha ya Kimataifa kuanzisha mfuko maalumu ya kusaidia nchi masikini zilianza kutoa matunda. Mfuko maalum wa Benki ya Dunia kwa nchi zilizo kusiwa Sahara (Special Assistance Facility for Sub-Saharan Africa), ulianza kutumika mwaka 1985. Vile vile Mfuko mwingine maalumu wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) litwalo "Structural Adjustment Facility" unategemewa kuwa na kiasi cha SDR 2.7 bilioni katika kipindi cha 1985—89 umeshaanza kutoa mikopo hiyo nafuu kwa nchi zinazofanikiwa kupata mikopo ya kawaida toka mashirika hayo. Hata hivyo ni muhimu kuzingatia ukweli kuwa japokuwa kiasi kilichotengwa katika mfuko hiyo hakitoshelezi mahitaji ya nchi masikini, masharti ya kupata fedha, hizo vile vile bado magumu.

20. Katika nyanja nyingine za ushirikiano, mkataba wa Lomé III sasa unatekelezwa na Tanzania itapata ECU 169 milioni (Sh. 2,130 milioni) kuendeleza miradi ya sekta za kilimo na Mawasiliano. Nyanja nyingine za ushirikiano katika kutekeleza mkataba huo bado zinajadiliwa. Shughuli za ushirikiano baina ya nchi zilizo kusiwa Sahara la Afrika SADCC na Soko nafuu la Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika, PTA ziliendelea kuimarishwa. Tokeo lingine muhimu katika kipindi hiki lilikuwa Maandalizi ya Mkutano maalumu wa Umoja wa Mataifa chini ya usimamizi wa OAU na ECA utakaofanyika New York tarehe 27—31 Mei, 1986. Mkutano huu una lengo la kujadili Mpango wa kufufua uchumi wa nchi za Afrika unatarajiwa kugharimu dola 116.9 milioni katika kipindi cha 1986—90. Dola 81.1 bilioni zitatolewa na nchi za Afrika zenyewe na dola 35.8 bilioni zitakuwa misaada toka nje.

## SURA YA PILI

### UTEKELEZAJI WA MPANGO WA 1985/86

1. Makadirio ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 1985/86 yalipangwa kuwa sh. 6,829 milioni ikilinganishwa na sh. 6,540 milioni kwa mwaka wa fedha uliopita, na kufanya ongezeko la sh. 269 milioni au asilimia 4. Ongezeko hilo ni dogo mno ikilinganishwa na mahitaji halisi ya fedha kwa stughuli za maendeleo na hasa ikitiliwa maaanani uongezekaji wa bei na miradi mingi viporo ambayo ilibidi itengewe fedha ili kuikamilisha au kuiendeleza.

2. Kati ya sh. 6,828 milioni zilizo idhinishwa na Bunge, sh. 3,402 milioni au asilimia 49.8 ni fedha za humu nchini (local funds) na sh. 3,427 milioni au asilimia 50.2m msaada na mikopo kutoka nje (foreign grants and loans). Kwa upande wa fedha za nje, sh. 1,052 milioni au asilimia 30,7 ya fedha hizo ni mikopo na sh. 2,375 milioni au asilimia 69.3 ni msaada. Kiasi kikubwa cha fedha za nje na mikopo kimeelekezwa kugharamia sekta za uzalishaji moja kwa moja (directly productive) pamoja na huduma za kiuchumi (economic infrastructure) wakati kiasi kikubwa cha fedha za msaada kimeelekezwa kwenye sekta ya huduma za kijamii.

3. Kama ilivyo kawaida, fedha zote za nje zilifanywa katika mafungu matatu makubwa. Kati ya fedha hizo za nje za kiasi cha sh. 3,427 milioni, sh. 210 milioni au asilimia 6.1 ni fedha rasimu ambazo huingizwa nchini (C-cash disbursement), sh. 287 milioni au asilimia 8.3 ni zile ambazo kwanza lazima tutumie fedha zetu za humu nchini na baadaye kuomba kurudishiwa na wahesani mbali mbali (R-reimbursable disbursement) na sh. 2,930 milioni au asilimia 85.6 ni zile ambazo zimelipwa moja kwa moja kwenye mradi kwa njia ya kugharamia vifaa, zana, utaslam na huduma (D-direct to project disbursement). Ni dhahiri kwamba kiasi kikubwa cha fedha za nje kimetengwa chini ya fungu la D.

4. Idadi ya miradi iliyoidhinishwa kutekelezwa katika kipindi cha 1985/86 ilikuwa 3,494. Kati ya miradi hii, miradi 1,068 ni ya kitaifa na miradi 2,426 ni ile ya mkoa pamoja na wilaya. Kuanzia mwaka wa fedha 1983/84, kumekuwapo na ongezeko kubwa la idadi ya miradi. Ongezeko hili limetokana na miradi midogo midogo ya wilaya na mji ambayo mingi inafanana na kurudiwa mwaka hadi mwaka. Ongezeko limesababishwa na urejeshaji wa Serikali za Mitaa ambapo kila wilaya au mji unakuwa na miradi yake badala ya kuwa na miradi mmoja wa mkoa ambao unatekelezwa kwa kila wilaya inayohusika. Kabla ya kurejesha Serikali za Mitaa, wasiani wa jumla ya miradi iliyokuwa inadhinishwa na Bunge ilikuwa haiyuki kiwango cha miradi 200 hivi na mgawanyo wa miradi hiyo kati ya ile ya kitaifa na ya mkoa, kiidadi ulikuwa hautofautiani sana kama ilivyo sasa.

5. Mwelekeo wa matumizi ya fedha kwa kuzingatia matumizi ya miezi sita ya kwanza unaonyesha kwamba matumizi yanatarajiwa kufikia sh. 5,940 milioni ifikapo Juni 1986. Hii ni asilimia 87 ya makadirio ya 1985/86. Upungufu huo wa sh. 888 milioni unatokana hasa na matumizi kidogo ya fedha za nje. Inatarajiwa kwamba matumizi ya fedha za humu nchini yatavuka makadirio kwa sh. 410 milioni wakati kwa upande wa fedha za nje, matumizi yanatarajiwa kuwa pungufu kwa sh. 1,378 milioni.

6. Katika nusu ya kwanza ya 1985/86, miradi mingi iliendelea kukabiliwa na matatizo kadhaa ya utekelezaji hasa uhaba wa vifaa na zana za kutekeleza miradi (project inputs). Tatizo hili si geni kwa kuwa limekuwapo mwaka hadi mwaka. Sababu mojawapo ya tatizo hili kuendelea ni kwamba hakuna uwiano kati ya miradi inayoidhinishwa kutekelezwa na upatikanaji wa vifaa na zana ambazo zingeweza kufanikisha utekelezaji wa miradi hiyo. Hali kadhalika kuna baadhi ya matatizo ambayo yanatokana na upungufu mkubwa wa petroli na dizeli ambao ulikumba nchi hasa katika robo ya pili pamoja na ukatikaji wa mara kwa mara wa maji na umeme ambao ulisababisha uzalishaji mdogo wa zana na vifaa vinavyohitajika katika utekelezaji wa miradi. Pale ambapo zana na vifaa vichache vililweza kupatikana, vilicheleweshwa au kutowasilishwa kabisa kwenye sehemu za miradi kwa sababu ya upungufu wa petroli na dizeli ulioelezwa hapo juu pamoja na uhaba wa matairi, vipuri vya magari n.k. na hali mbaya ya barabara. Tatizo jingine ni lile la uhaba wa fedha za kigeni kwa miradi ambayo kutekelezwa kwake kulihitaji fedha za aina hiyo.

7. Kutokana na matatizo hayo ya utekelezaji inatazamiwa kwamba matumizi ya fedha yatafikia asilimia 87 na utekelezaji halisi (physical implementation) unakisiwa kuwa asilimia 41 hivi. Hali ya kuwa na matumizi makubwa ya fedha wakati utekelezaji halisi ni mdogo inaanza kuonekana kuwa ni ya kawaida na inatokana na sababu kadhaa zikiwemo maamuzi mbali mbali ya Serikali kama vile upandishaji wa bei za vifaa na zana za miradi, ucheleweshaji wa kutekeleza miradi ambao matokeo yake ni uongezekaji wa gharama za miradi (cost overruns), makadirio ya gharama za miradi yasiyo sahihi yakiambatana na usimamizi dhifu na kupuuzia viwango vya gharama (standard costs) vinavyotokana na michoro maalum (standard designs). Haya yote yamesababisha matumizi makubwa ya fedha wakati utekelezaji halisi ni mdogo. Kuna haja ya kuimarisha usimamizi wa utekelezaji miradi ili angalau matumizi ya fedha yalinganelingane na hali halisi ya utekelezaji.

## SURA YA TATU

### MISINGI YA MPANGO 1986/87—MPANGO WA KUFUFUA UCHUMI 1986/87—1988/89

1.1 Jitihada za kutanzua matatizo na kurekebisha hali ngumu iliyoukumba uchumi tangu mwaka 1979 zimekuwa zikifanywa na Taifa. Msukumo mkubwa ulifanywa mwaka 1980/81 wakati Serikali ilipoandaa Mpango wa Kujibami Kiuchumi wa mwaka 1981, na 1982. Mpango huo ulimarishwa zaidi na Mpango wa Kurekebisha Uchumi wa 1982/83—1984/85. Japokuwa mafanikio ya Mpango miwili hiyo ya kurekebisha uchumi hayakufanikiwa vyema katika kutanzua matatizo ya kimsingi ya uzalishaji mdogo uhaba wa fedha za kigeni, upandaji haraka wa bei na uzorotaji wa rasilimali za Taifa, hata hivyo, ilikuwa imeandaliwa chini ya misingi mizuri. Kwa kuzingatia pia hatua za kibajeti zilizochukuliwa mwaka 1983/84, na hasa mwaka 1984/85 misingi ya Mpango iliyopita ya kurekebisha uchumi imetumika katika kuandaa Mpango wa Kufufua Uchumi.

1.2 Mpango wa Kufufua Uchumi unaendeleza, kuimarisha na kuzidisha msukumo wa sera zilizopo na zinazokubalika. Pamoja na hayo, Mpango unatambua kwamba matumaini ya kupata misaada mikubwa katika kipindi kilichosalia cha miaka ya Themanini ni madogo sana. Hivyo, tatizo la uhaba wa fedha za kigeni litaendelea. Hii inamaanisha kwamba hatua zitaendelea kuchukuliwa katika sekta ya nje kuzuia upotevu na kuimarisha matumizi bora ya rasilimali. Pia msukumo utakuwa kuelekea rasilimali katika kuongeza uzalishaji mashambani kwa wakulima wadogo wadogo kwa kutambua ya kwamba mafanikio makubwa zaidi yatatokana na kutumia rasilimali haba tulizonazo katika mipango inayolenga wakulima wadogo na vijijini. Kupanua shughuli za kiuchumi vijijini kutahamasisha wananchi kujiongeza maisha bora.

1.3 Malengo: Malengo ya Mpango ni kama ifutavyo.

- (i) Kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na ya biashara kwa kutumia motisha sahihi za uzalishaji, kuongeza ufanisi na kuimarisha ununuzi na uuzaji wa mazao, na kuelekea rasilimali zaidi kwenye kilimo.
- (ii) Kufufua huduma za kiuchumi nchini ili zisaidie shughuli za uzalishaji. (To rehabilitate the physical infrastructure of the country in support of directly productive activities).
- (iii) Kuongeza matumizi ya uwezo wa viwanda vilivyopo na kurudhisha tena ongezeko halisi la pato la taifa linalotokana na viwanda (to increase capacity utilization in industry and restore positive industrial GDP growth).
- (iv) Kurudhisha tena urari wa ndani na wa nje katika uchumi kwa kufuata na kuzingatia sera sahihi za bajeti, fedha na biashara (to restore internal and external balances in the economy by pursuing prudent and appropriate fiscal, monetary and trade policies).

1.4 Mpango umetayarishwa kwa kutambua na kuzingatia kwamba matatizo ya uchumi yaliyopo ni "structural" na kwamba kuondoa vikwazo vya uzalishaji na kuweka misingi ya kuwezesha uchumi kujiendeleza wenyewe ni masuala ya upeo wa kati na upeo mrefu. Kwa sababu hizo na ili kufanikisha malengo ya Mpango, Serikali itachukua hatua za kisera zilizobuniwa kuongeza uzalishaji na uwekaji na kuongeza ufanisi wa matumizi ya rasilimali zilizopo ili kuimarisha ukuaji wa uchumi kwa jumla na hasa wa mauzo nje.

#### Msukumo wa Sera.

1.5 Msukumo katika Mpango utaelekezwa kwenye maeneo ya sera za kiuchumi kwa jumla na sera za kiuchumi kissekta zenye matumaini ya kufufua uchumi.

1.5.1. Sera za Kiuchumi za Kijumla (macro-economic policies): Hatua zitakazochukuliwa zitakuwa na lengo la kutoa motisha ya kutosha kwa wakulima na wazalishaji wengine; kupunguza nakisi kati ya mahitaji na upatikanaji vitu toka ndani na nje ya nchi; na vile vile kupunguza "inflationary pressures". Sera muhimu zinazohusu Bei za Wakulima, Viwango vya ubadilishaji wa Sarafu, bajeti na fedha, biashara ya ndani na ya nje.

- (i) Bei za Wakulima: Bei za wakulima zitazingatia mfumo wa SAP, yaani zitaongezwa kwa asilimia 5 halisi (real), au wakulima watalipwa asilimia 70 ya bei za dunia za mazao kutegemea nilipi kubwa kati ya hizo mbili.
- (ii) Kiwaango cha Ubadilishaji wa Sarafu: Kutakuwa na mapitio ya mara kwa mara ya sera ya viwango vya kubadilishana sarafu ili kuimarisha mauzo nje na kuwezesha kulipa bei nzuri wakulima na wauzaji nje bila kutegemea ruzuku ya Serikali.
- (iii) Bajeti: Kuendelea na juhudi za kupunguza na kubana matumizi, kuongeza ufanisi katika sekta ya Umma, na kuongeza mapato.
- (iv) Fedha: Kuwa na sera sahihi za bajeti na kuzuia ongezeko lisilostahili la ujazi wa fedha.
- (v) Biashara ya Ndani: Kuendeleza na kuimarisha ufanisi katika taratibu za biashara ya ndani.
- (vi) Biashara ya nje: Kuimarisha hatua za kuwianisha (rationalize) biashara ya nje na kuongeza mauzo nje;

1.5.2. Sera za Kissekta: Hatua hizi zina lengo la kushughulikia masuala mbali mbali katika sekta muhimu ili kuongeza ufanisi na kuimarisha "the recovery momentum". Kwa mfano:—

- (i) Kilimo—kuwianisha na kuimarisha (rationalization) uuzaji na ununuzi wa mazao ya chakula, kusukuma mauzo nje; kuongeza ubora wa huduma za kitaalam (extension services).
- (ii) Viwanda—kuongeza matumizi ya uwezo wa viwanda, kujenga msingi wa malighafi ya humu nchini.
- (iii) Transport ku-"revamp" njia muhimu za usafiri ili kuongeza ufanisi na uwezo wa uchukuzi.
- (iv) Nishati—kuendeleza vyanzo vyenye gharama nafuu hasa vya humu nchini.
- (v) Maliasili—Kuvuna ama kutumia kwa madhumuni ya kupata fedha za kigeni.

#### 1.6. Mahitaji ya Mpango kwa kipindi cha miaka mitatu, 1986/87—1988/89:

Mpango wa Kufufua Uchumi imekadiriwa kugharimu \$4,568 milioni. Kati ya hizo, \$831 milioni ni nyongeza ya gharama za ndani (Tshillings) na zilizobakia \$3,737 milioni, ni jumla ya fedha za kigeni zitakazohitajika (Minimum Import Requirements component). Mgawanyo wa gharama hizo ni kama ifuatavyo:

(US \$ Million)

	1986/87		1987/88		1988/89	
	Local	Foreign	Local	Foreign	Local	Foreign
Investment Rehabilitation	302	443	280	418	249	407
Recurrent	—	763	—	813	—	893
<b>Jumla</b>	<b>302</b>	<b>1,206</b>	<b>280</b>	<b>1,231</b>	<b>249</b>	<b>1,300</b>

#### Investment:

Kwa ujumla hii ni Bajeti ya Maendeleo ya Serikali. Miradi inayojumuishwa ni ile ambayo imekwishaanzishwa na inaendelea. Miradi mipya ni ile tu ambayo itaongeza mauzo nje au itapunguza vikwazo vya kutumia uwezo wa kuzalisha uliopo.

#### Rehabilitation:

Hizi ni gharama za kufanya marekebisho na matengenezo makubwa na muhimu katika sekta hesa za Kilimo, viwanda, Uchukuzi na Mawasiliano, Maji, na Nishati.

#### Recurrent:

Haya ni matumizi kwa ajili ya ununuzi wa malighafi za viwanda, vipuri vya aina mbali mbali na bidhaa muhimu zisizozalishwa humu nchini.

### 1.7. Mifano ya mipango iliyopo chini ya kila kifungu cha Mpango wa Kufufua Uchumi ni kama ifuatavyo:

#### 1.7.1. Investment:

- Kilimo:**—matumizi ya kiasi cha \$159 milioni yana kusudi la kupanua uzalishaji wa vyakula na mazao ya biashara. Miradi inayohusika ni pamoja na ya umwagiliaji maji, utafiti wa mazao na huduma kwa wakulima, uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula muhimu k.m. mahindi, mpunga, ngano na sayiri ili kupunguza uagizaji wa nafaka nje na kuimarisha lengo la kujitosheleza. Mazao ya biashara yatashughulikiwa chini ya miradi ya "Crop Packages" ambayo inasisitiza kutekeleza kwa pamoja sera zinazolenga kuongeza uzalishaji wa kila zao ili uuzaji wa mazao nje ukue kwa wastani wa asilimia 9 kwa mwaka.
- Viwanda:**—Kwa kutumia kiasi cha \$101 milioni lengo litakuwa kuongeza uwezo wa uzalishaji kutoka viwango vya sasa vya kati ya asilimia 20 na 30 hadi asilimia 60. Miradi itahusu kuendeleza upatikanaji wa malighafi za nchini na kukamilisha miradi inayoendelea, ili kuzalisha pembejeo muhimu za sekta nyingine na bidhaa za matumizi muhimu.
- Mawasiliano:**—Miradi inayohusika ni ile inayoendelea ambayo ni pamoja na ujenzi wa maharabara, upanuzi wa magati, uimarishaji wa vifaa vya mawasiliano na katika viwanja vya ndege; na ujenzi wa maghala. Miradi yote inakadiriwa kugharimu kiasi cha \$265 milioni.
- Maji na Nishati:**—Lengo litakuwa kupunguza uagizaji wa mafuta ya petroli na kuimarisha upatikanaji wa nishati na maji kwenye sekta muhimu. Miradi muhimu chini ya sekta hii ni pamoja na kusambaza umeme unaotokana na maporomoko ya maji kwenye mikoa mingine, uendelezaji wa vyanzo vingine vya nchini vya nishati na uimarishaji wa huduma za maji.
- Sekta Nyinginezo:**—Lengo litakuwa uimarishaji katika sekta za uchimbaji madini, ujenzi na huduma za kijamii.

#### 1.7.2. Rehabilitation:

- Kilimo:**—shughuli zitakazopewa msukumo wa juu ni matengenezo ya zana, maghala na udhibiti hasa wa mazao muhimu. Gharama zinakisiwa kuwa kiasi cha \$166 milioni kila mwaka.
- Viwanda:**—Matarajio ni kwamba shughuli ya kufufua viwanda vilivyopo itakuwa zaidi katika kipindi cha mwaka wa kwanza wa Mpango; na kwa gharama ya kiasi cha \$43 milioni.
- Mawasiliano:**—shughuli zitakuwa hasa kufufua zana za ujenzi, mashine za kukokota mchanga na karakana kwa kuzipatia vipuri na vifaa vingine muhimu kwa gharama inayokisiwa kuwa \$60 milioni.

#### 1.7.3. Recurrent:

- Kilimo:**—Kitahitaji kiasi cha \$427 milioni kununulia pembejeo muhimu; k.m. mbolea, madawa, vifaa vya kulimia, vyakula na magunia.
- Viwanda:**—Vitahitaji wastani wa \$151 milioni kila mwaka kununulia malighafi, vipuri na vifaa muhimu kwa ajili ya viwanda muhimu.
- Mawasiliano:**—Kiasi cha \$326 milioni zitahitajika kununulia vipuri na vifaa muhimu katika sekta ya mawasiliano na uchukuzi.

## B. MPANGO WA FEDHA NA KARADHA

### Mapitio ya Mwaka 1985/86

2.1 Katika jumla ya Sh. 30,198 milioni zilizokadiriwa kama bajeti ya Serikali mwaka 1985/86 Sh. 23,360 milioni zilihusu matumizi ya kawaida; na Sh. 6,829 milioni zilikuwa zimekisiwa kukidhi matumizi ya maendeleo. Kwa upande mwingine, mapato halisi yalikuwa kufikia jumla ya Sh. 24,989 milioni zikiwa ni pamoja na Sh. 19,912 milioni za mapato ya kawaida; na Sh. 5,077 milioni za mapato ya maendeleo. Pengo la kuzibwa kutokana na mikopo ya mabanki lilikadiriwa kuwa la kiasi cha Sh. 5,200 milioni sawa na makadirio ya mwaka 1984/85.

2.2 Matarajio ya bajeti ya Serikali kwa mwaka 1985/86 kwa kuzingatia mwenendo halisi hadi kufikia Machi, 1986, na matazamio katika robo ya mwisho ya mwaka, ni kama ifuatavyo:

- Bajeti kwa ujumla itaongezeka kwa Sh. 3,129 milioni au asilimia 10.4 kutoka Sh. 30,189 milioni zilizokadiriwa hadi Sh. 33,318 milioni.
- Mapato pia yataongezeka kwa asilimia 4.0 sawa na Sh. 777 milioni kutoka Sh. 24,989 milioni za makadirio hadi Sh. 25,766 milioni zinazotarajiwa.
- Matarajio hayo ya bajeti yanaacha pengo la kiasi cha Sh. 7,552 milioni ambalo litabidi lizibwe kwa kutumia mikopo ya mabanki. Tegemeo la kuwa na pengo la Sh. 7,552 milioni katika bajeti linazidi makadirio kwa kiasi cha Sh. 2,352 milioni au asilimia 45.2.

2.3 Maana halisi ya matarajio ya matokeo hayo katika bajeti ni kama ifuatavyo:

- Mapato halisi yataongezeka kwa kiasi cha Sh. 777 milioni au asilimia 4.0 zaidi ya makadirio. Ongezeko hilo linatokana na ongezeko la Sh. 2,063.1 milioni sawa na asilimia 10.4 katika mapato ya kawaida hasa kodi ya mapato kodi ya leseni za biashara ushuru wa stempu na ushuru wa viwanda vya ndege pamoja na kodi mpya za "road tolls" na "payroll levy" zilizoanzishwa Julai, 1985. Vianzio vikuu vya mapato havioneshi dalili za kuongezeka zaidi ya viwango vilivyokadiriwa. Kwa mfano, mapato yatokanayo na ushuru wa forodha na kodi ya mauzo kwa bidhaa zinunuliwazo nje huenda yakabakia katika viwango vilivyokisiwa ambavyo ni chini kidogo ya mapato ya mwaka 1984/85, pengine kwa kuwa shauku ya kuagizia bidhaa nje imepungua na kwamba shehena za nyuma bado zipo madukani. Kwa upande mwingine mapato ya maendeleo yatapungua kwa kiasi kikubwa cha Sh. 1,286 milioni au asilimia 25.3 kutokana na kutokuweza kupata misaada kutoka nje kwa wakati uliotarajiwa.



- (b) Matumizi yatakuwa na jumla ya ongezeko la Sh. 3,129 milioni au asilimia 10.4. Katika jumla hiyo matumizi ya kawaida yataongezeka kwa asilimia 17.2 au Sh. 4,018 milioni. Nyongeza imetokana na mafungu matatu ya matumizi yaani Mfuko Mkuu wa Matumizi, Wizara na Tawala za Mikoa. Nyongeza ya Sh. 517.6 milioni au asilimia 9.0 katika Mfuko Mkuu wa matumizi inatokana na kupanda kwa viwango vya riba (kwa dhamana za Serikali); kulipa mikopo mingi iliyo-  
 pevuka na kuongezeka kwa malipo ya viinua mgongo na malipo ya uzeeni kutokana na zoezi la Serikali kupunguza watu-  
 mishi. Wizara na Tawala za Mikoa zimevuka viwango vya matumizi vilivyokadiriwa kwa kiasi cha Sh. 2,511 milioni au asilimia 23.7 na Sh. 277.9 milioni au asilimia 19.1. Vifungu hivi vimevuka viwango vya matumizi kutokana na kukimu magari na kuongezeka kwa gharama za vyakula mashuleni, katika hospitali, kwenye mgereza na majeshi, kuongezeka kwa gharama za uendeshaji hasa kufuatia kupanda haraka kwa bei nchini na kukamilika kwa baadhi ya miradi ya maen-  
 -leleo. Katika fungu la Wizara baadhi ya kasma zilizovuka sana viwango vya matumizi zilizowekewa awali ni Ngome, Usalama, Elimu, Ofisi ya Rais, Nje, Mawasiliano, JKT na Kilimo. Kuhusu bajeti ya maendeleo matumizi ya miradi yanategemewa kupungua kwa asilimia 13.0 au Sh. 889 milioni kutokana na matatizo ya upatikanaji kwa wakati fedha za kigeni kutokana na masharti yake ya mzunguko na urasmi mwingi; na vile vile uhaba wa fedha za kigeni kwa ile miradi tunayogharamia sisi wenyewe. Kwa upande mwingine fedha za nchini zimeongezeka kwa kiasi cha Sh. 322.8 milioni au asilimia 9.5. Mambo yaliyosababisha ongezeko hilo katika matumizi ya maendeleo ni pamoja na upandaji haraka wa bei nchini na udhibiti dhifu wa miradi.

### 3. Makisio ya Fedha na Karadha Mwaka 1986/87

- 3.1 Shabaha katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka 1986/87 zitakuwa kuendeleza jitihada za kurudisha uwiano wa kifedha katika uchumi na kati ya fedha na uchumi halisi. Ili kutekeleza shabaha hizo mbinu zifuatazo zitatumika:—
- (a) Bajeti ya Serikali: Dhamira itakuwa kuzidisha jitihada kufuatilia upatikanaji wa mapato kwa upande mmoja; na kuzuia maongezeko yasiyo ya lazima ya matumizi. Hivyo;
- (i) Mapato ya kawaida yanakadiriwa kuongezeka na kufikia Sh. 35,011 milioni; ambapo
  - (ii) matumizi ya kawaida yanakisiwa kuwa 39,736 milioni;
  - (iii) Matumizi ya maendeleo yanatarajiwa kuwa Sh. 15,860 milioni;
  - (iv) Ununuzi wa dhamana za Taifa wa watu binafsi, Makampuni na mashirika yasiyo ya kibenki unakisiwa kufikia Sh. 2,143 milioni.
  - (v) Mikopo ya Serikali kutoka mabanki itakuwa kiasi cha 2,500 milioni. Jedwali Na. 1 linaonyesha muhtasari wa fedha za Serikali katika miaka 1985/86—1987/88. Na. Jedwali Na. 2 linaonyesha ununuzi wa dhamana za Taifa katika miaka 1983/84—1986/87.
- (b) Ujazi wa Fedha na Kuongezeka kwa Karadha. Lengo litakuwa kuendeleza jitihada kupunguza maongezeko yasiyostahimilika ya ujazi wa fedha hasa kwa kuzingatia hisia zifuatazo:
- (i) Maongezeko ya mikopo ya mabanki kwa Serikali yanakadiriwa kuwa Sh. 2,500 milioni.
  - (ii) Karadha za mabanki kwa sekta nyinginezo zinakisiwa kuongezeka kwa kiasi cha Sh. 1,220 milioni.
  - (iii) Jitihada zitaendelezwa kuimarisha akiba ya fedha za kigeni angalau kwa kiwango cha kukabili matumizi muhimu na ya dharura;
  - (iv) Kwa pamoja karadha itakuwa na ongezeko la jumla ya asilimia 17.
  - (v) Na kwa jumla ongezeko la ujazi wa fedha litakuwa katika kiwango cha asilimia 11.0. Jedwali Na. 3 linaonyesha mwendo wa ujazi wa fedha na maongezeko ya karadha kwa mwaka 1982—1987.

MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI

Jedwali Na 1.

(Shilingi Million)

	1981/82	1982/83	1983/84	1984/85	1984/85	1985/86		1986/87	
	Halisi	Halisi	Halisi	Makisio	Mategemeo (1)	Makisio	Mategemeo	Makisio	
<b>I.—BAJETI YA KAWAIDA:</b>									
<b>I. Mapato ya Kawaida</b>									
1.1. Mapato yato'kanayo na kodi	10,960-00	13,145-00	15,464-60	15,028-70	19,143-00	19,912-00	21,975-10	24,554-00	
1.1. 1. Kodi ya Forodha	9,229-0	10,752-00	13,564-50	12,910-70	17,254-50	17,302-00	19,515-80	20,461-00	
1.1. 2. Kodi ya Bidhaa zilizwa'zo Nje	675-00	743-00	959-00	735-00	1,531-40	1,491-00	1,490-90	1,500-00	
1.1. 3. Kodi ya Mauzo (Ndaoni)	29-00	19-00	12-00	10-00	14-20	-00	8-40	-00	
1.1. 4. Kodi ya Mauzo (Nje)	5,092-00	6,307-00	7,6-80	8,287-80	8,878-30	9,268-00	9,429-00	9,860-00	
1.1. 5. Kodi ya Mapato	-00	-00	-00	-00	1,275-60	124-00	1,248-00	1,370-00	
1.1. 6. Nyingine...	209-00	455-00	761-70	701-40	877-20	1,010-00	1,392-40	1,460-00	
1.2. Mapato yasiyotokana na kodi	1,731-00	2,993-00	1,901-10	2,118-00	1,888-10	2,610-00	2,459-30	4,223-00	
1.2.1. Kasma Na. 50	-00	-00	129-10	330-00	170-50	300-00	149-20	1,919-00	
1.2.2. Misada ya Ugiziji Bidhaa	1,159-80	1,867-00	1,271-00	724-00	1,185-00	1,128-00	1,128-00	1,239-00	
1.2.3. Gawio la Mashirika ya Umma	199-00	347-00	368-10	650-00	408-60	657-00	657-10	500-00	
1.2.4. Mapato Mengine (Wizara na Mikoa)	-00	-00	63-80	357-50	75-00	454-00	464-00	500-00	
1.2.5. "Appropriation in-Aid"	373-00	179-00	68-70	56-50	49-00	61-50	61-00	65-00	
2. Matumizi ya Kawaida	13,214-10	14,871-50	18,182-00	18,119-90	21,336-50	23,360-00	25,604-30	30,309-40	
2.1. Mfuko Mkuu wa Taifa	1,567-50	2,325-20	3,719-70	3,930-50	4,192-20	5,749-80	6,267-40	8,194-40	
2.2. Wizara	8,544-60	9,121-30	11,393-40	9,328-70	11,807-70	10,590-80	13,101-80	14,479-70	
2.3. Matumizi Maalum	-00	-00	-00	1,851-80	1,049-30	2,036-00	956-10	2,176-00	
2.4. Serikali za Mitaa	-00	-00	-00	1,684-90	2,445-80	3,524-70	3,542-40	3,822-00	
2.4.1. Halmashauri za Mitaa	-00	-00	-00	1,354-00	2,016-80	2,908-70	2,917-90	3,159-10	
2.4.2. Halmashauri za Miji	-00	-00	-00	330-90	429-00	616-00	624-50	663-10	
2.5. Tawala za Mikoa	3,102-00	3,425-00	3,068-90	1,324-00	1,841-50	1,458-70	1,736-70	1,637-30	
3. Salio (Nakisi) ya Bajeti ya Kawaida	-2,254-10	-1,726-50	-2,716-40	3,091-20	-2,193-50	3,448-00	-3,629-20	-5,625-40	
<b>II BAJETI YA MAENDELEO</b>									
4.1. Mapato kutoka humu Nchini	3,390-00	3,293-50	2,770-60	3,545-80	3,901-40	3,402-00	3,799-00	3,917-00	
4.1.1. Salio (Nakisi) ya Bajeti ya Kawaida	-2,254-10	-1,726-50	-2,716-40	-3,091-20	-2,193-50	-3,448-00	-3,629-20	-5,625-40	
4.1.2. Mikopo isiyo ya Mabanki	783-00	814-00	788-00	1,437-00	1,1-500	1,650-00	1,650-00	2,569-00	
4.1.3. Mikopo ya Mabanki	3,278-00	4,205-00	4,699-00	5,200-00	3,340-40	5,200-00	5,778-20	6,940-00	
4.1.4. Mapato Mengine	1,583-10	-	-00	-00	1,629-50	-	-	33-48	
4.2. Mapato kutoka Nje	1,795-00	1,852-00	2,965-40	2,995-10	1,489-70	3,427-00	2,141-00	3,068-00	
4.2.1. Mikopo	1,795-00	851-00	2,722-80	1,356-90	853-50	1,052-00	2,141-00	3,058-00	
4.2.2. Ruzuku	-	1,001-00	242-60	1,638-20	635-20	2,375-00	-00	-00	
4.3. Mapato ya Maendeleo	5,185-00	5,145-50	5,736-00	6,540-90	5,391-10	6,829-00	5,940-00	6,985-00	
5. Matumizi ya Maendeleo	5,185-00	5,145-50	5,736-00	6,560-00	5,391-10	6,829-00	5,940-00	6,985-00	
5.1. Wizara na Mashirika ya Umma	4,537-00	4,583-20	5,047-00	5,713-00	4,467-10	5,886-00	5,266-00	6,034-02	
5.2. Mikoa	648-00	562-30	689-00	847-00	924-00	943-00	674-00	950-8	

Chanzo:—Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango

Taibiti:

\*Mjadala unaendelea kuhusu Mapato ya Bajeti ya Maendeleo

(1) Mikopo ya Mabanki itarekebishwa.

UNUNUZI WA DHAMANA ZA TAIFA

Jedwali Na. 2

(Sh. Million)

WANUNUZI	1982/83	1983/84	1984/85	1985/86	1985/86	1986/87
	Halisi	Halisi	Halisi	Makisio	Mategemeo	Makisio
1. Shirika la Bima la Taifa	166.2	149	120.7	170	175	200
2. Akiba za Mashirika ya Umma	178	158	170	280	200	300
3. Akiba ya Wafanyakazi	331	317.5	515	500	500	700
4. Benki ya Posta	31	60	84.6	70	160	250
5. Wanunuzi wengine	108	103.4	121.3	630	615	931
(i) Akiba nyingine za Serikali	66.3	38.5	53.6	55	100	151
(ii) "Sinking Fund"	2.4	3	15.8	4	23	30
(iii) Makampuni na Mashirika	37.6	61	48.7	568	489	791
(iv) Wengineo	1.7	1.4	3.2	3	6	10
<b>Jumla</b>	<b>814.2</b>	<b>788.4</b>	<b>1,011.6</b>	<b>1,650</b>	<b>1,650</b>	<b>2,431</b>

UJAZI WA FEDHA NA MAENDELEO YA KARADHA:—1982—1987

Jedwali Na. 3

	1982 Desemba Halisi	1983 Juni Halisi	1983 Desemba Halisi	1984 Juni Halisi	1984 Desemba Halisi	1985 Juni Mategemeo	1985 Juni Halisi	1986 Juni Makisio	1986 Juni Mategemeo	1987 Juni Makisio
1. Akiba halisi ya Fedha za Kigeni (1) ...	-4,202-00	-5,347-40	-6,258-40	-7,517-30	-8,144-20	-7,022-00	-8,861-90	6,844-00	-8,862-00	-9,500-00
2. Karadha ...	26,246-00	27,422-80	30,538-50	3,3101-90	37,731-50	38,127-00	40,021-80	44,227-00	49,200-00	59,140-00
(a) Mikopo ya Serikali kutoka Mabenki ...	17,775-00	19,419-80	21,048-80	23,929-40	25,750-00	27,865-00	27,216-80	33,065-00	32,995-00	39,935-00
(b) Karadha kwa sekta nyingine za Uchumi ...	8,471-00	8,003-00	9,489-70	9,172-50	11,981-50	10,262-00	12,805-00	11,362-00	16,205-00	19,205-00
3. Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Pana ...	19,708-00	22,091-70	24,590-40	26,308-80	29,787-10	31,105-00	31,869-20	36,705-00	40,571-20	49,873-20
(a) Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Finyu ...	13,361-00	14,634-70	16,104-20	17,520-90	20,338-10	20,809-00	21,549-30	24,556-00	27,345-00	33,614-55
(b) Amana za Muda Maalum na za Akiba ...	6,347-00	7,457-00	8,486-20	8,787-90	9,449-00	10,319-00	10,319-90	12,149-00	13,226-20	16,258-65
4. Mambo Mengineyo ...	2,336-00	-16-30	-310-30	-724-20	-199-80	00	-709-30	878-00	-233-20	-361-60

Chanzo:—Benki Kuu.

(1) Zinajumlisha Malimbikizo ya Madeni.

C. MPANGO WA FEDHA ZA KIGENI WA MWAKA 1986/87

Mapitio katika Mwaka 1985/86

4.1. Kipindi cha mwaka 1985/86 kimeendelea na mfululizo wa matatizo yanayokabili uchumi wetu. Urari wa malipo yote unatarajiwa kuwa na nakisi ya \$ 396.9 milioni ikilinganishwa na nakisi ya \$ 269.9 milioni iliyofikiwa mwaka 1984/85. Kwa ujumla urari wa malipo uliendelea kuzorota katika mwaka 1985/86 kutokana hasa na sababu zifuatazo:

- (a) Kupungua kwa kiasi na bei kwa baadhi ya mazao muhimu yanayouzwa nchi za nje.
- (b) Kuongezeka kwa malimbikizo ya madeni ambayo mpaka Desemba 1985 yalifikia Sh. 8879.2 milioni.
- (c) Upungufu wa bidhaa za viwanda zinazouzwa nchi za nje kutokana na uhaba wa malighafi hivyo kushindwa kufikia malengo yaliyowekwa.

4.2. Licha ya matatizo hayo, mapato kutokana na mauzo ya nje kwa mwaka 1985/86 yanategemewa kufikia kiasi cha \$ 376.5 milioni ambazo ni asilimia 6.4 zaidi ya kiwango kilichofikiwa mwaka 1984/85. Ongezeko hili katika thamani ya mauzo nchi za nje linatokana na "nominal price increase". Hii ni kwa sababu ukiondoa pamba, tumbaku na chai hapakuwa na ongezeko la kiasi cha uzaji nje; na kwa kweli kiasi cha mauzo ya kahawa paretu na nyonyo kwa upande wa mazao ya kilimo na madini na bidhaa za viwanda kwa upande wa bidhaa zingine zinazouzwa nje kilipungua.

4.3. Kwa upande mwingine kulikuwa na ongezeko la \$ 58.5 milioni au asilimia 6.5 katika thamani ya ugizaji bidhaa nje kutoka \$ 905.7 milioni mwaka 1984/85 hadi \$ 964.2 milioni mwaka 1985/86.

4.4. Urari wa huduma ulikuwa na nakisi ya \$ 3.87 milioni ingawaje makisio ilikuwa ni ziada ya \$ 5.10 milioni katika mwaka huo. Nakisi hii imetokana na kuongezeka kwa malipo ya riba katika kipindi hicho. Nyongeza ya \$ 104.5 milioni zaidi ya makisio katika urari wa mali ilitokana na maongezeko ya kiasi cha mapato ya Serikali na Mashirika. Urari wa rasilimali za Serikali Mashirika na Binafsi ulikuwa na ziada ya \$ 62.5 milioni. Hii imetokana na kuongezeka kwa malipo ya mikopo. Urari wa karadha na bidhaa ikijumlisha na karadha za mafuta ulikuwa na nakisi ya \$ 18.0 milioni. Nakisi hii ilitokana hasa na malipo yaliyofanywa ya Sh. 1588.0 milioni kwa mikopo ya muda mfupi ya mafuta ya petroli. Jiihada za kutafuta misaada zaidi zilifanikisha kupatikana kwa \$ 94.3 milioni mwaka 1985/86 ikilinganishwa \$ 74.5 milioni zilizopatikana katika mwaka 1984/85.

MAKISIO YA MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE KATIKA MWAKA 1986/87

4.5. Malengo muhimu katika makisio ya mizania ya malipo na nchi za nje katika mwaka 1986/87 ni kama yafuatayo:

	US \$ milioni
Uuzaji bidhaa ...	454.8
Ununuzi bidhaa ...	1,200.0
Huduma ...	-105.2
Uhamisho wa mali ...	347.7
Mikopo ...	-0.5
Karadha za bidhaa ...	-28.0
Misaada ya uagizaji ...	83.5
Misaada maalum ...	327.0
Mabadiliko halisi ya akiba ya fedha za kigeni ...	-63.0
Upunguzaji madeni ...	183.7

4.6. Makadirio hayo yametayarishwa kwa kutumia hisia zifuatazo:

- (i) Kiasi cha uzalishaji na bei za bidhaa ziuwazwa nje zitaongezeka na thamani yake katika dola vitaongezeka kwa asilimia 20.1 kutoka kiwango kinachotarajiwa mwaka 1985/86 cha wastani wa dola 376.5 milioni.
- (ii) Kiasi cha uagizaji bidhaa nje kinakadiriwa kuongezeka hadi dola 1,200 milioni ikilinganishwa na dola 964.2 milioni zinazotegemewa mwaka 1985/86.
- (iii) bei za mafuta zinatarajiwa kuwa katika viwango vya juu na pia kwamba bei za bidhaa nyingine zinunuliwazo kutoka nje zinatarajiwa kuongezeka kutokana na sera zinazotumiwa na nchi za Magharibi zilizoendelea katika kuthibiti fedha kwa jumla.
- (iv) Juhudi zaidi zitaendelea kufanywa katika kutafuta misaada kutoka nje ili kukidhi mahitaji yetu muhimu.

Kwa jumla mizania ya malipo na nchi za nje katika mwaka 1986/87, inakadiriwa kubakia katika viwango vinavyotarajiwa hadi mwisho wa mwaka 1985/86.

#### Bidhaa:

4.7. Uuzaji wa bidhaa nchi za nje unakisiwa kuingiza \$ 454.84 milioni katika mwaka 1986/87 ambalo ni ongezeko la asilimia 20.8 kutoka kiasi cha \$ 376.5 milioni kinachotarajiwa mwaka 1985/86. Pato hilo litatokana na.

Bidhaa	US \$ milioni
(a) Mazao ya kilimo ... ..	309,36
(b) Bidhaa za Viwanda ... ..	60,25
(c) Madini ... ..	32,50
(d) Bidhaa nyingine ... ..	52,73
Jumla ... ..	454,84

4.8. Ongezeko hili linatarajiwa kutokana na kuongezeka katika kiasi kitakachouzwa nje kwa mazao ya kahawa, korosho, chai, na katani na matarajio ya maongezeko ya uuzaji nje wa bidhaa za petroli, viwandani na madini; na haya yote kufuatana na hisia zifuatazo:

#### A. Kahawa:

4.9. Uzalishaji wa kahawa utaongezeka kwa kiasi cha asilimia 5 kutoka tani 62,000 zinazotarajiwa mwaka 1985/86 hadi kufikia tani 65,100 mwaka 1986/87 hasa kutokana na kuongezeka kwa bei kwa wakulima (producer prices) na mpango unaoendelea wa kuimarisha uzalishaji. Kiasi cha kahawa kinachouzwa nje kinakisiwa kuwa tani 56,330, na bei katika masoko inatarajiwa kuongezeka kutoka wastani wa \$ 3,384 kwa tani 1985/86 hadi \$ 3,750 kwa tani hasa kutokana na kupungua kwa uzalishaji wa kahawa nchini Brazil iliyoharibiwa na theluji. Kwa jumla kahawa inakisiwa kutupatia \$ 211.21 milioni katika fedha za kigeni ikilinganishwa na kiasi cha \$ 164.82 milioni zinazotarajiwa kupatikana katika mwaka 1985/86. Makisio ya mwaka 1987/88 ni kuuzwa nje jumla ya tani 62,970 zenye thamani ya \$ 228.52 milioni.

#### B. Pamba:

4.10. Uzalishaji wa pamba unakisiwa kufikia tani 54,800 mwaka 1986/87 kutoka tani 52,727 zinazotegemewa katika mwaka 1985/86 na ongezeko hili linatokana hasa na juhudi zilizochochukuliwa na Serikali za kufufua uzalishaji wa zao hili. Kiasi cha pamba itakayouzwa nje inakisiwa kuwa tani 32,960 itakayoingiza kiasi cha \$ 33.97 milioni ikilinganishwa na tani 32,000 zinazokadiriwa kuleta \$ 36.63 milioni katika mwaka 1985/86. Matumizi ya viwanda vya nchini vile vile yanatarajiwa kuongezeka hasa kutokana na kuzinduliwa kwa viwanda vya kusokota nyuzi vya Ubungo na Tabora. Katika mwaka 1987/1988 pamba inakisiwa kuuzwa nje kwa kiasi cha tani 35,445 zenye thamani ya \$ 36.60 milioni.

#### C. Katani:

4.11. Uzalishaji wa zao la katani unakisiwa kuongezeka kutoka tani 40,000 zinazotarajiwa katika mwaka 1985/86 hadi kufikia tani 42,000 mwaka 1986/87 hasa kutokana na juhudi zilizochochukuliwa na Serikali za kufufua zao hili kwa kuuza baadhi ya mashamba kwa wazalishaji ambao wanaonyesha ufanisi zaidi na kwa kuwaruhusu kubakiza asilimia 10 ya ya mapato ya fedha za kigeni kutokana na uuzaji wa katani nje ili kuwawezesha kununua pembejeo na vifaa vingine muhimu.

Uuzaji wa katani nje unakisiwa kufikia tani 26,875 zitakazotupatia kiasi cha \$ 8.76 milioni ikilinganishwa na tani 25,000 zenye thamani ya \$ 8.15 milioni zinazotarajiwa kupatikana katika mwaka 1985/86. Uuzaji wa zao hili nchi za nje kwa mwaka 1987/88 unakisiwa kuwa tani 30,045 zenye thamani ya \$ 9.97 milioni wakati ambao juhudi za Serikali zinazochukuliwa za kufufua zao la katani zinatarajiwa kuwa zitakuwa zimeshazaa matunda zaidi.

#### D. Chai:

4.12. Uzalishaji wa chai utaendelea kuongezeka katika mwaka 1986/87 hasa kutokana na bei nzuri kwa wakulima ambapo karibu kila mwaka kunakuwepo na ongezeko halisi la kiasi cha asilimia 5. Kwa hali hiyo kiasi cha tani 20,800 za chai zinakadiriwa kuzalishwa ikilinganishwa na tani 18,700 zinazotarajiwa kupatikana mwaka 1985/86. Kati ya hizo tani 15,050 zenye thamani ya \$ 22.63 milioni zitauzwa nje ambapo mwaka 1985/86 tani zinazokadiriwa kuwa tani 13,000 zenye thamani ya \$ 18.30 milioni zilizuwa nje. Katika mwaka 1987/88 jumla ya tani 16,825 za chai zinakisiwa kuuzwa nje na \$ 26.83 milioni katika fedha za kigeni kupatikana.

#### E. Tumbaku:

4.13. Zao hili halitarajiwi kuongezeka sana kiuzalishaji katika mwaka 1986/87 (tani 17,200) ikilinganishwa na matarajio ya mwaka 1985/86 (tani 17,138). Kiasi cha tumbaku itakayouzwa nje kinakisiwa kuwa tani 9,675 zitakazotupatia \$ 12.26 milioni zikilinganishwa na tani 9,500 zenye thamani ya \$ 13.09 milioni zinazotarajiwa kuuzwa nje katika mwaka 1985/86, jitihada zinachukuliwa za kuzidisha ubora wa zao hili. Makisio ya mwaka 1987/88 ni kuuzwa nje tani 10,815 zitakazolingiza \$ 13.56 milioni katika fedha za kigeni.

## F. Bidhaa Zilizokuwa za Asili:

4.14. Jumla ya \$ 145.48 milioni zinakisiwa kupatikana kwa kuuza bidhaa zilizokuwa za asili (non-traditional exports) katika kipindi cha mwaka 1986/87 ikilinganishwa na kiasi cha \$ 118.16 milioni zinazotarajiwa kupatikana katika mwaka 1985/86. Ongezeko hili linatokana na matazamio kuwa mwaka huu baadhi ya viwanda vitazanza kufufuliwa na vitaweza kufanya kazi katika uwezo mkubwa zaidi kutokana na Sera za Serikali zinachukuliwa za kufufua uchumi.

4.15. Jedwali lifuatalo linaonyesha mwenendo wa uuzaji bidhaa nchi za nje katika miaka ya 1981/82—1985/86 na makisio yake katika mwaka 1986/87.

### MWENENDO WA UUZAJI BIDHAA NCHI ZA NJE 1981/82—1985/86 NA MAKISIO YA 1986/87

Jedwali Na. 4

(Thamani—US \$ Milioni)

Aina ya Bidhaa	1981/82	1982/83	1983/84	1984/85	1985/86	1985/86	1986/87
	(Halisi)	(Halisi)	(Halisi)	Matarajio	Lengo	Matarajio	Makisio
1. Kahawa—Kiasi (Tani)	56,445-30	55,257-00	54,819-40	49,100-00	55,000-00	48,700-00	56,330
Thamani	131-68	135-49	153-21	128-27	135-59	164-80	211-21
Bei kwa kilo	2-33	2-45	2-79	2-61	2-47	3-38	3-75
2. Pamba—Kiasi (Tani)	40,741-80	38,956-50	38,656-50	29,700-00	25,000-00	32,000-00	32,960
Thamani	63-69	56-29	58-62	47-49	35-43	36-65	33-97
Bei kwa kilo	1-56	1-44	1-52	1-60	1-42	1-15	1-03
3. Katani—Kiasi (Tani)	54,466-00	32,438-00	23,752-00	26,050-00	10,000-00	25,000-00	26,875
Thamani	28-46	15-58	11-28	9-16	4-01	8-15	8-76
Bei kwa kilo	-52	-48	-47	-35	-40	-33	-33
4. Chai—Kiasi (Tani)	11,275-70	12,235-30	15,651-00	11,300-00	12,000-00	13,000-00	15,050
Thamani	17-46	19-27	23-85	18-72	19-47	18-30	22-63
Bei kwa kilo	1-55	1-57	1-52	1-66	1-62	1-41	1-50
5. Tumbaku—Kiasi (Tani)	11,263-90	5,960-40	5,600-00	7,300-00	8,000-00	9,500-00	9,675
Thamani	19-88	13-31	10-48	10-85	15-67	13-10	12-26
Bei kwa kilo	1-76	2-23	1-87	1-49	1-96	1-38	1-27
6. Korosho—Kiasi (Tani)	5,421-00	9,000-00	-00	21,550-00	-00	21,000-00	23,650
Thamani	6-95	43-74	23-69	21-49	-00	17-35	20-53
Bei kwa kilo	1-28	4-86	N/A	1-00	N/A	-83	-87
<b>Jumla Ndogo (Thamani)</b>	<b>268-12</b>	<b>283-58</b>	<b>281-13</b>	<b>235-98</b>	<b>210-16</b>	<b>258-35</b>	<b>309-36</b>
<b>Bidhaa Zisizo za Asili:</b>							
1. Bidhaa za Mafuta ya Petroli	9-53	20-98	20-95	20-27	32-75	24-95	27-73
2. Madini	67-10	41-08	40-80	29-34	24-00	27-65	32-50
3. Bidhaa za Viwandani	46-98	42-10	54-53	34-98	65-25	41-55	60-25
4. Bidhaa nyinginezo	59-40	37-91	35-15	23-40	20-95	24-00	25-00
<b>Jumla Ndogo (Thamani)</b>	<b>183-00</b>	<b>142-07</b>	<b>151-43</b>	<b>107-98</b>	<b>142-95</b>	<b>118-15</b>	<b>145-48</b>
<b>Jumla Kubwa</b>	<b>451-12</b>	<b>425-65</b>	<b>432-56</b>	<b>343-97</b>	<b>353-11</b>	<b>376-50</b>	<b>454-84</b>

4.16. Kwa upande mwingine, uagizaji nje unakadiriwa kugharimu \$ 1,200.0 milioni. Licha ya kununulia mafuta (\$ 168.5) milioni kiasi kingine kitatumika kununulia zana na spea, malighafi na kuendeshea shughuli za utalii. Makisio hayo ya uagizaji ni makubwa kuliko matarajio ya mwaka 1985/86. Hii ina maana kwamba kiasi cha bidhaa zitakaoagizwa kutoka nchi za nje kitakuwa zaidi ikilinganishwa na kiwango cha bidhaa zinazotegemewa katika mwaka 1985/86.

#### Huduma:

4.17. Inakadiriwa kuwa, urari wa huduma utakuwa na nakis ya \$ 105.2 milioni katika mwaka 1986/87. Hii inatokana na hisia kwamba riba za mikopo iliyopevuka na za malimbikizo ya madeni zitalipwa katika kipindi hiki. Vile vile huduma zingine zitalipwa ipasavyo.

#### Uhamisho wa Mali:

4.18. Urari wa uhamisho halisi wa mali ambazo ni pamoja na ruzuku za Serikali na za binafsi unakadiriwa kuwa na ziada ya \$ 347.7 milioni katika kipindi cha mwaka 1986/87, ikilinganishwa na ziada ya \$ 104.5 milioni zinazotarajiwa mwaka 1985/86. Ziada hii inatokana na mapato halisi kiasi cha \$ 132.5 milioni za binafsi na \$ 215.2 milioni za Serikali.

#### Rasilimali:

4.19. Mapato kutokana na mikopo kwa Serikali, Mashirika na Makampuni binafsi yanakadiriwa kuwa na pengo la \$ 0.5 milioni katika mwaka 1986/87 ikilinganishwa na matarajio ya \$ 62.5 milioni mwaka 1985/86. Kuongezeka kwa malipo kunatokana na kupevuka kwa madeni mengi ya miaka ya nyuma.

4.20. Urari wa karadha na bidhaa unakadiriwa kuwa na pengo la \$ 28.0 milioni.

#### Malipo Mengine:

4.21. Katika mwaka 1986/87 mapato kutokana na misaada maalum yanakadiriwa kuwa dola 410.5 milioni.

4.22 Jedwali Na. 5 linaonyesha mizania ya malipo baina yetu na nchi za nje katika miaka 1980/81—1985/86; na makisio ya mwaka 1986/87.

MPANGO WA FEDHA ZA KIGENI KWA MWAKA 1986/87

Jedwali Na. 5

(US . Milion)

	1980/81 halisi	1981/82 halisi	1982/83 halisi	1983/84 halisi	1984/85 halisi	1985/86 Matarajio	1986/87 Makadirio
<b>A. Urari wa Biashara ya Bidhaa:</b>							
Ziuzwazo nje (f.o.b.)...	534-40	488-21	395-95	372-78	353-79	376-50	454-8
Zinunuliwazo nje(c.i.f.)	1196-76	1134-10	956-70	829-09	905-68	964-21	1,200-0
<b>B. Urari wa Huduma</b>	44-54	54-43	31-04	17-86	16-77	-3-87	-105-2
Mapato	187-35	156-54	112-70	107-75	118-19	117-71	125-0
Malipo	142-81	102-11	81-66	89-89	101-43	121-58	230-2
<b>C. Urari wa Uhamisho wa Mali</b>	107-20	100-60	89-05	90-44	100-49	104-50	347-7
Iliyolingia	108-95	102-10	92-15	94-35	104-00	108-00	347-7
Iliyotoka	1-75	1-50	3-10	3-91	3-51	3-50	347-7
<b>Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho wa Mali</b>	-510-63	-490-86	-440-66	-348-01	-434-63	-487-10	-502-7
<b>D. Rasilimali:</b>							
Mikopo ya muda mrefu/wakati (urari)	173-0	210-23	187-27	128-84	109-85	62-50	-0-5
Iliyolingia	213-30	257-93	225-83	174-42	191-42	205-00	160-0
Iliyotoka	40-20	47-70	38-56	45-58	81-57	142-50	160-5
Karudhara za Biadhaa (Urari)	80-60	79-15	79-70	105-81	38-91	-18-00	-28-0
<b>E. Makosa na Masahihisho</b>	41-70	7-1	-110-0	-89-6	-58-5	-48-6	0-0
<b>F. Misada ya Uagizaji</b>	110-0	101-8	76-2	54-8	74-5	94-3	83-5
Misada Msalum							327-0
<b>G. Urari wa Malipo Yote</b>	-105-20	-92-6	-207-5	-148-2	-269-9	-396-9	
<b>H. Mahabiliko: Akiba ya fedha za Kigeni</b>	105-2	92-6	207-5	148-2	269-9	396-9	

(-)-Chagezeko.

001,01	---	001,01	---	001,01	---	001,01	---
001,02	---	001,02	---	001,02	---	001,02	---
001,03	---	001,03	---	001,03	---	001,03	---
001,04	---	001,04	---	001,04	---	001,04	---
001,05	---	001,05	---	001,05	---	001,05	---
001,06	---	001,06	---	001,06	---	001,06	---
001,07	---	001,07	---	001,07	---	001,07	---
001,08	---	001,08	---	001,08	---	001,08	---
001,09	---	001,09	---	001,09	---	001,09	---
001,10	---	001,10	---	001,10	---	001,10	---
001,11	---	001,11	---	001,11	---	001,11	---
001,12	---	001,12	---	001,12	---	001,12	---
001,13	---	001,13	---	001,13	---	001,13	---
001,14	---	001,14	---	001,14	---	001,14	---
001,15	---	001,15	---	001,15	---	001,15	---
001,16	---	001,16	---	001,16	---	001,16	---
001,17	---	001,17	---	001,17	---	001,17	---
001,18	---	001,18	---	001,18	---	001,18	---
001,19	---	001,19	---	001,19	---	001,19	---
001,20	---	001,20	---	001,20	---	001,20	---
001,21	---	001,21	---	001,21	---	001,21	---
001,22	---	001,22	---	001,22	---	001,22	---
001,23	---	001,23	---	001,23	---	001,23	---
001,24	---	001,24	---	001,24	---	001,24	---
001,25	---	001,25	---	001,25	---	001,25	---
001,26	---	001,26	---	001,26	---	001,26	---
001,27	---	001,27	---	001,27	---	001,27	---
001,28	---	001,28	---	001,28	---	001,28	---
001,29	---	001,29	---	001,29	---	001,29	---
001,30	---	001,30	---	001,30	---	001,30	---
001,31	---	001,31	---	001,31	---	001,31	---
001,32	---	001,32	---	001,32	---	001,32	---
001,33	---	001,33	---	001,33	---	001,33	---
001,34	---	001,34	---	001,34	---	001,34	---
001,35	---	001,35	---	001,35	---	001,35	---
001,36	---	001,36	---	001,36	---	001,36	---
001,37	---	001,37	---	001,37	---	001,37	---
001,38	---	001,38	---	001,38	---	001,38	---
001,39	---	001,39	---	001,39	---	001,39	---
001,40	---	001,40	---	001,40	---	001,40	---
001,41	---	001,41	---	001,41	---	001,41	---
001,42	---	001,42	---	001,42	---	001,42	---
001,43	---	001,43	---	001,43	---	001,43	---
001,44	---	001,44	---	001,44	---	001,44	---
001,45	---	001,45	---	001,45	---	001,45	---
001,46	---	001,46	---	001,46	---	001,46	---
001,47	---	001,47	---	001,47	---	001,47	---
001,48	---	001,48	---	001,48	---	001,48	---
001,49	---	001,49	---	001,49	---	001,49	---
001,50	---	001,50	---	001,50	---	001,50	---
001,51	---	001,51	---	001,51	---	001,51	---
001,52	---	001,52	---	001,52	---	001,52	---
001,53	---	001,53	---	001,53	---	001,53	---
001,54	---	001,54	---	001,54	---	001,54	---
001,55	---	001,55	---	001,55	---	001,55	---
001,56	---	001,56	---	001,56	---	001,56	---
001,57	---	001,57	---	001,57	---	001,57	---
001,58	---	001,58	---	001,58	---	001,58	---
001,59	---	001,59	---	001,59	---	001,59	---
001,60	---	001,60	---	001,60	---	001,60	---
001,61	---	001,61	---	001,61	---	001,61	---
001,62	---	001,62	---	001,62	---	001,62	---
001,63	---	001,63	---	001,63	---	001,63	---
001,64	---	001,64	---	001,64	---	001,64	---
001,65	---	001,65	---	001,65	---	001,65	---
001,66	---	001,66	---	001,66	---	001,66	---
001,67	---	001,67	---	001,67	---	001,67	---
001,68	---	001,68	---	001,68	---	001,68	---
001,69	---	001,69	---	001,69	---	001,69	---
001,70	---	001,70	---	001,70	---	001,70	---
001,71	---	001,71	---	001,71	---	001,71	---
001,72	---	001,72	---	001,72	---	001,72	---
001,73	---	001,73	---	001,73	---	001,73	---
001,74	---	001,74	---	001,74	---	001,74	---
001,75	---	001,75	---	001,75	---	001,75	---
001,76	---	001,76	---	001,76	---	001,76	---
001,77	---	001,77	---	001,77	---	001,77	---
001,78	---	001,78	---	001,78	---	001,78	---
001,79	---	001,79	---	001,79	---	001,79	---
001,80	---	001,80	---	001,80	---	001,80	---
001,81	---	001,81	---	001,81	---	001,81	---
001,82	---	001,82	---	001,82	---	001,82	---
001,83	---	001,83	---	001,83	---	001,83	---
001,84	---	001,84	---	001,84	---	001,84	---
001,85	---	001,85	---	001,85	---	001,85	---
001,86	---	001,86	---	001,86	---	001,86	---
001,87	---	001,87	---	001,87	---	001,87	---
001,88	---	001,88	---	001,88	---	001,88	---
001,89	---	001,89	---	001,89	---	001,89	---
001,90	---	001,90	---	001,90	---	001,90	---
001,91	---	001,91	---	001,91	---	001,91	---
001,92	---	001,92	---	001,92	---	001,92	---
001,93	---	001,93	---	001,93	---	001,93	---
001,94	---	001,94	---	001,94	---	001,94	---
001,95	---	001,95	---	001,95	---	001,95	---
001,96	---	001,96	---	001,96	---	001,96	---
001,97	---	001,97	---	001,97	---	001,97	---
001,98	---	001,98	---	001,98	---	001,98	---
001,99	---	001,99	---	001,99	---	001,99	---
001,00	---	001,00	---	001,00	---	001,00	---

## SURA YA NNE

### MIPANGO YA SEKTA MBALIMBALI

#### Mahtasari wa Mpango:

1. Mpango wa maendeleo wa mwaka 1986/87 utaendeleza juhudi za serikali za kutoa umuhimu wa juu kabisa katika sekta ya kilimo. Kutokana na hali isiyoridhisha inayoendelea kuikabili Taifa, matatizo mengi ya uchumi wetu yangeweza kutatuliwa kama maendeleo ya sekta ya kilimo yangekuwa bora zaidi kuliko ilivyo hivi sasa, kwa pande zote, yaani mazao ya chakula, mazao ya biashara na mifugo. Kwa hiyo mpango wa mwaka 1986/87 utajaribu kutafsiri kwa vitendo nia ya kuipa sekta ya kilimo umuhimu wa juu kwa kuitengea sekta hii sehemu kubwa ya bajeti ya maendeleo, na papo hapo kuzielekza sekta nyingine zilenge mipango yao ya maendeleo kwa kusaidia sekta ya kilimo.

2. Kwa hiyo kilimo kitakuwa ndiyo kiini cha mpango mzima. Hivyo sekta nyingine zote, hasa za Mawasiliano na Uchukuzi, Ujenzi na Viwanda zitaielekza shughuli zao kwenye sekta ya kilimo ili iweze kuongeza uzalishaji.

3. Katika kipindi cha mwaka 1986/87, Bajeti ya Maendeleo ya serikali inakadiriwa kuwa sh. 6,985 milioni. Kati ya fedha hizo, sh. 3,917 milioni, au asilimia 56.1, ni fedha zinatarajiwa kutoka kwenye vianzio vya hapa hapa nchini, na sh. 3,068 milioni au asilimia 43.9 ni fedha kutoka nje. Fedha nyingine, ambazo siyo sehemu ya bajeti ya serikali lakini zitatokana na mikopo kutoka kwenye mabanki, fedha za mashirika ya umma yenyewe, mifuko maalum, na misaada mingine kwa jumla, zinatarajiwa kuwa sh. 950.8 milioni, ambayo ni sawa na asilimia 13.6 ya bajeti yote ya maendeleo, ambapo bajeti za Wizara na Mashirika yake zitakuwa ni sh. 6,034.2 milioni.

4. Mahtasari wa Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka 1986/87 ni kama ilivyoonyeshwa katika jedwali Na. 6.

### FEDHA ZA MAENDELEO MWAKA 1986/87

Jedwali Na. 6

Fungu	Wizara	BAJETI YA SERIKALI		Jumla	Fedha Nyingine	Sh. '000 Jumla ya Mahitaji ya Fedha 1986/87
		Fedha za Hapa	Fedha za Nje			
30	Ikulu	12,500	—	12,500	—	12,500
31	Makamu	1,500	—	1,500	—	1,500
32	Kazi na Maendeleo ya Utumishi	33,115	31,342	64,457	169,700	234,157
34	Nje	4,000	—	4,000	—	4,000
37	Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais	25,492	13,850	39,342	—	39,342
38	Ngome	5,000	—	5,000	—	5,000
39	Jeshi la Kujenga Taifa	18,650	—	18,650	—	18,650
40	Mahakama...	4,900	—	4,900	—	4,900
41	Sheria	2,000	—	2,000	—	2,000
43	Kilimo na Mifugo	510,636	502,734	1,013,370	411,963	1,425,333
44	Viwanda na Biashara	248,600	432,000	680,600	523,561	1,204,161
46	Elimu	160,500	336,769	497,269	—	497,269
47	Mawasiliano na Ujenzi	439,450	479,560	919,010	499,481	1,418,491
48	Ardhi, Maji, Nyumba na Maendeleo Mijini	200,102	125,727	325,829	—	325,829
49	Nishati na Madini	352,000	401,842	753,842	111,902	865,744
50	Fedha Uchumi na Mipango	172,697	74,538	247,235	984,856	1,232,091
51	Mambo ya Ndani	130,000	—	130,000	—	130,000
52	Afya na Ustawi wa Jamii	38,620	42,208	80,828	27,500	108,328
53	Maendeleo ya Jamii, Utamaduni, Vijana na Michezo	22,500	3,046	25,546	—	25,546
54	Radio	4,000	—	4,000	—	4,000
55	Makao Makuu (CDA)	154,000	70,946	224,946	158,000	382,946
57	Ulinzi	475,300	—	475,300	—	475,300
60	Maliasili na Utalii	93,020	177,594	270,614	—	270,614
61	Serikali za Mitaa na Maendeleo ya Ushirika	159,638	73,844	233,482	—	233,482
	<b>Jumla Wizara</b>	<b>3,268,220</b>	<b>2,766,000</b>	<b>6,034,220</b>	<b>2,886,963</b>	<b>8,921,183</b>
	<b>Jumla Mikoa na Halmashauri za Wilaya</b>	<b>648,780</b>	<b>302,000</b>	<b>950,780</b>	<b>—</b>	<b>950,780</b>
	<b>Jumla ya Bajeti ya Serikali</b>	<b>3,917,000</b>	<b>3,068,000</b>	<b>6,985,000</b>	<b>2,886,963</b>	<b>9,871,963</b>

#### Mahtasari wa Mahitaji ya Fedha Kisekta:

5. Mgawanyo wa fedha unaonyesha juhudi za serikali za kutoa umuhimu wa juu katika sekta ya kilimo yenyewe, na sekta ina zozalisha mali moja kwa moja.

6. Sekta ya kilimo peke yake imetengewa asilimia 22.8 ya Bajeti ya Serikali ya maendeleo na asilimia 30.6 ya Bajeti nzima ya maendeleo. Sekta za uzalishaji mali moja kwa moja, yaani kilimo, mifugo, viwanda, maliasili na madini zimetengewa asilimia 41.7 ya Bajeti ya Serikali ya maendeleo na asilimia 46.0 ya Bajeti nzima ya maendeleo.

7. Huduma za kiuchumi zimepangiwa asilimia 24.5 ya Bajeti ya Serikali na asilimia 29.3 ya Bajeti yote ya maendeleo. Huduma za Kijamii nazo zimetengewa asilimia 20.0 ya Bajeti ya maendeleo.

8. Kwa jumla mgawanyo huu wa fedha unaonyesha nia ya Serikali ya kufufua uchumi, kwa kuweka rasilimali zaidi katika sekta zinazozalisha mali moja kwa moja na katika sekta za huduma za kiuchumi ambazo zinatoa huduma za moja kwa moja kwa sekta zinazozalisha mali. Uchumi unaokuwa pekee ndiyo unaoweza kuendeleza huduma za kijamii ambazo ingawaje pia ni muhimu, matokeo yake katika uchumi huchukua muda mrefu.

9. Ufafanuzi zaidi kuhusu mgawanyo wa fedha kissekta unaonyeshwa katika jedwali Na. 7.

10. Yafuatayo hapa chini ni maelezo ya shughuli na miradi muhimu inayokusudiwa kutekelezwa. Orodha ya miradi ya maendeleo kwa Wizara na Mashirika ya Umma, gharama zake pamoja na vianzio mbali mbali vya fedha inapatikana katika Nyongeza A. Orodha ya miradi ya mikoa na wilaya imeonyeshwa katika Nyongeza B.

**MPANGO WA MAENDELEO 1986/87: MUHTASARI WA MAHITAJI YA FEDHA KISEKTA:**

Jedwali Na. 7

(Katika Sh \*000)

Sekta	Bajeti ya Serikali			Asilimia	Fedha Nyingine	Jumla ya Mahitaji ya Fedha 1986/87	Asilimia ya Mahitaji yote
	Fedha za Hapa	Fedha za Nje	Jumla				
<b>KUZALISHA MALI:</b>							
Kilimo na Mifugo ... ..	888,063	703,148	1,591,211	22.8	1,431,819	3,023,030	30.6
Viwanda ... ..	274,476	492,099	766,575	11.0	172,750	939,325	9.5
Maliasili ... ..	86,901	20,326	107,227	1.5	2,840	110,067	1.1
Madini ... ..	232,100	211,842	443,942	6.4	25,520	469,462	4.8
<b>Jumla ... ..</b>	<b>1,481,540</b>	<b>1,427,415</b>	<b>2,908,955</b>	<b>41.7</b>	<b>1,632,929</b>	<b>4,326,591</b>	<b>46.0</b>
<b>HUDUMA ZA KIUCHUMI:</b>							
Maji ... ..	61,988	38,000	99,988	1.4	—	99,988	1.0
Nishati ... ..	123,800	230,000	353,800	5.1	86,382	440,182	4.5
Ardhi na Ujenzi ... ..	517,549	170,325	687,874	9.8	403,618	1,091,492	11.1
Biashara na Utalii ... ..	41,000	—	41,000	0.6	335,691	376,691	3.8
Mawasiliano na Uchukuzi ... ..	153,330	378,460	531,790	7.6	349,333	881,123	8.9
<b>Jumla ... ..</b>	<b>897,667</b>	<b>816,785</b>	<b>1,714,452</b>	<b>24.5</b>	<b>1,175,024</b>	<b>2,836,263</b>	<b>29.3</b>
<b>HUDUMA ZA KIJAMII:</b>							
Maji ... ..	169,261	130,204	299,465	4.3	—	299,465	3.0
Elimu na Utamaduni ... ..	332,603	511,806	844,409	12.1	—	844,409	8.5
Afya ... ..	188,645	66,543	255,188	3.6	37,500	292,688	3.0
<b>Jumla ... ..</b>	<b>690,509</b>	<b>708,533</b>	<b>1,399,062</b>	<b>20.0</b>	<b>37,500</b>	<b>1,295,360</b>	<b>14.5</b>
Utawala na Huduma Nyingine ... ..	847,284	115,247	962,531	13.8	41,510	1,004,041	10.2
<b>Jumla ya Sekta ... ..</b>	<b>3,917,000</b>	<b>3,068,000</b>	<b>6,985,000</b>	<b>100.0</b>	<b>2,886,963</b>	<b>9,871,963</b>	<b>100.0</b>

**1.—KILIMO**

1. Mpango wa maendeleo wa mwaka 1986/87 utaendelea kuweka mkazo mkubwa katika kutekeleza miradi na kuimarisha huduma mbali mbali kwa wakulima ili kuweza kufikia shabaha kuu zifuatazo:—

(a) Kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula hasa ya nafaka ili kuvuka kiwango kilichofikiwa mwaka 1985/86 na pia ili kupunguza uagizaji kutoka nje na hivyo kuweza kujitosheleza na kuokoa fedha za kigeni.

(b) Kuongeza uzalishaji wa mazao ya biashara kwa shabaha ya kuyauza nje baada ya kusindikwa au kama yalivyo ili kujiongeza mapato yetu ya fedha za kigeni.

2. Katika kuendeleza mazao mbali mbali, Wizara ya Kilimo na Maendeleo ya Mifugo pamoja na Idara na Mashirika yaliyo chini yake inatarajiwa kutekeleza miradi 126 inayohusu mazao na imetengewa kiasi cha Sh. 862.969 milioni kutoka katika Bajeti ya Serikali. Kati ya fedha hizo, Sh. 422.154 milioni zinatarajiwa kuwa fedha za hapa na Sh. 440.818 milioni kutoka nje. Hata hivyo ukijumlisha na vianzio vingine vya fedha kwa ajili ya miradi ya mazao jumla ya fedha zinazokusudiwa kutumika ni Sh. 1,163.787 milioni. Umuhimu mkubwa katika kutenga fedha kwa miradi mbali mbali umewekwa katika miradi inayozalisha moja kwa moja.

3. Hata hivyo kwa kuzingatia kuwa uzalishaji mkubwa wa mazao nchini unategemea sana wakulima wadogo wadogo, umuhimu umewekwa pia katika kuimarisha huduma mbali mbali za kitaalamu na upatikanaji wa zana za pembejeo na kuhakikisha kuwa mazao hayaharibiwi na magonjwa, wadudu, wanyama waharibifu na unyevu. Kwa jumla mwelekeo wa shughuli za uendelezaji mazao katika mwaka 1986/87 ni katika kuwasaidia wakulima wadogo wadogo vijijini.

**Mazao ya Chakula:**

4. Katika jitihada za kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula nchini ili hatimaye tuweze kujitosheleza, sekta ya Kilimo inakusudia kuchukua hatua mbali mbali katika maeneo yaliyoelezwa hapa chini.



(a) Umwagiliaji Maji: Hadi sasa jitihada imekuwa ikirwekwa katika kuanzisha na kuimarisha Ofisi za umwagiliaji katika kanda mbali mbali kwa kuzipatia majengo ya Ofisi, nyumba za kuishi, wataalamu na zana za kufanyia kazi. Pamoja na kuendelea kuwepo matatizo ya zana na wataalamu, baadhi ya kanda zimekwisha kufikia hatua ya kutekeleza kwa ufanisi miradi mbali mbali ya umwagiliaji.

5. Shabaha kubwa ya Ofisi za umwagiliaji za kanda ni kushughulikia miradi midogo midogo, hii ikiwa ni pamoja na kurekebisha (rehabilitate) ile iliyochakaa na kuitengeneza upya ile ambayo haifanyi kazi kutokana na kuharibika kwa mifereji na pampu kwa muda mrefu bila matengenezo. Hivyo katika mpango wa mwaka 1986/87 msukumo mkubwa utawekwa katika miradi midogo midogo ya umwagiliaji juhudi zikielekezwa hasa katika usafishaji na au uwekaji wa mifereji na katika ujenzi au matengenezo ya "weirs" ambazo ni muhimu sana katika umwagiliaji.

6. Lengo kwa kanda zote ni kuanza kushughulikia miradi si chini ya mitatu ya aina hii isipokuwa kwa kanda za Tabora na Mwanza ambazo zitashughulikia miradi zaidi ya mitatu kutokana na uwezo wao mkubwa zaidi wa kumudu shughuli hizi na kufanya miradi mingi ya kiwango hiki kuanza tena kufanya kazi.

7. Kwa miradi ya umwagiliaji yenye ukubwa wa kati—yaani Kitivo (Ha. 600), Mwamapuli, Lower Moshi na Usangu (600), Serikali inakusudia kutenga fedha zaidi ili kuiwezesha kukamilisha na uzalishaji kuanza.

(b) Mashamba ya Mbegu bora:

8. Mahitaji ya mbegu bora katika mwaka 1986/87 ni tani 23,000 na uwezo wa kuzalisha nchini ni tani 9,000. Matarajio ya kuagiza kutoka nje ni tani 1,120. Hata hivyo pamoja na kutegemea kuwa pengo hilo lililosalia litahimizwa litokane na mbegu nzuri kutoka katika vijiji na wakulima stadi, Serikali itaendelea na juhudi za kuimarisha mashamba ya mbegu bora yaliyopo ili yaweze kuzalisha kulingana na uwezo uliopo pamoja na kuyapanua. Pia inakusudiwa kuendelea na mafunzo kwa wataalamu katika fani hii na kuendelea kudhibiti ubora wa mbegu kwa kujenga maabara ya tatu huko Njombe.

9. Hata hivyo, pamoja na juhudi hizo zitakazochukuliwa, kati ya hekta 5,291 zilizopo hivi sasa, ni hekta 2,610 tu sawa na asilimia hamsini, zinazotarajiwa kutumika kuzalisha mbegu bora. Hivyo Serikali itaendelea pia kutafuta uwezekano wa vyombo vingine nchini kwa mfano Magereza, JKT na hata watu binafsi kusaidia katika uzalishaji wa mbegu bora ili hatimaye tuweze kuji-itosheleza.

(c) Zana na Pembejeo:

10. Katika maandalizi ya kilimo katika kila msimu, suala la zana na pembejeo ndilo linalopewa umuhimu wa kwanza. Hata hivyo, mahitaji ya zana na pembejeo nchini yanaathiriwa sana na uwezo mdogo wa kuzalisha hapa hapa nchini na uhaba wa fedha za kigeni za kuagiza moja kwa moja. Hali hii haitegemewi kuwa tofauti katika kipindi cha mwaka 1986/87. Mahitaji ya zana na pembejeo katika mwaka 1986/87 ni kama ifuatavyo:—

Mbolea	...	...	...	...	...	Tani	180,000
Mbegu bora	...	...	...	...	...	Tani	23,000
Magunia milioni	...	...	...	...	...	Tani	30
Madawa ya Maji	...	...	...	...	...	Lita	3,900,000
Majembe ya mkono	...	...	...	...	...	...	2,100,000
Plau	...	...	...	...	...	...	54,000
Minyororo	...	...	...	...	...	...	420,000
Ndimi za Plau	...	...	...	...	...	...	420,000
Matrekta	...	...	...	...	...	...	1,800

11. Kwa kuzingatia uzoefu wa miaka iliyopita, inatarajiwa kuwa kiasi cha tani 167,758 za mbolea zitapatikana; hii ikiwa ni tani 41,403 zitakazotokana na uzalishaji nchini na tani 126,355 zikiwa ni kutoka nje na hivyo kubakisha pengo dogo la tani kama 13,000. Mkegu bora zinatarajiwa kupatikana tani 10,457 ambapo kati ya hizo tani 8,430 zinatarajiwa kuzalishwa nchini, tani 1,120 kutoka nchi za nje na tani 907 zikiwa ni bakaa kutokana na msimu uliopita. Hivyo kutakuwa na bakaa ya tani 12,543 mbazo zinatarajiwa zitokane na wakulima wenyewe na hasa kutoka kwa wakulima stadi.

12. Kwa upande wa magunia, uzoefu ni kuwa upatikanaji wake umekuwa kati ya milioni 12 na 15. Upatikanaji nchini ni wastani wa milioni 9.8 ukilinganisha na mahitaji ya magunia milioni 30. Kiasi kitakachoagizwa kitategemea sana uwezo wetu wa fedha za kigeni.

13. Kwa madawa na zana za kilimo, hivi vyote hutegemea uwezo wetu wa kupata fedha za kigeni kwa kuagiza moja kwa moja ingawa kwa zana za kilimo, hasa zile za mikono, upatikanaji wa malighafi kutoka nje ndiyo unaotegemewa. Hata hivyo, kwa uzoefu uliopo, upatikanaji wa zana za mikono hasa majembe, na pia ndimi za plau na minyororo, haitegemewi kuwa ya matatizo. Tatizo linategemea kuendelea kuwa katika upatikanaji wa madawa ya maji na unga, risasi na matrekta.

(d) Uzalishaji mazao ya Chakula:

14. Ili kutumia kikamilifu zaidi uwezo ambao mikoa ya Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma inayo katika uzalishaji wa mazao ya chakula hasa yale ya nafaka, inatarajiwa katika kipindi cha mwaka 1986/87 kuanza na programu ya kuongeza uzalishaji katika mikoa hii kwa kushirikiana na Shirika la IFAD. Shughuli muhimu zitakazofanywa ni pamoja na kuwekwa na kuimarisha mfumo wa upatikanaji na usambazaji zana na pembejeo ili mkulima mdogo aweze kuvipata kwa urahisi; kuimarisha mfumo wa usafirishaji na kuipatia mikoa hii zana na vifaa vinavyohitajika; na kusaidia juhudi za kuimarisha utoaji huduma za kitaalamu kwa wakulima (extension) na kuimarisha vyamba vya ushirika kwa kuvipatia usafiri, usimamizi na mafunzo.

(e) Elimu kwa Wakulima:

15. Shabaha itakuwa ni kuendelea na kazi za kuanzisha mashamba ya maonyesho kwa wakulima hasa katika matumizi ya aina mbali mbali za mbolea na mbegu bora kwa kutumia matokeo ya utafiti ambayo yapo; pia kuanzisha mfumo unaoeleweka na wa moja kwa moja utakaowezesha matokeo ya utafiti hasa wa mbegu bora, mbimu za ukulima na mapendekezo mapya ya utafiti kumfikia bwana shamba (extension staff) ili aweze kumfikisha mkulima na pia matatizo ya mkulima kurudi hadi kwa matafiti ili asidie kuyatatua.

16. Katika kuimarisha elimu kwa wakulima inakusudiwa kuimarisha sehemu za radio, uhariri wa magazeti, uchapishaji wa vitabu, senema na vyo vya wakulima. Umuhimu mkubwa utakuwa katika kuzipatia shughuli za elimu zana na vifaa vinavyohitajika kufikisha ujumbe wa mambo mbali mbali ya kuendeleza kilimo kwa wakulima wengi na pia kuimarisha vyo vya wakulima ili viwe kweli kielelezo kwa wanafunzi wanaopitia vyo hivyo na kwa wanakijiji jirani.

**(f) Ujenzi wa Maghala:**

17. Pamoja na kuendelea kuhimiza Vyama vya Ushirika na hasa vyama vya msingi kujenga maghala kwa shabaha ya kupunguza uharibifu wa mazao, Serikali, kwa kupitia shirika la Taifa la Usagishaji itaendelea na juhudi za kuongeza uwezo wake wa kuhifadhi nafaka kutoka katika maeneo yaliyo na ziada kwa matumizi katika maeneo yenye upungufu na pia kwa hifadhi ya tahadhari (strategic reserves). Inategemewa kuwa kwa kumaliza ujenzi wa maghala ya Mbeya na Kipawa II, Shirika litakuwa na uwezo wa kuhifadhi tani 457,466 za nafaka.

18. Vile vile juhudi zitaendelezwa katika kuzuia uharibifu wa mazao mashambani na katika maghala kwa kuua wadudu, ndege na wanyama waharibifu. Kazi hizi ni za kila mwaka lakini ni lazima kila wakati Serikali ijiandae kupambana na adui hawa.

**Matarajio ya uzalishaji mazao ya Chakula:**

I. Sukari (Tani)	1984/85	1985/86	1986/87
Kampuni		(matarajio)	(makisio)
Kilombero ... ..	45,709	45,507	46,000
Kagera ... ..	6,051	3,816	10,000
TPC ... ..	37,022	40,000	40,000
Mtibwa ... ..	19,698	14,000	23,000
Jumla ... ..	108,480	103,323	119,000

**(2) Shirika la Taifa la Kilimo na Chakula (NAFCO)**

Zao (Tani)	1985	1986
Ngano ... ..	46,588	40,548
Mpunga ... ..	19,692	21,592
Mahindi ... ..	8,160	12,350

**Mazao ya Biashara:**

19. Shabaha kubwa ni kuongeza uzalishaji wa mazao ya biashara ili kuweza kusafirisha nchi za nje na pia kujitosheleza mahitaji ya viwanda nchini. Pamoja na kuendelea kuhimiza uzalishaji wa chai na tumbaku kwa wakulima wadogo, jitihada zitaendelezwa katika kurweka msingi imara kuinua uzalishaji wa mazao ya mkonge na korosho hapo baadaye. Hii ni kwa sababu mazao haya huchukua muda kwa matunda yake kuonekana lakini ni budi kwa wakati huu kuendelea kurekebisha makosa yaliyofanywa miaka ya nyuma hadi uzalishaji wa mazao haya ukaanguka.

**(a) Mkonge:**

20. Utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa upande wa zao la Mkonge, unatarajiwa kulenga katika kuendelea kutatua matatizo ambayo yamekabili zao hili kwa karibu miaka kumi. Matatizo hayo ni pamoja na ukojefu wa upandaji upya wa zao ambao umesababisha limbikizo la mahitaji ya upandaji upya hadi kufikia hekta 70,000; uhaba wa vifaa vya usafirishaji na zana za kilimo, matatizo ya uhaba wa wafanyakazi na hasa wakataji mkonge na matatizo ya bei.

21. Hivyo juhudi zitaendelezwa katika kupanda upya zao la mkonge, lengo kwa mwaka 1986/87 likiwa ni kutayarisha hekta 5,000 tayari kwa upandaji, kupanda hekta 5,000 zilizotayarishwa na kuhudumia mkonge ambao haujakomaa wenye hekta 8,175. Shabaha ni kuwa ifikapo mwaka 1988/89 hekta 39,304 zive zimepandwa upya na zao la mkonge. Zaidi ya hayo ili kuvutia wafanyakazi wengi zaidi kujitunga na kubaki katika uendelezaji zao hili, hali ya maisha kwa wafanyakazi itaendelea kuinuliwa kwa kuwauzia chakula kwa bei nafuu na kutumia mapato hayo ili kuwajengea nyumba bora. Lengo katika mwaka 1986/87 ni kukamilisha nyumba 156.

**(b) Chai:**

22. Mamlaka ya Chai itaendelea hasa na miradi ya kuimarisha uzalishaji chai kutoka kwa wakulima wadogo ikiwa ni pamoja na kurekebisha na kupanua viwanda ili kumudu kusindika ongezeko la majani mabichi; kuimarisha shughuli za usafiri hasa wa usombaji majani mabichi kutoka mashamba ya wakulima wadogo hadi viwandani; ukuzaji wa miche kwenye vitalu hasa katika wilaya ya Rungwe ili kufidia hekta 114, kupanda hekta 200 za msitu wa kuni kwa matumizi ya viwanda badala ya mkaa; uajiri wa wataalamu, mafunzo na kumalizia ujenzi wa barabara za chai Njombe.

23. Mamlaka pia inakusudia kuchukua hatua kadhaa ili kuhakikisha kuwa uzalishaji wa chai umeongezeka.

(a) Mamlaka imetayarisha mpango wa kutoa motisha kwenye maeneo ya mashamba makubwa yaendeshwayo na Mamlaka. Nia ya mpango huu ni kuweza kupata fedha za kigeni ili kuendesha mashamba, kuongeza ubora wa huduma mashambani na hivyo kuwavutia wachumaji wengi ili mazao yatakatikana yaongezeka.

(b) Kwa upande wa mashamba ya wakulima, wakubwa binafsi, mamlaka inakusudia kushauriana na Serikali hasa kwa wakulima wale ambao ni dhau ili nao waweze kupata kiasi fulani cha msaada kutoka kwa wahisani nchi za nje ili nao waweze kuimarisha huduma zao na kuongeza uzalishaji. Msaada huu umekuwa nkipewa baadhi ya wakulima binafsi na matokeo yake yamekuwa yakuridhisha.

(c) Mamlaka itaendelea na ujenzi wa nyumba bora na motisha nyingine hasa kwa wachumaji ili waweze kuishi mashambani na kufanya kazi kwa muda mrefu zaidi na vizuri. Hatua hii inategemewa pia kuchukuliwa na mashamba ya watu binafsi.

24. Mategemeo ya ongezeko la uzalishaji wa chai katika miaka miwili ijayo hategemewa kuwa mkubwa kwa vile sekta hii imekusudiwa kutayarisha na kuanza kutekeleza mbinu za kurekebisha shughuli za uendelezaji chai na kukabili matatizo. Matokeo ya mikakati itakayowekwa yatajitokeza kuanzia mwaka 1988/89. Lengo kwa mwaka 1986/87 ni kupata kilo milioni 18 ambapo kiasi cha tani milioni 5.5 zitokata katika mashamba ya Mamlaka na thamani ya mauzo inakadiriwa kuwa Sh. 540 milioni asilimia 80 kati ya hizo zikiwa katika fedha za kigeni.

**(c) Tumbaku:**

25. Shughuli za zao la tumbaku nchini zinahudumiwa na Wizara ya Kilimo na Maendeleo ya Mifugo, kwa upande wa uzalishaji na utoaji huduma kwa wakulima wadogo, vyama vya ushirika katika ununuzi kutoka kwa wakulima na Bodi ya Tumbaku kwa upande wa uteuzi wa zao (classification), mbege bora, mashamba ya maonyesho, usindikaji na uzaji.

Wizara ya Kilimo itaendelea kuwahudumia wakulima wadogo katika masuala ya uzalishaji na ukaushaji kwa lengo la:

(a) Kuongeza uzalishaji kwa kila hekta, kuongeza ubora wa tumbaku na kupunguza uharibifu wa tumbaku wakati wa kukausha

(b) Kupunguza matumizi ya kuni na hatari za kuenea kwa jangwa kwa kuhakikisha kuwa kuni kidogo zitakazohitajika zinapatikana karibu na kusafirishwa kwa urahisi kwa kutumia makasi.

(c) Kuhakikisha kuwa maji yanapatikana kwa urahisi kwa ajili ya miche.

26. Ili kuweza kufikia malengo haya inakusudiwa kujenga mabani ya kisasa 20 katika tarafa 20 za mikoa ya Tabora, Iringa na Mbeya kama kielelezo kwa wakulima wa tumbaku katika maeneo hayo. Mabani haya hutumia kuni chache zaidi ukilinganisha na yale ya sasa na hukausha tumbaku kwa ufanisi zaidi, kutayarisha bustani 5 za miche ya miti Tabora (1), Urambo (2), Iringa (1), na Songea (1) kwa matumizi katika upandaji miti; kuchimba visima 15 vyenye vina vidogo katika vijiji katika mikoa ya Tabora, Iringa na Mbeya.

27. Kwa upande mwingine, Bodi ya Tumbaku inatarajiwa kutoa tani 1,100 za mbegu bora za tumbaku na kwa kushirikiana na Wizara pamoja na Vyama vya Ushirika kuoanisha shughuli za vyombo vyote vinavyohusika na hao hili ili kuongeza uzalishaji. Pia Bodi inakusudia kuendelea kushirikiana na uongozi wamikoa ili kurahisishana kupunguza muda wa kumunua tumbaku kwa kuiga uongozi wa Mkoa wa Tabora ulivyofanya katika msimu uliopita.

28. Matarajio katika kipindi cha 1986/87 ni kuwa hekta zitakazolimwa zitaongezeka kutoka hekta 27,462 hadi hekta 29,331 na tumbaku itakayozalishwa inakadiriwa kuwa tani 12,056 zenye thamani ya Sh. 529.7 milioni.

#### (d) Pareto:

29. Katika kipindi cha 1986/87, Bodi ya Pareto inakusudia kuendelea kutunza na kuendeleza mashamba ya mbegu pamoja na bustani za miche zilizopo ili kupata mbegu za miche ya kutosha na kusambaza kwa wakulima. Lengo katika kipindi hiki ni kuendelea hekta 125 za shamba la mbegu ambalo litazalisha kilo 2,500 za mbegu za pareto. Mbegu hizi zitawezesha kupanda hekta 45 za bustani ya miche na zitakazosalia kusambazwa kwa wakulima.

30. Bodi inakusudia pia kuendelea na ujenzi wa nyumba za wafanyakazi ili wawe karibu na kiwanda ambacho kinafanyakazi usiku na mchana lakini kiko mbali na mji wa Mafinga.

31. Ili kuhakikisha kuwa wakulima wa pareto wanapata zana na pembejeo kwa wakati, inakusudiwa kuanzisha duka moja lenye ghala na nyumba ya kuishi ili liweze kutoa huduma hizo zitakazowawezesha wakulima kuzalisha zaidi.

32. Lengo katika kipindi hiki ni kuzalisha tani 1,600 za mausa, tani 45.5 za crude extract, tani 285 za pyrethrum powder, tani 100 za marc powder na tani 940 za dry mark.

#### (e) Pamba:

33. Lengo la mpango wa mwaka 1986/87 ni kulima jumla ya hekta 400,000 na kuzalisha jumla ya tani 162,000 za pamba ambazo ni sawa na marobota 300,000. Mbinu zitakazotumika ni pamoja na kuhakikisha kuwa pembejeo za kutosha zinawafikia mapema wakulima. Vifaa vya ununuzi na uchambuzi—fedha, magunia, n.k. vinatayarishwa mapema ili kuhakikisha kuwa wazalishaji ambao hasa ni wakulima wadogo wadogo wanaongeza uzalishaji. Hadi sasa bodi ya Pamba imekwisha kupata leseni ya kuagiza kutoka nje magunia na madawa kwa msimu ujao.

34. Kwa upande wa Bodi ya Pamba, juhudi zitaendelezwa katika kurekebisha vinu vya kuchambulia pamba na vya kukamua mafuta ya pamba ili kuongeza ubora wa pamba itakayochambuliwa na mafuta yatakayopatikana. Bodi pia itaendelea na matayarisho ya uendelezaji shamba la Kwamsisi ambalo linatarajia kuchangia nguvu za wakulima wadogo katika uzalishaji pamba nchini.

#### (f) Korosho:

35. Bodi ya Korosho inakusudia kufanya marekebisho ya mashine za kubangulia korosho za TANITA I na kuzimarisha ziweze kutoa korosho zenye ubora wa kimataifa pia inakusudia kufanya matengenezo makubwa ya jengo la kiwanda hicho. Zaidi ya hayo, Bodi inakusudia kumaliza ujenzi wa kiwanda cha Tunduru ili kiweze kutumika mara uzalishaji korosho utakapongezeka katika Wilaya hiyo.

36. Kwa upande wa uzalishaji, kazi hii itaendelea kuendeshwa na wakulima wadogo wadogo kwa kupata ushauri wa kitaalam kutoka Wizara ya Kilimo na Maendeleo ya Mifugo. Shabaha kuu ya programu ya majaribio ya kuongeza ubora wa uzalishaji ni kuimarisha ufoaji huduma za kitaalamu na kuwafunza mabwana shamba na wakulima wa korosho. Shabaha katika mwaka 1986/87 ni kuendelea kuimarisha usafiri wa mabwana shamba kuanzisha mashamba 34 ya mfano; kuendelea bustani zenye uwezo wa kutoa miche 280,000 zinazoweza kupandwa katika eneo la ukubwa wa hekta 700; kuendesha mafunzo kwa mabwana shamba 30 na wakulima 480, kuendelea na shughuli za ushauri kwa wakulima na kuendelea shamba lililopo la mbegu lenye ukubwa wa hekta 400.

#### (g) Kahawa:

37. Katika juhudi za kuendelea kuongeza kiasi cha kahawa inayozalishwa pamoja na ubora wa ile tunayouza nchi za nje kwa kupata fedha za kigeni, juhudi zitaendelezwa hasa katika maeneo matatu:—

- Uendelezaji wa vitalu vya miche. Hadi sasa mahitaji ya miche hayatoshelezi wakulima waliopo na kwa kuzingatia upanuzi wa maeneo yanayoanza kulimwa kahawa hasa katika kanda ya kusini, umuhimu mkubwa utawekwa katika kuendelea uoteshaji na usambazaji wa miche ambayo hutolewa bure kwa wakulima na imekadiriwa kuwa miche 12 milioni itaoteshwa.
- Uendelezaji barabara ndogo (feeder Roads) katika maeneo yanayolima kahawa: Hii itawezesha kuhakikisha usombaji kahawa kutoka kwa wakulima na usambazaji wa zana za pembejeo. Lengo la programu nzima ni kutengeneza km. 12,000 za barabara za aina hii na hadi sasa km. 8,172 zimekwisha kutengenezwa pamoja na madaraja.
- CBD/Pesticides: Ili kupunguza upotevu wa uzalishaji unaotokana na wadudu pamoja na ugonjwa wa CBD hadi kufikia kiwango cha chini (asilimia 10) inakusudiwa kuhakikisha kuwa madawa yanapatikana na kusambazwa mapema, vinginevyo uzalishaji katika kipindi kijacho yatapungua sana.
- Curing Mills: Shabaha ni kupunguza tatizo la usafirishaji wa kahawa laini kwa kusindikwa katika kanda ya kusini na kusafirishwa hadi Dar es Salaam kwa kupeleka katika masoko ya nchi za nje. Hii itaondokana na tatizo la usafiri na upunguaji wa ubora wa kahawa kutokana na kulazimika kusafirishwa kutoka kusini hadi Moshi na daadaye kwenda Tanga. Ujenzi wa vinu viwili, Mbinga na Mbozi unatarajiwa kuendelea kwa nguvu katika kipindi cha 1986/87.

## 2. MIFUGO—

1. Mpango wa mwaka 1986/87 kama Mpango wa mwaka 1985/86 umeelekezwa kutekelezwa na kuimarisha miradi inayoundelea ili ikamilike na kuimarika kwa makusudi ya kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo na mazao yake (nyama, maziwa, mayai, ngozi n.k.) na hivyo kuongeza mchango wa Sekta ya Mifugo katika Uchumi wa Taifa. Miradi itakayotekelezwa ni pamoja na ile ya kuimarisha mifugo ya asili kwa kuipatia huduma muhimu kama vile maji, malisho bora, kuondoa ndorobo, kutumia madume bora, kuongeza uzalishaji wa mitamba ya maziwa, kuimarisha huduma za uzalishaji kwa kutumia chupa, uzalishaji wa wanyama wadogo wadogo, ufoaji wa huduma za afya ya mifugo n.k. Ili kutekeleza miradi yote hii, Idara ya Maendeleo ya Mifugo inategemea kutumia Sh. 93.481 milioni fedha za hapa, Sh. 61.916 milioni fedha za nje na Sh. 111.149 milioni fedha nyingine. Jumla ya fedha zote ni Sh. 266.546 milioni.

#### **Utekelezaji wa Mpango wa mwaka 1985/86:**

2. Katika kipindi cha mwaka 1985/86 sekta ya mifugo ilitengewa jumla ya Sh. 93.576 milioni fedha za hapa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Desemba mwaka 1985 jumla ya Sh. 46.631 milioni au asilimia 49.8 ya fedha zote za maendeleo kwa mwaka huo zilikuwa zimeshatumika na utekelezaji halisi wa miradi ya maendeleo ulikuwa ni asilimia 45.

#### **Matatizo ya Utekelezaji ya Mpango wa 1985/86:**

3. Pamoja na juhudi kubwa zilizofanywa na vyombo mbali mbali katika kuendeleza mifugo nchini katika kipindi cha mwaka 1985/86, malengo ya utekelezaji miradi yaliyowekwa katika kipindi hicho hayakuweza kufikiwa. Utekelezaji wa miradi mbali mbali na uzalishaji mali katika sekta ya mifugo ulikuwa sio wa kuridhisha kama ilivyokuwa katika miaka michache iliyopita. Mwenendo huu usioridhisha ulisababishwa na sababu nyingi. Zifuatazo ni baadhi ya sababu hizo:—

- (a) Upungufu wa vyakula bora vya mifugo hasa vyakula vya kuku, nguruwe na ng'ombe wa maziwa.
- (b) Uhaba wa fedha za kigeni na mara nyingine fedha za hapa ulikwamisha utekelezaji wa miradi kwani huwa vigumu kununua nyanzo na vifaa muhimu madawa ya tiba na kinga kwa mifugo.
- (c) Ukosefu wa vifaa vya ujenzi, pembejeo muhimu na ugumu wa usafiri pia uliathiri utekelezaji wa miradi mbali mbali ya mifugo.
- (d) Uzalishaji maziwa haukuweza kuongezeka sana kama ambavyo ilikusudiwa kutokana na ukosefu wa ng'ombe wa maziwa pamoja na kuwepo kwa "infrastructure" mbaya katika mashamba ya ng'ombe yaliyopo.

#### **Mpango wa mwaka 1986/87:**

4. Katika mpango wa maendeleo na bajeti ya mwaka 1986/87, sekta ya Mifugo itaendelea kutiliwa mkazo mkubwa katika kukamilisha na kuimarisha miradi na huduma zinazoendelea. Uimarishaji wa mashirika yanayoshughulikia maendeleo ya mifugo na bidhaa zake ili yaongeze tija na ufanisi katika uzalishaji mali pia utazingatiwa.

#### **Uzalishaji Mifugo:**

5. Katika kuendeleza mifugo bora kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya wananchi ya mazao ya mifugo, shughuli mbali mbali zitakelezwa katika mpango wa mwaka 1986/87 ambazo ni pamoja na uzalishaji ng'ombe kwa chupa katika vituo vya Arusha (NAIC), Butiama (BAIC), uzalishaji ng'ombe kwa chupa vijijini, uzalishaji mitamba katika vituo vya Mivumoni, Kibaha, Saohill n.k., uzalishaji wa mbegu za majani Langwira—Mbeya. Ili kuongeza uzalishaji wa mbuzi, huduma muhimu zitaongezwa katika kituo cha mbuzi wa maziwa—Moshi, kituo cha mifugo Ngoka—Lindi na kuendeleza mbuzi Newala. Miradi yote hii imetengewa jumla ya Sh. 23.956 milioni fedha za hapa na Sh. 25.376 milioni fedha za nje.

#### **Afya ya Mifugo:**

6. Mpango wa mwaka 1986/87 utaendelea na juhudi za kuimarisha miradi ya afya ya mifugo ili kuongeza mazao ya mifugo. Miradi ambayo itakelezwa ni pamoja na kudunga sindano na kuchanja ng'ombe ili kuzuia magonjwa ya sotoka na magonjwa yakupe, lengo ni kuwachanja ng'ombe 12 milioni mwaka huu, kufufua na kuimarisha majosho, kuimarisha njia za mifugo na kusi mika mizani 150 katika minada yote ya kuuzia ng'ombe. Miradi hii inatarajiwa kutumia Sh. 17.254 milioni fedha za hapa, Sh. 13.000 milioni fedha za nje na Sh. 6.000 milioni fedha nyingine.

#### **Utafiti wa Mifugo (TALIRO):**

7. Shirika la Utafiti TALIRO limepanga kutekeleza miradi ya utafiti wa mifugo katika vituo vyake vya utafiti vya DSM FMD Temeke ADRI, Mpwapwa LPRI, Kongwa PRC, Tse-Tse Ily-Tanga na Taasisi ya utafiti wa malisho Kilosa. Makao Makuu ya muda pia yataimarishwa. Lengo ni kutafiti maradhi mbali mbali kama vile magonjwa ya miguu na midomo, malisho bora na kuwaelimisha wafugaji juu ya matokeo ya utafiti ambao utawawezesha wafugaji hawa waongeze ubora wa mifugo yao. Shirika limetengewa Sh. 12.588 milioni fedha za hapa ili kutekeleza majukumu yake katika kipindi cha mwaka 1986/87.

#### **Kampuni ya Ranchi za Taifa—(NARCO):**

8. Katika kipindi cha mwaka 1986/87 NARCO inategemea kuimarisha ranchi zake sita za Kongwa, Uvinza, Kalambo, Kitangule, Mkata na Dakawa. Shughuli muhimu zitakazotekelezwa ni pamoja na kuimarisha huduma za maji katika ranchi, mawasiliano (ununuzi wa Walkie Talkie) majosho na kulimia barabara za moto. Miradi mingine inayotegemewa kutekelezwa katika kipindi hiki ni kuendeleza ranchi ya Ruvu, kukamilisha Ranchi ya Kielelezo Dakawa, kuendeleza mradi wa Madume wa Boran West Kilimanjaro. Ranchi ya Misenyi nayo itaendelezwa. Miradi yote hii itagharimu Sh. 14.908 milioni toka Serikalini.

#### **Kampuni ya Ng'ombe wa Maziwa (DAFCO):**

9. Katika mpango wa maendeleo wa mwaka 1986/87 DAFCO inakusudia kuendeleza miradi ya ng'ombe wa maziwa katika mashamba ya Kitulo 6 na 7 ambayo yanategemewa kutoa lita 11,000 milioni za maziwa kila mwaka katika kipindi cha muda wa miaka 10 ijayo. Mashamba mengine yatakayohusika ni Malenje—Sumbawanga. Miradi mingine itakayotekelezwa ni uzalishaji mitamba katika mashamba ya Ngerengere na Utegi. Sh. 8.919 milioni zimetengwa kwa ajili ya miradi hii.

#### **Kampuni ya Kuku ya Taifa (NAPOCO):**

10. Kampuni ya Kuku ya Taifa (NAPOCO) inakusudia kutekeleza miradi miwili ya maendeleo katika mwaka wa 1986/87. Miradi hii ni ya kukamilisha ujenzi wa kuku wazazi Arusha na kukamilisha uimarishaji wa Majohe—D'Salaam. Mradi wa kuku Wazazi Arusha utakapokamilika utakuwa na uwezo wa kutoa vifaranga wa kuku wa nyama na majike 120,000 kwa mwaka na kuku wa mayai majike 45,000. Baada ya mradi wa Majohe kuimarishwa utakuwa na uwezo wa kutoa kuku wazazi 60,000 kwa mwaka kutoka uwezo wa sasa wa kuku 40,000. Miradi hii itagharimu jumla ya Sh. 14.556 milioni fedha za hapa na Sh. 18.000 milioni fedha za nje.

#### **Kampuni ya Kusindika Maziwa (TDL):**

11. Kampuni inatarajia kuendelea na ujenzi wa kiwanda cha maziwa cha Mbeya pamoja na kuimarisha viwanda vingine vya Dar es Salaam, Mara Tanga na Tabora ili kuviongezea uwezo wao wa kusindika maziwa. Kampuni inategemea kutumia jumla ya Sh. 29.040 milioni ili kutekeleza miradi hii.

#### **Kampuni ya Ngozi Tanzania (THS):**

12. Katika kipindi cha mwaka 1986/87 Kampuni ya Ngozi itaendelea na mradi wa ukaushaji ngozi katika machinjio yote nchini. Mradi huu utakapokamilika ngozi za ng'ombe 500,000, ngozi 300,000 za mbuzi na ngozi 100,000 za Kondoo zitaweza kukaushwa kwa njia hii kila mwaka. Mwaka huu Kampuni inategemea kutumia Ruzuku ya Sh. 1.300 milioni kutoka Serikalini kutekeleza mradi huu.

#### **Kampuni ya Viwanda vya Nyama (TPL):**

13. Kampuni ya Viwanda vya nyama mwaka huu wa fedha itakuwa na mradi mmoja tu wa kutekeleza ambao ni kuimarisha viwanda vyake vya Kawe, Mbeya na Shinyanga.

### 3.—VIWANDA

#### Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi katika Mwaka 1985/86:

1. Kiasi cha fedha kilichoidhinishwa kwa ajili ya miradi inayotekelezwa chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara ni Sh. 715,258,000/- zikiwa Sh. 232,136,000/ fedha za hapa na Sh. 483,122,000/- fedha za Nje.

Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 1985, kiasi kilichokuwa kimetolewa (amount released) ni Sh. 175,924,000/- zikiwa Sh. 93,800,000/- fedha za hapa na Sh. 82,124,000/- fedha za Nje.

Kwa hiyo kiasi kilichokuwa kimetolewa hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 1985 ni asilimia 40.45 kwa upande wa fedha za hapa na asilimia 17 kwa upande wa fedha za kigeni.

2. Hatua zilzofikiwa kwa upande wa utekelezaji miradi (physical implementation) kwa ujumla kiasi kikubwa cha malengo ya utekelezaji kimetekelezwa hadi kufikia Desemba, 1985. Hata hivyo baadhi ya matatizo yaliyoathiri utekelezaji wa miradi ni:—

- Upungufu wa fedha za hapa na za kigeni.
- uhaba/ukosefu wa vifaa vya ujenzi.
- kuchelewa kuwasili kwa mitambo kutoka ng'ambo.
- ukosefu na uzorotaji wa huduma muhimu za kiuchumi hasa usafirishaji (uhaba wa dizeli kwa miezi ya Novemba na Desemba) na ukosefu wa umeme.

#### Mpango wa Mwaka 1986/87:

##### (a) Malengo ya Mpango:

Mpango wa Maendeleo wa mwaka 1986/87 una malengo yafuatayo:—

- Kuendelea na utekelezaji wa miradi ambayo inaendelea (on going projects) ili iweze kukamilika katika kipindi kilichotarajiwa.
- Kutekeleza miradi itakayowezesha kuongeza ufanisi katika viwanda na sekta nyingine za uchumi.

3. Mpango mzima wa Sekta ya Viwanda na Biashara utagharimu Sh. 1,204.16 milioni. Kati ya jumla hiyo, Sh. 680.6 milioni ni kutoka katika bajeti ya Serikali na Sh. 523.561 milioni ni kutokana na mikopo, mifuko maalum ya makampuni/mashirika yenye-we. Kutoka Serikalini fedha za hapa ni Sh. 248.6 na kiasi cha Sh. 432.60 ni fedha kutoka Nje.

#### Viwanda vya Chuma, Mashine na Zana za Chuma:

Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) litaendelea na Maandalizi ya awali ya uanzishaji wa kiwanda cha chuma kwa kutumia machimbo ya chuma ya Liganga. Maandalizi haya yanahusu ujenzi wa nyumba na ofisi ndogo karibu na mradi wa utafiti na ukusanyaji habari. Ujengaji wa "captive foundry" katika kiwanda cha kutengeneza mashine kilichoko Moshi utaendelea. Kazi hii itakapokamilika kiwanda kitaweza kutengeneza sura na miundi (castings and moulds) ya mashine mbali mbali hapa hapa nchini badala ya kazi hiyo kufanywa nje ya nchi kama ilivyo sasa. Kiwanda cha Mang'ula Mechanical and Machine Tools kitaendelea kuimarishwa kwa kujenga nyumba za wafanyakazi na kujenga upya karakana ambazo zimeharibika kutokana na mvua.

#### Viwanda vya Nguo:

Viwanda vya nyuzi vya Tabora na Ubungo ambavyo karibu asilimia 50 ya nyuzi zake zitakuwa zinanzwa nje vilianza kujengwa mwaka 1978 bado havikamilika. Vimetengewa fedha kwa ajili ya shughuli za ukamilishaji, zikiwa ni pamoja na kuwalipa makontrakta. Vinatarajiwa kukamilika Desemba, 1986. Ujenzi wa Kiwanda cha nguo cha Mbeya upo katika hatua za mwisho na umetengewa fedha za kumaliza.

#### Viwanda vya Bidhaa za Ujenzi:

Ujenzi wa Mradi wa chupe (Nyanza Glasswares) ulioko Mwanza utaendelea kwa kukamilisha jengo la kiwanda na nyumba za wafanyakazi, nao mradi wa vigae wa Arusha umetengewa Sh. 15 milioni fedha za hapa na Sh. 15.0 milioni fedha kutoka Bulgaria kwa ajili ya utekelezaji.

#### Viwanda vya Madawa:

Maandalizi ya ujenzi wa Kiwanda cha madawa ya kuulia wadudu waharibuo mimea yamekamilika. Kiwanda kitaanza kujengwa kwa ushirikiano baina ya AISCO, NCI na TCMB (Pamba), Mwaka 1986/87 serikali kupitia NCI itatoa Sh. 12.5 milioni, mkopo kutoka Italy utakuwa Sh. 92.1 milioni ambapo mchango wa AISCO, TCMB na mkopo kutoka TIB ni Sh. 57 milioni. Bohari za TFC zitakazojengwa Sumbawanga, Songea na Mbeya, zenye uwezo wa kuhifadhi tani 10,000 kila moja, zimetengewa Sh. 6 milioni fedha za hapa ambapo mchango wa Netherlands katika mradi huu unatarajiwa kuwa Sh. 47.65 milioni.

#### Viwanda vya Ngozi:

Viwanda vya ngozi na bidhaa za ngozi zinasimamiwa na Shirika la Viwanda vya Ngozi (TLAI). Viwanda hivi vimekuwa vikikabiliwa na matatizo ya upatikanaji wa ngozi kutoka kwa wafugaji na malighafi nyingine kutoka nje. Utekelezaji wa mradi wa Morogoro Leather Board na mradi wa kutoa kemikali zinazotokana na mkusanyiko wa viwanda vya Morogoro utaendelea.

#### Viwanda vya Karatasi:

Viwanda vya National Printing Company, Kibo Paper Industries Ltd. na Printpak (T) Ltd. vitafanyiwa matengenezo (rehabilitation) ili kuongeza uwezo wa uzalishaji. Kazi hii itafanywa kwa msaada wa Sweden. Fedha za hapa Sh. 14.8 milioni zimetengwa ili kufanya kazi zinazohitaji fedha za hapa.

Uwezo wa viwanda vya uchapishaji wa kutoa vitabu na magazeti umethiriwa vibaya na uhaba wa huduma za "typesetting". Mradi wa typesetting upo katika hatua za mwisho za ukamilishaji na umetengewa Sh. 3 milioni ili kukamilisha mradi.

#### Viwanda vya Chakula, Vinywaji na Sigara:

Baada ya fedha za kigeni kupatikana kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha bia cha Mwanza, Sh. 20 milioni fedha za hapa zimetengwa ili kuanza ujenzi. Mkopo kutoka Chekoslovakia Sh. 22.35 milioni unatarajiwa kutumika mwaka 1986/87.

Kampuni ya Sigara itatumia Sh. 66.5 milioni kwa miradi mbali mbali ikiwa ni pamoja na Sh. 20.0 milioni kwa ujenzi wa nyumba za wafanyakazi, na Sh. 30.0 milioni kwa ajili ya mashine za vifaa.

#### Viwanda Vidogo:

Uendelezaji wa mitaa ya viwanda (industrial estates) Morogoro, Iringa, Mbeya, Shinyanga, Tabora na Mtwara utaendelea kwa ujenzi wa mabanda, kununua na kufunga mitambo na kununua malighafi. Ujengaji wa "Common facility workshops" na "foundries" utaendelea, pamoja na uendelezaji wa teknolojia vijijini. Miradi ya viwanda vidogo imetengewa jumla ya Sh. 89.6 milioni, kati ya hizo Sh. 20.5 milioni zikiwa fedha za hapa na Sh. 69.1 milioni zikiwa fedha za nje.

#### Huduma za Viwanda:

Maendeleo ya sekta ya viwanda na maendeleo ya uchumi kwa ujumla yanahitaji huduma bora za viwanda. Huduma hizo hutokana na taasisi za uchunguzi, taasisi za utafiti, taasisi za kubuni mitambo na mashine na taasisi za kusimamia ubora wa bidhaa. Taasisi hizo ni Shirika la Viwango vya Bidhaa (TBS), Kituo cha Kujaribia Zana za Kilimo (CAMARTEC), Shirika la Utafiti wa Viwanda (TIRDO) Shirika la Ushauri wa Viwanda (TISCO) na Shirika la Kubuni mitambo ya Uhandisi na Umakenika. Taasisi hizi zitaendelea na ujenzi wa maabara, ofisi na nyumba za wafanyakazi, na ununujaji wa zana za kazi.

#### Makampuni ya Biashara:

Makampuni ya biashara chini ya Bodi ya Biashara ya Ndani (BIT) yatautumia fedha zao na mikopo kutoka THB, CRDB, Karadha na NPF. kujenga maofisi, mabohari, nyumba za wafanyakazi na kununulia magari. Makampuni ya Biashara ya Mkoa (RTCs) ya Arusha na Morogoro yanatarajiwa kujenga Supermarkets, ambapo Tanga RTC inatarajia kujenga mkahawa na duka sehemu za Horohoro kwa kutumia Sh. 7.9 milioni.

Kampuni ya BHESCO imetenga Sh. 10.0 milioni kwa ajili ya kushiriki kwake katika mradi wa Sheet Glass na Sh. 2.0 milioni kwa ajili ya Morogoro Ceramics. Kampuni ya HOSCO itatumia Sh. 10.0 milioni kwa ajili ya mradi wa Shamba la Mafura.

#### 4.—MALIASILI

##### Utangulizi:

1. Katika kuzingatia hali ngumu inayoikabili nchi zetu kwa hivi sasa, sekta ya Maliasili katika mpango wa 1986/87 itaendelea na kuimarisha shughuli zilizopo ili kuongeza uzalishaji na kutoa huduma bora za kiuchumi. Hata hivyo sekta hii itatekeleza, baadhi tu ya malengo yaliyowekwa kulingana na kiwango cha fedha kilichotengwa ambacho ni pungufu kuliko cha mwaka 1985/86.

##### Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 1985/86:

2. Utekelezaji katika kipindi kilichopita haukuwa mzuri sana kutokana na matatizo yaliyoikumba nchi yetu ya ukosefu wa fedha za kigeni, vipuri, malighafi kwa viwanda na nyenzo nyingine za kufanyia kazi. Kwa hiyo hali ya utekelezaji wa sekta hii ulikuwa wa chini sana. Hali hii ikiendelea itazidi kuleta wasi wasi katika kipindi kijacho cha 1986/87 endapo hatua madhubuti hazitachukuliwa.

##### Mpango wa Maendeleo 1986/87:

3. Katika mpango wa mwaka 1986/87, sekta ya Maliasili na Utalii itatilia mkazo wa upandaji wa miti ya aina zote, sorovea na upimaji, uvunaji na barabara, hifadhi ya ardhi na misitu, uvunaji wa samaki, mafunzo katika fani mbali mbali, uendelezaji wa mbuga za wanyama pori na nyuki. Vile vile huduma katika mahoteli zitaimarishwa ili kuwavutia watalii waingie nchini kwa wingi na kutupatia fedha za kigeni. Viwanda vya mbao vitaimarishwa kwa kuvipatia vifaa, kurekebisha mitambo na ushauri ili kuvipa uwezo zaidi wa kuongeza uzalishaji ambao umedidimia.

4. Shirika la Utalii litaendelea na shughuli zake za kuzimarisha hoteli zote za kitalii ikiwa ni njia mojawapo ya kutoa huduma bora kwa watalii.

Mpango huu utaigharimu serikali Sh. 93.0 milion za hapa.

Miradi itakayotekelezwa mwaka 1986/87 ni kama ifuatavyo:

##### Wanyamapori:

5. Ili kulinda na kuhifadhi maliasili ya wanyamapori tulionao kwa kukuza biashara ya utalii, kuvuna wanyama hao kwa kito-weo na kuuza nyama nje ya nchi kwa kuingiza fedha za kigeni, kazi muhimu zitakazofanyika ni kuimarisha mawasiliano katika mbuga zote. Pia juhudi kubwa itafanyika ya kuwapatia walinzi vifaa na nyumba bora. Kwa hiyo barabara zote, viwanja vya ndege 13 na madaraja vitaimarishwa. Ununuzi wa magari ambayo ni tipa, Landrover na lori utafanyika. Kambi 2 za doria zitajengwa na majengo ya walinzi yatarebishwa. Jumla ya Sh. 25.5 milioni zitatumika.

##### Uvuvi:

6. Matatizo ya wataalam na ukosefu wa zana za uvuvi yamekuwa kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya sekta ya uvuvi. Kwa hali hii mkazo mkubwa utatiliwa katika kuimarisha vyuo vya uvuvi ambavyo ni Mbegani, Kunduchi na Nyegezi. Vile vile kuimarisha viwanda vya mashua vilivyoko Mikindani, Kigoma na Mwanza kwa kuvipatia vipuri, malighafi na majengo. Katika kukomesha uvuvi haramu ambao umeeenea hivi sasa, vikosi vya kuzuia uvuvi huo vitapatiwa gari moja na "speedboat" moja.

7. Taasisi ya Utafiti wa uvuvi itaendelea na kazi zake za utafiti wa uvuvi. Taasisi hii pia itanunua vifaa zaidi vya uvuvi. Shirika la Uvuvi litashughulikia kumaliza ujenzi wa mahali pa kuzihudumia meli zake (shorebase facilities) na kujenga ukuta kando ya bahari ambako kuna hatari ya mmomonyoko wa udongo unaoweza kubomoa majengo hayo.

Miradi ya sekta ya uvuvi imetengewa Sh. 13.0 milioni katika mwaka huu.

##### Misitu:

8. Malengo ya mwaka 1986/87 kwa sekta ya misitu na nyuki yatakuwa kuhimiza upandaji wa miti ili kukidhi mahitaji ya malighafi kwa viwanda, kuhifadhi misitu ya asili kwa kuhifadhi ardhi na maendeleo ya kilimo na kukidhi mahitaji ya wananchi ya kuni, mkaa, ujenzi n.k. Kazi hizo zimekuwa zikisisitizwa mara kwa mara lakini utekelezaji umekuwa unalegalega kwa sababu ya matatizo mbali mbali hasa ukosefu wa zana, wataalam, fedha na usafiri.

9. Kwa hiyo upandaji wa miti ya aina zote utaendelea katika mashamba ya taifa na vijiji. Vyuo vya misitu vitaimarishwa kwa kupatiwa vifaa na kuimarisha majengo. Taasisi ya utafiti wa misitu itaendelea na shughuli zake za utafiti.

Malengo na shabaha kwa kila mradi yameelezwa hapa chini:—

10. Mradi mkubwa wa upandaji wa misindano huko Sao Hill utaendelezwa kwa kupanda miti, kupalilia mashamba kutayarisha mashamba na kuotesha miche. Uimarishaji wa barabara za moto na kazi za uvunaji utafanyika pia. Upimaji wa mashamba na sorovea utaendelezwa pia. Mradi umetengewa Sh. 8.0 milioni.

11. Kwa upande wa upandaji misindano sehemu zingine kazi kubwa zitakazofanyika ni kupunguza miti, kupogoa na kurudisha miti. Barabara za moto katika mashamba haya zitaimarishwa. Mradi umetengewa Sh. 3.5 milioni. Upandaji wa miti ya mbao ngumu utafanyika huko Longuza na Mtibwa pia kuotesha miche, kupunguza miti na kuimarisha barabara za kuzuia moto. Kwa kiasi cha Sh. 1.5 milioni.

12. Upandaji wa misitu ya hifadhi utaendelea kwa kupanda miti kando kando ya mipaka na kuhifadhi mabwawa ya Mindu na Kidatu. Mradi wa kuhifadhi ardhi Dodoma utaendelea kwa kuotesha miche, kununua vifaa vya kazi, kupanda na kupogoa miti. Pia itatengenezwa mikanda katika mashamba ya kilimo cha mchanganyiko. Mradi umetengewa Sh. 1.0 milioni.

13. Upandaji wa misitu vijijini utaendelezwa kwa kuendeleza semina za kutumia majiko ya kisasa kuchapisha na kusambaza vitabu mashuleni, kuimarisha ofisi na bohari. Mradi umetengewa Sh. 1.1milion. Vile vile upandaji wa miti huko Shinyanga ili kukabili ukame au kuenea kwa jangwa utafanyika kwa kutumia Sh. 10.0m.

14. Vyuo vya misitu ambavyo vinatoa wataalamu wa fani za misitu vya Olmotonyi na Moshi vitaimarishwa kwa kuvipatia vifaa, mitambo na magari. Kituo cha mafunzo ya majaribio ya vitendo kwa ajili ya wanafunzi wa shule ya viwanda—Moshi kitajengwa huko kwenye msitu wa West Kilimanjaro. Vyuo vyote viwili vimetengewa Sh. 1.66 milioni.

15. Taasisi ya utafiti wa misitu itaendelea na kazi za utafiti kwa kuimarisha maeneo ya majaribio. Taasisi hii vile vile itapatiwa vifaa vya kazi, madawa na usafiri. Kiasi cha Sh. 2.9 milioni kimetengwa kwa kazi hizo.

16. Upimaji wa misitu utafanyika huko Iringa na Singida. Uhesabu wa miti utafanyika huko Morogoro. Longuza, Mtibwa na Rubere. Vifaa zaidi vya upimaji vitanunuliwa. Mradi huu umetengewa Sh. 0.9m.

17. Mradi wa uvunaji na barabara utapatiwa vifaa kwa ajili ya mashamba yote ya misitu. Mradi huu umetengewa Sh. 3.5 milioni. Jumla ya Sh. 36.0 milioni zimetengwa kwa ajili ya sekta yote ya misitu.

#### Nyuki:

18. Sekta ya nyuki inakabiliwa na tatizo la vifaa na wataalamu. Kwa hali hii kazi ya kutengeneza mizinga (transitional) kwa ajili ya kuendeleza sekta hii utafanyika. Vile vile ujenzi wa maabara na nyumba za watumishi kwenye Chuo cha Nyuki utafanyika, Chuo kitapatiwa vifaa vya kinga pia. Jumla ya Sh. 0.7 milioni zimetengwa kwa sekta nzima.

#### Viwanda vya Mbao:

19. Viwanda vyote vya mbao vinakabiliwa na matatizo ya ubovu au uchakavu wa mitambo pamoja na uendeshaji. Matatizo haya yamesababisha kushuka kwa uzalishaji. Kwa hali hii kazi kubwa zitakazofanyika ni kuviimarisha kwa kuvipatia vifaa, ushauri na mafunzo yatakayotolewa na wataalamu wa nje. Vifaa hivyo ambavyo ni mashine za kupasulia mbao vitapelekwa kwenye viwanda vya mobile sawmills za West Kilimanjaro na Mbeya. Ushauri na mafunzo yatakayotolewa kwenye viwanda vya Fibreboard Africa na Sikh Sawmill ambapo kazi ya kuimarisha itafanyika kwenye kiwanda cha Kilimbers. Kiasi cha sh. 2.5 milioni zimetengwa kwa mwaka huu.

Sekta ya Maliasili na Utalii imetengwa Sh. 90.0 milioni katika mpango huu.

### 5.—MADINI

Mchango wa sekta ya madini kwa Pato la Taifa bado hauiridhishi. Ufanisi usioridhisha umcendelea kuwa mbaya zaidi hasa baada ya migodi ya zamani yenye kutegemewa sana ya Mwadui na Nyanza kuanza kupata hasara, licha ya kutumia zaidi ya wastani wa asilimia 50 ya uwezo uliopo. Pia migodi mipya ya dhahabu ya Buckreef na Phosphates ya Minjingu bado inaendeshwa kwa hasara. Ufanisi mbaya wa sekta unasababishwa na matatizo yafuatayo:—

- (i) Utayarishaji mbaya wa miradi ambayo ikamilikapo haizalishi ipasavyo. Kwa mfano migodi ya Buckreef na Minjingu
- (ii) Upungufu wa wataalamu wa kuendesha na kuendeleza miradi ya uchunguzi na uchimbaji wa migodi.
- (iii) Mchango wa wachimbaji binafsi wa migodi midogo midogo umcendelea kutelema kutokana na kukosa mashine, vifaa na zana za kutosha. Pia bei ndogo inayotolewa na Serikali haiwaridhishi wachimbaji ili kuendelea na uchimbaji.

Mwaka wa 1986/87 Serikali itaendelea kutekeleza malengo na shabaha za Mpango wa Kwanza wa Muungano wa Maendeleo wa Miaka Mitano, hasa katika kuimarisha miradi yenye matatizo, kupanua migodi iliyopo, kukamilisha na kuendeleza migodi mipya, uchunguzi wa madini na kutoa mafunzo ya wataalamu kwa gharama ya Sh. 221 milioni fedha za hapa na Sh. 74.8 milioni fedha za nje, kama ifuatavyo hapa chini:—

#### Idara ya Madini:

Idara ya Madini itatekeleza miradi saba ambayo ni Uchunguzi wa Madini sehemu Maalum, Uchunguzi kwa 'Helicopter', ujenzi wa Maabara ya Madini, Chuo cha Utafiti Madini Dodoma, Gold Basemetal na Agro-Geology. Miradi yote imetengewa Sh. 10,6 milioni fedha za hapa na Sh. 10 milioni fedha za nje.

#### Shirika la Madini (STAMICO):

Shirika la Madini mwaka 1986/87 litaendelea na uchunguzi wa madini, kuimarisha na kupanua migodi iliyopo na kujenga migodi mipya. Mwaka huu, miradi kumi na moja itatekelezwa kwa gharama ya Sh. 211.5 milioni fedha za hapa na Sh. 74.8 milioni fedha za nje.

Mradi wa chumvi wa Uvinza ulitegemewa kukamilika mwezi Juni 1986 na kuanza kufanya kazi mapema mwezi Julai 1986. Uwezo wa mgodi kuzalisha chumvi ni tani 60,000 kwa mwaka. Mradi wa chumvi wa Mwambao utatumia Sh. 24.5 milioni fedha za hapa kwa kuli pia gharama za mashine na zana zilizopo bandarini, ununuzi wa mashine, ujenzi wa mabeseni ya kukaushia chumvi na ujenzi wa nyumba za wafanyakazi. Utekelezaji wa miradi unategemea kuendelea vizuri mwaka huu baada ya kupata mkopo kutoka Italia wa Sh. 16 milioni fedha za nje kwa matumizi ya mwaka huu. Mradi utakapokamilika utakuwa na uwezo wa kutekengeneza tani 100,000 za chumvi kwa mwaka.

Kuna miradi mitatu ya makaa ya mawe nayo ni Kiwira, Ilima na Kabulo. Miradi yote itakapokamilika itakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 888,000 kwa mwaka. Mahitaji ya makaa ya mawe kwa sasa ni karibu tani 40,000 kwa mwaka na iikapo mwaka 1990 mahitaji yanakisiwa kuwa tani 850,000 kwa mwaka. Miradi yote mitatu kwa pamoja imetengewa kutumia Sh. 155 milioni fedha za hapa na Sh. 37.1 milioni fedha za nje.

Mradi wa makaa ya mawe wa Kiwira utakapokamilika mwaka 1987/88 utakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 150,000 kwa mwaka. Mwaka 1986/87 mradi umetengewa Sh. 135 milioni fedha za hapa na Sh. 17.1 milioni fedha za nje kwa ajili ya ujenzi wa mgodi, barabara, usanii na ujenzi wa nyumba za wafanyakazi na majengo ya mgodi.

Mwaka 1986/87 mradi wa Ilima utaendelea kupanuliwa kutoka uwezo wa tani 12,000 kwa mwaka mpaka tani 48,000 kwa mwaka kwa kutumia Sh. 6 milioni fedha za hapa. Shughuli zitakazofanyika ni ununuzi wa vifaa vya ujenzi na uchunguzi na kutathmini 'coal ore reserves'.

Mradi wa Kabulo utakapokamilika utakuwa na uwezo wa kutoa tani 690,000 kwa mwaka. Sh. 14 milioni fedha za hapa na Sh. 31 milioni fedha za nje zitatumika kwa shughuli za uchunguzi na kutayarisha 'feasibility study'.

Pugu Kaolin Inazalisha na una uwezo wa kuzalisha tani 5,000 kwa mwaka. Sh. 4 milioni fedha za hapa na Sh. 1.5 milioni fedha za nje zimetengwa mwaka huu ili kumaliza upanuzi wa mradi kufikia uwezo wa tani 12,000 kwa mwaka. Kazi zitakazofanyika ni kujenga nyumba tano za wafanyakazi, kuweka (installation) mitambo na vifaa vipya. Mradi wa Pugu Kaolin II ulisimamishwa uendelezaji miaka miwili iliyopita kwa sababu ya kukosa mfadhili wa fedha za nje. Mwaka 1986/87 mradi utaendelea kutekelezwa baada ya Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) kukubali kutoa mkopo. Kazi zitakazofanyika ni kutayarisha eneo, ujenzi na usanii kwa gharama ya Sh. 13 milioni fedha za hapa na Sh. 5 milioni fedha za nje. Mradi utakapokamilika utakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 36,000 kwa mwaka. Madini ya Kaolin ni muhimu kwa Viwanda vya Karatasi, Kioo, Ngozi, Madawa na Rangi.

Mgodi wa Minjingu unazalisha phosphates ambayo ni malighafi muhimu ya kiwanda cha Mbolea Tanga, T.F.C. Mwaka 1985 mgodi ulizalisha tani 21,000. Mwaka 1986/87 shughuli za ujenzi wa nyumba za wafanyakazi, zahanati, duka na usambazaji wa maji na umeme zimetengewa Sh. 10 milioni fedha za hapa na Sh. 15.2 milioni fedha za nje.

Mradi wa magadi wa Ziwa Natron uko Mkoa wa Arusha. Magadi ni malighafi muhimu inayotumiwa na viwanda vya Karatasi, Sabuni, Nguo na 'Caustic Soda'. Mradi unategemewa kuzalisha tani 30,000 kwa mwaka hapo utakapokamilika mwaka 1988. Shilingi 3 milioni fedha za hapa zimetengwa mwaka 1986/87 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za wafanyakazi Monduli Karakana, uimarishaji wa barabara, usambazaji wa maji na umeme ujenzi wa 'Condensers and Crystallizers'.

Kazi za uchunguzi za miradi ya mawe ya thamani Nzege Basemetal na Samena Pyrite kwa pamoja zitaendelea kwa kutumia shilingi 2 milioni fedha za hapa.

**A. Biashara:**

Uzalishaji mdogo katika Sekta za Kilimo na Viwanda, pamoja na ukosefu wa fedha toka nje, vimesababisha upungufu mkubwa wa bidhaa hapa nchini. Hali hii imeathiri vibaya sekta ya biashara, licha ya unafuu uliopatikana kutokana na bidhaa zilizo-ruhuswa kuingizwa na watu binafsi wenye fedha zao za kigeni. Bidhaa chache sana ziliagizwa toka nje na Makampuni ya Biashara ya Taifa (NTCs) kufidia pengo la bidhaa zinazozalishwa humu nchini.

2. Katika mwaka 1986/87 Wizara ya Viwanda na Biashara na Mashirika yake itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali yenye lengo la kuimarisha huduma za Biashara nchini. Kutekeleza lengo hili sekta ya Biashara itaendelea kuimarisha njia za kuhifadhi na kusambaza bidhaa kwa wananchi wote.

3. Bodi ya Biashara ya Ndani (BIT) na Kampuni za Biashara za Taifa itatumia kiasi cha Sh. 363.540 milioni kwa miradi iliyo chini yake na ile iliyo chini ya Mashirika yake. Fedha hizo zitataka kwenye mfuko wake. Makampuni ya Taifa (AISCO, BCS, BHESCO, HOSCO, NAPCO, S and O) yanategemea kutekeleza miradi ya ujenzi wa nyumba za wafanyakazi na super markets. Kampuni za Biashara za Mikoa RTCs zitatumia fedha kwa ajili ya kununulia magari, ujenzi wa ofisi na mabohari.

4. Ili kuthibitisha biashara na nchi majirani, Vyama vya ushirika, mashirika ya umma na vikundi vya watu binafsi vitaendelea kufungua maduka na kutoa huduma nyingine kwenye vituo vikubwa vya mipakani mwetu. Nia ya Serikali ni kuwa na maduka na masoko mengi yenye bidhaa nyingi na za aina mbalimbali upande wetu wa mpakani, ili wananchi wanaohitaji bidhaa ndogo ndogo wasilazimike kuzifuata kwa majirani na kuvusha bidhaa muhimu kama zile zinazotupatia fedha za kigeni.

**B. Utalii:**

5. Kazi ya kukiimarisha Chuo cha mafunzo ya hoteli na utalii kilichiko Dar es Salaam itaendelea. Chuo kitapatiwa vifaa vya mafunzo na kurekebisha majengo ya chuo ambayo yako katika hali mbaya. Pia ujenzi wa hoteli ya New Afrika awamu ya tatu utaendelea chini ya Shirika la Utalii. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwaka huu wa fedha ikiwa vifaa vyote vitapatikana. Sekta hii imetengewa Sh. 16.0 milioni za hapa na Sh. 4.5m- za nje.

**7.—ARDHI****A. Utangulizi**

1. Sekta ya ardhi inahusu mipango miji upimaji na ramani, uthamini wa ardhi, mifereji ya maji machafu, maendeleo ya nyumba na utafiti wa nyumba na vifaa vya ujenzi.

2. Katika kipindi cha 1985/86, umuhimu mkubwa ulielekezwa kwenye upimaji wa maeneo ya vijiji na utayarishaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Lengo lilikuwa ni kuwezesha kutoa hati za kumiliki ardhi ambazo zinatanzamiwa kuwa zitahamasisha uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo, misitu na hifadhi ya ardhi kulingana na matakwa ya Sera ya Kilimo. Mpango wa mwaka 1985/86 pia ulijihusisha na uimarishaji wa huduma za uondoaji wa maji machafu upimaji wa mipaka kati ya Tanzania na nchi za jirani utayarishaji wa mipango kabambe ya miji na upanuzi na uimarishaji wa vyuo vya mafunzo ya ardhi.

3. Kipindi cha 1985/86 kimeshuhudia mafanikio makubwa katika mradi wa uimarishaji mifereji ya maji machafu Dar es Salaam ambao asilimia 90 ya kazi zilizodhamiriwa kwa kipindi hiki zilikamilika na kuufikisha mradi kwenye asilimia 60 ya utekelezaji. Miradi mingi ya ardhi imekuwa na utekelezaji usioridhisha kutokana na matatizo kadhaa yakiwemo ya migogoro ya mipaka hasa katika upimaji wa maeneo ya vijiji, upungufu wa vifaa vya kitaalam, upungufu wa fedha ambao umesababisha kusimama kwa utekelezaji wa mradi wa mifereji ya maji machafu—Morogoro na usanii wa mifereji ya maji machafu—Mbeya. Matatizo mengine yamekuwa ni upungufu wa mafuta ya gari, matairi na magari na ya kusafirisha watu na vifaa kwenye maeneo ya kazi ambayo mara nyingi huwa mbali na ofisi za ardhi. Pia kwa upande wa mipaka kati ya Tanzania na nchi za jirani za Burundi, Kenya, Malawi, Msumbiji na Uganda, utekelezaji haukuridhisha kutokana na ushirikiano mdogo kutoka kwa nchi jirani katika suala hii.

4. Mpango wa maendeleo wa mwaka 1986/87 umeendelea kusisitiza umuhimu wa upimaji wa maeneo ya vijiji ikizingatiwa matokeo ya shughuli hizi katika kilimo matumizi bora na hifadhi ya ardhi. Maelezo ya Mpango wa 1986/87 ni kama yafuatayo:

**B. Upimaji na Ramani:**

5. Katika mpango wa maendeleo wa mwaka 1986/87 kazi zitakazofanywa chini ya mradi wa upimaji na ramani ni upimaji vijiji katika mikoa ya Mtwara, Tanga, Shinyanga, Ruvuma, Arusha, Kilimanjaro na Morogoro pamoja na upimaji wa mpaka kati ya nchi yetu na Kenya, Uganda, Burundi, na Msumbiji kazi ambazo kwa pamoja zimetengewa jumla ya Sh. 6.5 milioni.

**C. Mipango Miji:**

6. Katika mwaka wa maendeleo 1986/87 mpango kamambe kwa mji wa Arusha utaendelea kutekelezwa. "Physical Plans" kwa mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha zitakamilishwa na kuanza utekelezaji wa "Land use plans" kwa maeneo ya Loliondo na Tabora. Shughuli za "physical" na "land use plans" sasa zitasimamiwa na "Lands use planning commission". Ili kutekeleza sera ya kilimo kikamilifu mpango huu unatijia mkazo matumizi bora ya ardhi. Katika mwaka 1986/87 maeneo ya vijiji ya mikoa mmoja wa Tanzania bara yatapimwa na wananchi kukabidhiwa hati za kumiliki maeneo hayo. Pamoja na miradi hiyo, mradi wa "Environmental protection" wenye madhumuni ya kufanya utafiti wa chanzo cha mmonyocho wa pwani ya Dar es Salaam utatekelezwa. Kati hizi zimetengewa jumla ya shilingi milioni 10.0

**D. Uthamini wa Ardhi:**

7. Katika mpango wa maendeleo wa 1986/87 mradi wa uthamini wa ardhi utaendelea kutekelezwa ili kuiwezesha serikali kutoa orodha sahihi za thamani za kiuchumi za ardhi. Hii itaiwezesha serikali kutoa na kupanga kodi halali za viwanja kulingana na shughuli za kiuchumi zitakazokuwa zinaendeshwa kwenye maeneo hayo. Mikoa itakayoshughulikiwa katika mpango huu ni Mwanza, Mara na Kagera. Jumla ya shilingi milioni 0.82 zimetengwa kwa kazi hii.

**E. Mifereji ya Maji Machafu:**

8. Miradi itaendelea kutekelezwa katika Mikoa ya Morogoro, Mbeya na Dar es Salaam katika kipindi cha 1986/87. Kazi zitakazofanywa katika mji wa Morogoro ni kuchimba mifereji ya maji machafu katika sehemu ya kati ya mji pamoja na kujenga mabwawa ya maji machafu nje kidogo ya mji huu. Katika mji wa Mbeya usanii utakamilishwa. Katika mji wa Dar es Salaam kazi zitakazofanywa ni pamoja na kuendeleza ujenzi wa mabwawa ya kusafisha maji machafu yaliyopo vingunguti, Chuo Kikuu na Airwing; kuendelea na ujenzi wa vyoo bora; kuzibua na kusafisha mifereji ya maji machafu ya eneo la Muhimbili, Chuo Kikuu, na Airwing, na kufunga mashine mpya ya kusukuma maji machafu katika kituo cha Chuo Kikuu na Airwing. Mradi wa "Storm



water drainage" Dar es Salaam wenye madhumuni ya kuzuia uchafu na mchanga unaobebwa na maji ya mvua kwenye mifereji ya maji machafu utatekelezwa katika kipindi cha 1986/87. Pamoja na miradi hii hapo juu mradi wa "Environmental sanitation" wenye madhumuni ya kujenga vyoo bora (VIP latrines) na kuelimisha wananchi juu ya mazingira bora, utaendelea kutekelezwa katika mji wa Tanga. Miradi yote hii imetengwa jumla ya Shilingi milioni 18.7 za hapa na shilingi milioni 16.4 za nje.

#### F. Nyumba na Makazi:

9. Shirika la Nyumba limetenga jumla ya Sh. 28.3 milioni kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa nyumba zikiwemo za Buguruni, Tabata, Dodoma, Morogoro, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na ofisi ya Tanga. Pia, Sh. milioni 3.0 zimetengwa ili kukamilisha bohari na ujenzi wa daraja na ufugaji wa simu kwa ajili ya kiwanda cha matofali—Kisarawe.

11. Kituo cha utafiti wa nyumba na vifaa vya ujenzi kimetengwa Sh. 3.6 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za vielelezo na utafiti wa vifaa vya ujenzi katika kipindi cha 1986/87.

12. Mradi wa kulipatia huduma za makazi eneo la Tegeta utaendelezwa na Sh. 4.0 milioni zimetengwa kwa ajili hiyo.

#### G. Mafunzo:

13. Kazi za ujenzi zinazohusu upanuzi na marekebisho ya chuo cha Ardhi cha Dar es Salaam na Morogoro zimetengwa jumla ya Sh. 9.8 milioni katika kipindi cha 1986/87 zikiwamo Sh. 7.8 milioni za hapa na Sh. 2.0 milioni za kigeni. Chuo cha Ardhi Tabora kimetengwa Sh. milioni 1.2 ili kuendeleza ujenzi wa madarasa katika mpango wa maendeleo wa 1986/87.

## 8.—UJENZI

### A. Utangulizi

1. Sekta hii inahusu uimarishaji, matengenezo na ujenzi upya wa njia za uchukuzi, zikiwamo barabara, viwanja vya ndege na vivuko. Pia inahusu karakana za matengenezo ya zana za ujenzi na magari, ujenzi na uimarishaji wa nyumba na ujenzi wa makao makuu.

2. Ni dhahiri kuwa matatizo ya uchukuzi na usafiri ni miongoni mwa matatizo ambayo kwa kiasi kikubwa yanachangiwa na kutopitika nyakati zote za mwaka kwa njia za uchukuzi ambako nako kunatokana na ubovu wa barabara na madaraja. Ili kuchangia katika ufumbuzi wa matatizo haya, katika kipindi cha 1985/86 umuhimu wa kwanza katika sekta ya ujenzi ulitolewa kwa miradi iliyokuwa inaendelea ya matengenezo, uimarishaji na ujenzi mpya wa barabara, na viwanja vya ndege. Kukamilika kwa barabara ya Songea—Makambako yenye urefu wa KM. 313 na daraja la Kirumi ni baadhi tu ya mafanikio ya mwelekezo huo wa juhudi.

Licha ya mafanikio yaliyopatikana kipindi cha 1985/86 pia kilishuhudia matatizo kadhaa ya utekelezaji wa miradi ya sekta hii yakiwamo yale ya uhaba wa vifaa vya ujenzi, lami, ubovu wa zana za ujenzi na hasa ukosefu wa fedha za kigeni ambao umesababisha kutokuanza kwa utekelezaji wa baadhi ya miradi kama vile wa barabara ya Arusha-Minjingu na kuendelea kusimama kwa shughuli za usimikaji mitambo ya kiwanda cha kokoto, kiwanda cha Marumaru na kiwanda cha matofari na vigae vya Dodoma. Shughuli zilizofanyika katika viwanda hivyo kwa kipindi cha 1985/86 ni zile za uimarishaji wa ulinzi na hifadhi ya mitambo (Protective works).

4. Ili kuliepusha taifa kutokana na gharama zaidi za utekelezaji kunakosababishwa na kuchelewa kukamilisha miradi ya ujenzi na vile vile ili kulipatia taifa manufaa (benefits) ya miradi hiyo kwa wakati uliopangwa, katika kipindi cha 1986/87, umuhimu wa kwanza umelekezwa kwenye miradi iliyochukua muda mrefu bila kukamilika na hasa yenye mikataba na wakandara-si kama vile barabara za Lusahunga-Bukombe na Nyangunge-Musoma na mradi wa huduma za misingi unaohusu ujenzi wa mifereji ya maji machafu, ya maji ya mvua na utandazaji wa mabomba ya maji safi huko Dodoma. Umuhimu pia umewekwa kwenye miradi inayoendelea na ambayo kukamilika kwake kutakuwa na msukumo mkubwa katika sekta za uzalishaji za viwanda na kilimo kama vile wa barabara ya kwenda kiwanda cha karatasi Mufindi, barabara za pareto na ya Mombo-Lushoto. Miradi ambayo ina wafadhili nayo pia imepewa umuhimu unaostahili ili kufanikisha utekelezaji wake.

### B. Barabara:

Katika kipindi cha 1986/87 jitihada zitaendelezwa za kujenga barabara mpya na kufanya matengenezo hasa ya barabara ambazo zimeharibika mno. Katika kipindi cha 1986/87, barabara ya Makambako-Songea yenye urefu wa Km. 313 ilikamilika kujengwa. Shughuli za usanifu, ujenzi upya, uimarishaji na matengenezo ya barabara zimetengwa jumla ya Sh. 325.1 milioni.

#### 6. Ujenzi wa Barabara Mpya:

Ujenzi mpya utakaoendelea katika kipindi hiki ni pamoja na barabara za Nyangunge—Musoma, Mombo-Lushoto, Lusahunga Bukombe, Kibiti—Lindi, Mufindi Access Road na Arusha—Minjingu.

7. Nyangunge-Musoma: Ujenzi wa barabara hii yenye urefu wa km. 184 ulitegemewa kukamilika katika kipindi cha 1986/87 lakini utekelezaji wa mradi siyo mzuri na mategemeo ya sasa ni kuwa utakamilika 1987/88. Sh. 28.0 milioni zimetengwa katika kipindi cha 1986/87 ili kuendelea na ujenzi. Madhumuni ya barabara hii ni kupunguza matatizo ya usafiri hasa kwa mkoa wa Mara. Lengo ni kuendelea, hapo baadaye, na ujenzi wa barabara kutoka Musoma hadi Sirari (Mpakani na Kenya) ili pia kuwezesha kutumia kikamilifu daraja la Kirumi ambalo sasa limeanza kutumika.

8. Mombo—Lushoto: Ujenzi wa barabara hii yenye urefu wa Km. 41 unategemewa kukamilika 1986/87 na Sh. 10.5 milioni zimetengwa. Madhumuni ya kujenga barabara ya lami ni kurahisisha uchukuzi wa mazao (hasa matunda) kutoka kwenye eneo la Lushoto.

9. Lusahunga—Bukombe: Hii ni sehemu ya barabara ya Kobero-Rusumo-Lusahunga/Bukombe-Isaka yenye madhumuni ya kurahisisha uchukuzi wa bidhaa za nchi jirani za Burundi na Rwanda. Ujenzi wa sehemu ya Lusahunga-Bukombe, ulioanza 1984/85, utaendelea katika kipindi hiki kwa Sh. 47.0 milioni zilizotengwa. Jitihada zitaendelea kufanya ili kupata mfadhili kwa ujenzi wa sehemu ya Bukombe-Isaka.

10. Kibiti-Lindi: Ujenzi wa sehemu ya Nangurukuru-Kilwa Masoko unaendelea kutekelezwa na MECCO. Ujenzi wa barabara hii, kwa kutumia "Direct Labour Construction Unit" iliyo chini ya Wizara ya Mawasiliano na Ujenzi, utaendelea. Kiasi cha Sh. 55.0 milioni kimetengwa kwa 1986/78.

11. Mufindi Access Road: Barabara hii yenye urefu wa Km. 47 ina madhumuni ya kusafirisha magogo kwenda kwenye kiwanda cha karatasi, Mufindi. Sh. 38.4 milioni zimetengwa ili kuendelea na ujenzi.

## Matengenezo ya Barabara:

12. Miradi ya matengenezo (maintenance) na uimarishaji (rehabilitation) itazihusu barabara za Dar es Salaam—Tunduma Chalinze—Segera, barabara za pareto, na awamu ya I, II na ya III ya mradi wa kuimarisha barabara kuu (TRM). Taarifa za usanifu wa barabara ya Dar es Salaam—Tunduma zimeonyesha kuwa km. 418 zinahitaji matengenezo na kati ya hizo, km. 295 zitashughulikiwa chini ya TRM III na ni km. 123 tu zilizobaki ndizo zitakazohusika katika mradi huu wa matengenezo ya barabara ya Dar es Salaam—Tunduma. Matengenezo ya barabara ya Chalinze—Segera—Mkumbara yataendelezwa katika kipindi hiki. Lengo ni kuifanya iendelee kupitika wakati mfidhili anatafutwa wa kuwezesha ujenzi mpya. Matengenezo hayo yatahusu utandazaji upya wa changarawe kati ya Manga—Segera (km.20) Mombo—Masinde (km.15) na uimarishaji wa Segera—Korogwe Chekelei (km. 10) na Kitumbi—Mkata. TRM I na II zitahusu ukamilishaji na uendelezaji wa ujenzi wa kambi, ununuzi na usambazaji wa lami, vipuri, mipira na betri. TRM III itahusu ufufuzi wa mitambo ya magari ya TRM, uimarishaji wa km. 295 za barabara ya Dar es Salaam—Tunduma, uimarishaji wa km. 700—1000 za barabara za changarawe na huduma za wataalam. Katika kipindi hiki Sh. 114.9 milioni zimetengwa kwa utekelezaji wa shughuli zinazohusu matengenezo na uimarishaji wa barabara.

## Usanifu wa Barabara:

13. Katika kipindi cha 1986/87, usanifu utakamilishwa kwa barabara ya Songwe—Uyole kwa madhumuni ya kuimarisha barabara ili ihudumie vizuri uchukuzi wa bidhaa zindazo na zitokazo Malawi. Pia uchunguzi wa kiu chumi utafanywa kwa barabara ya Bukombe—Isaka ili kuwezesha kutafuta mfidhili kwa ajili ya ujenzi wa barabara.

## C.—VIWANJA VYA NDEGE

14. Umuhimu wa kuimarisha viwanja vya ndege utaendelea kuwepo katika kipindi hiki na Sh. 39,4 milioni zimetengwa. Uimarishaji wa "runways" kwa viwanja vya Mafia na Kilwa utakamilika ili kuwezesha ndege za Fokker kutua. Kiasi cha Sh. 4.5 milioni kwa kiwanja cha Mafia na Sh. 1.0 milioni kwa kiwanja cha Kilwa zimetengwa. Ujenzi wa kiwanja cha Mwanza utaendelea na Sh. 20.0 milioni zimetengwa, na katika kipindi hiki uimarishaji wa "runway" unategemea kukamilika ili kuwezesha ndege za Boeing kuanza tena kutumia kiwanja hicho. Shughuli mbali mbali zitaendelea katika viwanja vya Kigoma, Tabora Dodoma, Dar es Salaam na Mtwara.

## D.—UFUNDI NA MAJENGO

15. Ujenzi wa karakana ya Kanda ya Mtwara unategemea kukamilika katika kipindi hiki na Sh. 4.0 milioni zimetengwa. Kwa upande wa vivuko Sh. 9.0 milioni zimetengwa kwa shughuli za ununuzi wa kivuko cha Magogoni na matengenezo ya vivuko, hasa MV. Ukombozi (Magogoni). Hata hivyo ununuzi wa kivuko kipya utategemea upatikanaji wa fedha za kigeni.

16. Shughuli za majengo zitahusu ukamilishaji wa nyumba za wafanyakazi zilizopo Dar na kuanza awamu ya pili ya nyumba za watumishi. Jumla ya Sh. 6.6 milioni zimetengwa.

## E.—USTAWISHAJI MAKAO MAKUU

17. Mradi huu ulipobuniwa ulikadiriwa kuwa ungehitaji jumla ya Sh. 3,700 milioni kukamilisha katika kipindi cha miaka kumi, yaani, wastani wa Sh. 370.0 milioni kwa mwaka, zikiwamo fedha za hapa na za kigeni kutoka bajeti ya Serikali na vyanzo vingine. Kwa kuzingatia hayo, na hali ngumu ya uchumi inayolikabili Taifa, katika kipindi cha 1986/87 utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Makao Makuu umetengewa jumla ya Sh. 382.2 milioni zikiwamo Sh. 224.9 milioni kutoka bajeti ya Serikali na Sh. 158.0 milioni kutoka vyanzo vingine.

18. Miongoni mwa miradi iliyopewa umuhimu mkubwa ni ile inayoendelea na hasa inayotazamiwa kukamilika katika kipindi hiki cha fedha, ikiwamo ile yenye dhamira ya kuharakisha ubamiaji kwenye makao makuu kama vile ujenzi wa maofisi ya serikali na nyumba za kuishi wafanyakazi, pamoja na miradi itakayowahakikishia wakazi waliopo na wahamiaji wa Dodoma, huduma muhimu za elimu, afya, barabara na maji safi. Miradi mingine ni ile ya mifereji ya maji machafu na ya mvua na ile yenye kuupa mji mkuu sura ya kuvutia kama vile ya ustawishaji miche, upandaji miti na ile ya uimarishaji na hifadhi ya ardhi.

19. Awamu ya I na ya II za mradi wa huduma za msingi (Major Trunk Services) zinazohusu utandazaji wa bomba kuu za maji safi na ujenzi wa mifereji ya maji machafu na ya mvua, zimetengewa jumla ya Sh. 47.2 milioni ili ziendelee. Pia mradi wa huduma za barabara na maji safi kwa eneo la Nkuhungu East utaendelezwa na umetengewa Sh. 13.6 milioni.

20. Miradi ya viwanda itakayotekelezwa katika kipindi hiki ni ile ya kiwanda cha kokoto ambacho kitaunganishiwa umeme wa kutoka Kidatu ambao waya zake zimepita karibu na kiwanda hicho. Sh. 1.0 milioni zimetengwa kwa ajili hiyo. Pia Sh. 18.1 milioni zimetengwa kwa ajili ya sehemu ya ujenzi wa karakana, jengo la utawala na jengo la uzalishaji kwenye mradi wa Kituo cha kuhifadhi na kuzalisha vifaa vya ujenzi (Building Materials Production Centre).

21. Wakati ambapo katika kipindi cha 1986/87 ujenzi wa ofisi utahusu kuanza ujenzi wa majengo mawili ya serikali na kuendeleza ujenzi wa Mji Mlezi House, ujenzi wa nyumba za kuishi kwa upande mwingine utahusu kuendeleza hadi kukamilisha nyumba 123 zinazojengwa na Shirika la Bima la Taifa (NIC), kukamilisha nyumba 29 za gharama ndogo na kuanza hadi kukamilisha nyumba 4 za mawaziri. Jumla ya Sh. 55.4 milioni zimetengwa kwa shughuli hizo katika kipindi hiki cha fedha.

22. Ili kukidhi mahitaji ya huduma za elimu na afya yatakayotokana na ongezeko la wakazi wa Dodoma, ujenzi wa shule ya msingi ya Kikuyu utakamilishwa kwa Sh. 1.1 milioni; ujenzi wa shule ya msingi ya Mbwanga utaanza na kuendelezwa kwa Sh. 6.2 milioni na pia upanuzi wa hospitali ya Dodoma utakaoendelezwa kwa Sh. 5.0 milioni, utahusu upanuzi wa huduma za umeme na maji, ujenzi wa uzio, premature ward, vyumba vya watu mashuhuri (VIP), maternity operation theatre na ukamilishaji wa wadi ya wazazi.

23. Huduma za manispaa zitahusu miradi ya matengenezo ya barabara, na kuendeleza ujenzi wa soko la Majengo ambao umekuwa ukiendelea kwa kasi ya kuridhisha na jumla ya Sh. 26.0 milioni zimetengwa kwa mradi wa soko hilo na Sh. 5.0 milioni kwa ajili ya mradi wa matengenezo ya barabara.

24. Miradi ya kuupa sura nzuri mji wa Dodoma ni ule wa hifadhi ya ardhi (Landscape consolidation programme) ambao umetengewa Sh. 2.5 milioni na ule wa upandaji miti ambao nao umetengewa Sh. 4.5 milioni. Mradi wa miche ulioko barabara ya Arusha nao pia utaendelezwa na Sh. 2.5 milioni zimetengwa kwa ajili hiyo.

25. Miradi ya usanifu wa kihandisi, usanifu wa ujenzi, mapitio ya mara kwa mara ya mpango kabambe wa mji na upimaji viwanja itaendelezwa katika kipindi hiki na Sh. 41.6 milioni zimetengwa.

## 9.—NISHATI

1. Nishati ni muhimu kwa taifa katika kuendeleza huduma za kiuchumi na za kijamii. Vyanzo vya nishati hapa Tanzania ni kuni na mkaa, mafuta (crudeoil) gesi, maporomoko ya maji, mkaa wa mawe, mionzi ya jua, mabaki ya jua, mabaki ya mimea (biomass), samadi (biogas) na upepo. Sera ya nishati inatilia mkazo utumiaji na uendelezaji wa vyanzo vya asili na hasa nguvu za maji, gesi, mkaa wa mawe na upepo ili kupunguza matumizi ya mafuta ambayo yanaagizwa kutoka nchi za nje kwa kutumia fedha za kigeni. Hatua nyingine za kupunguza matumizi ya petroli ni kuweka viwango maalum vya matumizi yake.

Katika mpango wa maendeleo wa mwaka 1986/87 miradi itakayotekelezwa inalenga katika kutekeleza sera ya nishati. Miradi hiyo imetengewa jumla ya shilingi milioni 527,244. Kati ya fedha hizo shilingi 105.1 milioni fedha za hapa na shilingi 326,242 milioni ni fedha za nje zimetengwa kutoka bajeti ya serikali na shilingi milioni 95,902 ni mchango ya mashirika yanayoshughulikia nishati hapa nchini.

## 2. Umeme:

Mchango wa umeme katika pato la taifa umeanza kuonyesha matumaini mema. Mchango huo unajidhihirisha wazi katika takwimu za mafuta yanayotumika kwa ajili ya kutengeneza umeme, ambazo zinaonyesha kwamba kiasi cha mafuta kina- chotumika kwa ajili hiyo kinaanza kushuka hasa baada ya miji ya Iringa, Mbeya na Dodoma kuunganishwa kwenye gridi ya taifa.

Katika mpango wa maendeleo wa mwaka 1986/87 shirika la umeme la taifa TANESCO, litatumia jumla ya shilingi milioni 369,42 kwa kuendeleza miradi yake. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 105.1 fedha za hapa na shilingi milioni 264,642 fedha za nje zitataka kwenye bajeti ya serikali, na mchango wa shirika ni shilingi milioni 90,23 Mkazo mkubwa utakuwa ni kuendeleza gridi ya taifa kuendeleza ujenzi wa mradi mkubwa wa Mtera, na kufanya marekebisha ya jumla (rehabilitation) kwa miradi ya zamani na Ujenzi wa "Grid Control Centre".

## 3. Mtera Power Plant:

Ujenzi wa mradi huu umaendelea. Kazi ambazo zitafanywa mwaka huu ni pamoja na uchimbaji wa "headrace tunnel" "cable shaft", na "tailrace tunnel". Kazi nyingine ni: concreting of machinery hall, entrance building and concreting of penstock 1 and 2. Mradi umetengewa jumla ya shilingi milioni 217,327 kati ya hizo shilingi milioni 27,5 ni fedha zao shilingi milioni 151,327 ni fedha za nje na shilingi milioni 38,5 zitataka kwenye bajeti ya serikali.

## Uendelezaji wa gridi ya taifa:

### 4. Singida Mwanza 220 T.L.:

Baada ya kukamilika kwa uunganishaji wa miji wa Singida katika gridi ya taifa hapo 1985/86 imefanya idadi ya miji iliyo- kwishaunganishwa kwenye gridi kufikia 9 yaani DSM, Iringa, Mbeya, Morogoro, Arusha, Moshi, Dodoma, Singida na Zanzibar. Katika mpango wa 1986/87 mkazo utawekwa katika uunganishaji nyaya za umeme kati ya Singida/Tabora 132 K.V.T.L. Shinyanga/Tabora 132 K.V.T.L. na Mwanza/Musoma 132 K.V.T.L. Miradi hii imetengewa jumla ya shilingi milioni 92,1 kati ya hizo shilingi milioni 44,0 zitataka bajeti ya serikali shilingi milioni 38,1 ni mchango wa TANESCO.

5. Mradi wa Uwemba/Mbinga utaendelea kutekelezwa katika kipindi cha 1986/87. Mradi huo umetengewa shilingi milioni 3,9 za hapa. Kati ya hizo shilingi milioni 1,5 zitataka kwenye bajeti ya serikali na shilingi milioni 2,4 ni mchango wa Shirika

6. Mradi wa Masaka/Bukoba 132 K.V.T.L. wenye lengo la kuupatia mkoa wa Kagera umeme kutoka Uganda unategemewa kuanza kutekelezwa katika kipindi cha 1986/87 wakati wafadhili watakuwa wameshaweka ahadi ya kuufadhili mradi huo. Mradi umetengewa shilingi milioni 1,8 kwa ajili ya kufanya matayarisho ya mwanzo. Kati ya fedha hizo shilingi laki moja zitataka kwenye bajeti ya serikali na shilingi milioni 1,7 ni mchango wa Shirika.

7. Pamoja na miradi hiyo ya maendeleo shirika litatekeleza mradi wa kurekebisha mitambo nyaya za kusambaza na kugawa (transmission and distribution lines) umeme. Mradi umetengewa jumla ya shilingi milioni 97,415. Kati ya hizo shilingi milioni 20,0 zimetengewa kutoka bajeti ya serikali, shilingi milioni 14,73 kutoka mfuko wa Shirika na shilingi milioni 62,685 ni fedha za nje.

8. Mradi wa kuwianisha shughuli za umeme katika gridi ya taifa kwa jina "Grid control centre" ni mradi mpya utakaanza kutekelezwa 1986/87. Mradi huo umetengewa jumla ya shilingi milioni 6,8. Kati ya hizo shilingi milioni 1,0 zimetengwa toka bajeti ya serikali na shilingi milioni 5,8 ni mchango wa Shirika.

## 9. T.P.D.C.

Pamoja na shughuli zake za kutafuta mafuta na gesi ambazo zitaendelea kufanywa kipindi cha 1986/87 Shirika la maendeleo ya petroli hapa nchini (TPDC) litatekeleza miradi mitatu ya maendeleo.

10. Mradi wa Tanzania/Norwegian petroleum utaendelea kutoa mafunzo kwa Watanzania katika fani za utafiti wa mafuta na gesi, geolojia na geophysics. Pamoja na shughuli hiyo ya kufundishia wanafunzi, NORAD ikishirikiana na TPDC watafanya utafiti wa mafuta na gesi katika sehemu za bonde la Kilosa Ruvu, Nyasa ya Kaskazini na Tukuyu, Shirika limetenga shilingi milion 2,0 toka mfuko wake na shilingi milioni 30,6 ni fedha za nje.

## 11. Oil Storage tank:

Ujenzi wa tangi kubwa la kuhifadhi mafuta utaendelezwa katika kipindi cha 1986/87 kwa gharama ya shilingi milioni 5,0 kutoka Serikali ya Italia.

## 12. Songo Songo Rehabilitation:

Katika kipindi cha 1986/87 marekebisha ya visima vya gesi ya Songo Songo yataendelezwa. Jumla ya shilingi milioni 28,672 zimefungwa. Kati ya hizo shilingi milioni 3,672 zitataka kwenye mfuko wa shirika na shilingi milioni 26,0 ni za nje Mamlaka ya uendeshaji bonde la mto Rufiji litatekeleza miradi miwili ya maendeleo ya nishati.

## 13. Rubada:

14. Mradi wa kupima wingi wa maji katika bonde la Mto Rufiji kwa ajili ya kutumia takwimu hizo katika miradi ya umeme utaendelea kutekelezwa. Mkazo wa mradi huu utawekwa kwenye kurekebisha vyombo vya kupima wingi wa maji. Mradi umetengewa shilingi laki 5,0 fedha za hapa.

## 15. Mradi wa Kihandisi:

Benki ya dunia ilishauri kwamba mradi huu ndio mradi pekee wa gharama nafuu ambao utaongezea umeme wa maporomoko ya maji baada ya mradi wa Mtera. Kwa vile miradi ya aina hii huchukua miaka mingi kabla ya ujenzi kukamilika inabidi utafiti na gharama za mradi (feasibility study) zifanyike mapema iwezekanavyo. Mradi huu ambao ni mpya umetengewa shilingi laki 1, wakati mfadhili anatafutwa.

## 10.—USAFIRISHAJI NA MAWASILIANO

### Utangulizi:

1. Sekta ya usafirishaji na mawasiliano ambayo ni muhimu katika kufanikisha shughuli za sekta nyingine na hasa kilimo, viwanda, madini n.k. katika uchukuzi wa mazao na bidhaa, iliendelea kukabiliwa na matatizo mbali mbali na hivyo kutoa huduma ambazo haziridhishi. Matatizo makubwa yaliyokuwemo ni ya upungufu wa Vifaa na vyombo mbali mbali, ubovu wa njia za uchukuzi na uhaba wa mafuta. Uwezo wa uchukuzi kwa njia ya barabara umebakia kuwa mdogo kutokana na barabara nyingi

kutofanyiwa matengenezo yanayotakiwa kwa sababu ya ukosefu wa lami na ubovu wa "graders" na "dozers". Pia uhaba wa mafuta (petroli na diselii, uliathiri sana shughuli za uchukuzi hasa usombaji wa mazao. Uchukuzi wa njia ya reli nao ulikabiliwa na matatizo ya ukosefu wa fedha za kigeni za kuagizia vipuri vya vichwa vya treni na mabehewa ya mizigo na abiria, uchakavu wa reli na kutokuwepo na mawasiliano kabisa au mawasiliano (telecommunications) ya kuaminika. Matatizo haya yamesabisha wastani wa upatikanaji (availability) wa injini (locomotives) na mabehewa (abiria na mizigo) kuwa asilimia 50. Huduma nyingine kama za mawasiliano, hali ya hewa na usafiri wa anga zimeendelea kuathiriwa kutokana na uchakavu wa vifaa na mitambo. Tatizo kubwa ni la ukosefu wa fedha za kigeni ili kununulia kutoka nje ya nchi vifaa vya kuimarisha njia na vyombo vya uchukuzi na mawasiliano.

2. Kutokana na matatizo mbali mbali huduma za uchukuzi hazikuwa nzuri kwa kipindi cha 1985/86. Uchukuzi wa mazao unaendelea kukwama katika sehemu mbali mbali na kusababisha hasara kutokana na uharibifu wa mazao na pia upungufu wa vyakula katika maeneo ambayo hayajitegemei kwa chakula. Jitihada mbali mbali ziliendelea kufanyika ili kupunguza matatizo haya ya uchukuzi ambayo ni pamoja na magari matara (petroli na diselii), ununuzi wa magari na spea kwa ajili ya matengenezo ya "locomotives".

#### A. USAFIRI WA BARABARA:

3. Katika kipindi cha 1986/87 jitihada zitaendelea za kuimarisha huduma za uchukuzi wa mazao, bidhaa na abiria. Kampuni za uchukuzi za Mkoa (RETCOs) ya Dodoma (KAUDO), Mwanza (KAUMA), Tabora (KAUTA), Mtwara (KAUMU) na Ruvuma (KAURU) zitaendelea kuimarishwa kwa ununuzi wa magari mapya, ujenzi wa karakana na ununuzi wa spea. Ingawa makampuni yalikabiliwa na matatizo ya upatikanaji wa mafuta, matairi na spea katika kipindi cha 1985/86, lakini kwa ujumla yataendesha shughuli kwa faida na hivyo utekelezaji wa miradi kwa kipindi cha 1986/87 utatokana na Sh. 38.0 milioni ambazo ni fedha zao na Sh. 32.8 milioni mkopo kutoka mabanki. Kampuni ya Uchukuzi ya Mkoa wa Kagera itaendelea kuimarishwa kwa ununuzi wa magari mapya yatakayogharimu Sh. 18.0 milioni. Hata hivyo Kampuni hii itabidi iongezewe mtaji ili iweze kujimarisha zaidi kwa ujenzi wa karakana. Ingawa katika kipindi cha 1985/86 Shirika la Uchukuzi la Taifa (NTC) litaendelea na jitihada za kuanzisha Second Trucking Project kwa madhumuni pia ya unuzishaji wa kampuni mpya za uchukuzi za mikoa lakini kutokana na matatizo mbali mbali yanayokabili kampuni zilizo inakuwa vigumu kuanzisha nyingine mpya.

4. Kutokana na utekelezaji mzuri wa mradi wa ufufuaji Magari (vehicle repair project), ambao uliwezesha kufufua magari 574 na kujenga bodi 900 za magari ambayo matokeo yake ni kuongeza uwezo wa uchukuzi kwa tani 8,736, Shirika la Uchukuzi la Taifa linategemea kuanza utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi na kukamilisha mwaka 1991. Awamu hii itahusu matengenezo makubwa ya magari 900 na utengenezaji upya (reconditioning) ya mabodi ya magari 1,900.

5. Huduma za uchukuzi zitolewazo na Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) zimeendelea kuathiriwa na uchache wa mabasi Jitihada za kununua mabasi mapya zitaendelea kwa kukamilisha kujenga bodi kwa mabasi 40 ambayo 18 kati yao yamekamiliwa katika kipindi cha 1985/86. Shirika linategemea kutumia Sh. 71.0 milioni kutokana na faida za Shirika pamoja na mikopo kwa shughuli za ununuzi wa mabasi ununuzi wa Vifaa vya karakana, ujenzi wa nyumba za wafanyakazi na ununuzi wa spea.

6. Huduma kutokana na Kampuni ya Mabasi ya Taifa (KAMATA) hazikuridhisha kutokana na uchakavu wa mabasi pamoja na uhaba wa spea, mafuta, mipira na matairi.

#### B. USAFIRI WA RELI:

7. Uchukuzi wa njia ya reli ni wa kutegemewa sana hasa kwa usafirishaji wa mbali. Hivyo ni muhimu kuwa na huduma nzuri ili kuweza kusafirisha mazao na bidhaa bila matatizo. Huduma hizi ambazo pia hutegemewa sana na nchi za jirani zinaendelea kuathiriwa kutokana na matatizo mbali mbali hasa ya uchakavu wa njia za reli na madaraja, uhaba wa spea za kufanyia matengenezo na pia uwezo mdogo wa uchukuzi kutokana na upungufu wa injini na mabehewa.

8. Katika kipindi cha 1985/86 Shirika la Reli (TRC) liliendelea na jitihada za kuimarisha huduma za uchukuzi kwa kutekeleza miradi ya upasuaji kokoto na utengenezaji wa madaraja mabovu ili kuimarisha njia ya reli. Hata hivyo shughuli hizi za kuimarisha njia ya reli zimeendelea kukwama kwa kukosa mataruma ambayo yanahitajika ili kutandika reli mpya yenye uzito mkubwa kwenye reli ya kati na ili kuwezesha treni za uzito mkubwa kupita bila matatizo na kupunguza kwa kiasi kikubwa matukio ya ajali. Uwezo wa uchukuzi uliathiriwa sana kutokana na ukosefu wa fedha za kigeni ili kuagiza spea za locomotives. Jitihada za kutafuta misaada ya fedha nje hazikufanikiwa na hivyo kusababisha ukosefu wa spea hasa kwa locomotives zilizonunulia kutoka Uingereza na India. Huduma za mawasiliano pia ni hafifu na jitihada za kuimarisha ziliendelea kwa kutekeleza miradi ya mawasiliano (telecommunications) na njia za ishara (signals).

9. Katika kipindi cha 1986/87 Shirika litaendelea na utekelezaji wa miradi yenye lengo la kuimarisha huduma za uchukuzi wa mazao, bidhaa na abiria ili kupunguza matatizo ya uchukuzi hapa nchini na nchi za jirani. Hata hivyo jitihada za Shirika zitaendelea kuathiriwa kutokana na ukosefu wa fedha za kigeni ili kutekeleza miradi muhimu hasa ya uimarishaji wa njia ya reli, ununuzi wa mabehewa na injini na pia ununuzi wa spea za locomotives. Ili kuweza kuimarisha njia ya reli, Shirika linategemea kutumia Sh. 26.2 milioni kwa mradi wa upasuaji kokoto sehemu za pangani na Tora. Shirika pia litaendelea na jitihada ili kuwezesha kutekeleza mradi wa "steel sleeper reconditioning plant" wenye madhumuni ya kutengeneza mataruma ambayo yameharibika lakini yanaweza kutengenezwa na kutumika hasa kwenye "link lines" na pia kwenye ujenzi wa reli Manyoni-Singida na Sh. 15.0 milioni zinategemea kutumika. Kwa vile jitihada za ununuzi wa mataruma zimekwama, Shirika litafanya utafiti ili kuona uwezekano wa kutengeneza mataruma ya saruji (concrete sleepers) kwenye karakana ya Mang'ula. Mradi wa uimarishaji wa njia ya reli unaohusu uimarishaji madaraja unatarajiwa kukamilika katika kipindi cha 1986/87 na Sh. 15.0 milioni zimetengwa.

10. Ili kuongeza uwezo wa uchukuzi Shirika litaendelea na miradi ya ununuzi wa spea za kufanyia matengenezo ya magari moshi, kwa kiasi cha Sh. 20.0 milioni. Pia Shirika litajitahidi kutafuta misaada ya fedha ili kuwezesha ununuzi wa mabehewa ya aina mbali mbali.

11. Ili kuongeza ufanisi, njia za mawasiliano (telecommunications) na ishara (signals) zitaendelea kuimarishwa. Mawasiliano yaliyopo kati ya vituo vya reli vya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na Moshi ni ya kizamani na yamechakaa. Hivyo Shirika litaendelea na juhudi za kuimarisha mawasiliano kati ya vituo vikubwa ili kuongeza ufanisi wa kuendesha magari moshi. Pia mawasiliano yataimarishwa kati ya Tabora na Kigoma na kiasi cha Sh. 7.2 milioni kimetengwa 1986/87. Kazi ya kuweka vifaa vipya vya mawasiliano ya ishara (signals) kati ya vituo vya Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma na Tabora (signalling Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Tabora) iliyoanza mnamo 1983/84 inaendelea na kwa kipindi cha 1986/87 Sh. 28.2 milioni kwa shughuli za ununuzi na usmikaji vifaa katika vituo vya reli.

12. Uchukuzi wa bidhaa za nchi za jirani Unawekewa umuhimu katika jitihada za kuimarisha huduma za uchukuzi wa reli. Hata hivyo huduma hizi lazima ziende sambamba na huduma nzuri katika maziwa ya Tanganyika na Victoria. Jitihada zinazofanywa na Shirika ni pamoja na uimarishaji wa bandari ya Kigoma kwa kuipanua na kununua Vifaa, na kwa kipindi hiki Sh. 10.2 milioni zimetengwa. Pia katika kipindi cha 1986/87 Shirika litaendelea na uimarishaji wa uchukuzi katika Ziwa Victoria kwa Ujenzi wa karakana inayoeleza ya matengenezo ya meli (floating dry dock) na ununuzi wa meli ya abiria (MV. Serengeti), na kiasi cha Shs. 10.8 milioni kimetengwa.

13. Ujenzi wa reli ya Manyoni-Singida Utaendelea katika kipindi hiki na Shs. 30.0 milioni zimetengwa. Utekelezaji wa mradi huenda ukaathiriwa na ukosefu wa vifaa mbali mbali na kama fedha za kigeni za kutosha hazitapatikana.

14. Shirika linategemea kutumia jumla ya Shs. 158.1 milioni katika kipindi cha 1986/87 kwa utekelezaji wa miradi mbali mbali.

### C. USAFIRI WA BAHARINI

15. Mamlaka ya Bandari imeendelea kuimarisha huduma katika bandari zote zilizopo mwambao wa bahari ya Hindi. Mamlaka inatekeleza mpango wa kurekebisha bandari ya Dar es Salaam na kuifanya ya kisasa kwa madhumuni ya kuongeza ufanisi wa kazi hasa kufuatana na hali ya sasa hivyo ya matumizi zaidi ya makasha.

16. Katika kipindi cha 1986/87 miradi itakayoendelea kutekelezwa ni pamoja na:—

(a) **Conversion of Berths 9-11**—Mradi huu una madhumuni ya kujenga gati la makasha (container terminal) ili kuongeza ufanisi wa kazi bandarini hasa kutokana na kuongezeka utumiaji wa makasha. Mradi huu ulioanza kutekelezwa Desemba 1984 unaendelea kutekelezwa vizuri na kiasi cha Shs. 20.7 milioni kimetengwa kwa mwaka 1986/87. Mradi huu ni sambamba na mradi wa Ujenzi wa bohari la mizigo lendayo Zambia (import cargo warehouse) kwa kutumia vifaa vitakavyotokana na kubomolewa kwa shedi lililopo gati Na. 10/11. Ujenzi wa bohari utaendelea kwa kiasi cha Sh. 11.7 milioni. Pia mradi huu wa container terminal unahusisha ujenzi wa "Inland Container Depot-Ubungo" ili kupakua na kupakia (stripping and stuffing) mizigo. Shohona inayokadiriwa kupitia katika kituo (depot) hicho ni tani 201,600 katika mwaka 1987 na tani 286,100 katika mwaka 1992. Kiasi cha Shs. 5.9 milioni kimetengwa kwa 1986/87.

(b) **Grain Terminal**—Mradi huu unahusu ujenzi wa ghala la nafaka lenye uwezo wa kuhifadhi tani 30,000 za nafaka na pia kuwezesha upakiaji wa haraka zaidi (tani 3,000 kwa siku) hivyo kuziwezesha meli kupunguza muda wa kukaa bandarini. Mradi huu ulioanza kutekelezwa 1985/86 unaendelea vizuri na kwa kipindi cha 1986/87 Shs. 42.5 milioni zimetengwa ili kuendelea na ujenzi.

(c) **Rehabilitation of Kurasini Oil Jetty**—Mradi huu unahusu matengenezo/marekebisho ya jeti lililopo, badala ya kujenga jingine jipya, ili iweze kupokea meli za mafuta zenye uwezo wa tani 25,000 zilizojaa (fully loaded) au tani 35,000 zisizojaa (partly loaded). Mradi ulianza kutekelezwa 1984/85 na Shs. 5.0 milioni zimetengwa katika kipindi cha 1986/87 ili kuendelea na shughuli za ujenzi.

(d) **Uimarishaji wa Bandari ndogo**—Mradi huu una lengo la kuimarisha bandari za kilwa, Lindi na Mafia ambazo ziko katika hali mbaya sana kiasi cha kuhatarisha usalama wa abiria na mizigo, pamoja na vyombo vinavyotua kwenye bandari. Mradi ulianza kutekelezwa 1984/85 na kwa kipindi hiki Sh. 13.5 milioni zimetengwa ili kuendelea na shughuli za uimarishaji.

(e) **Container Handling Equipments**—Lengo la mradi ni kupata zana mpya za kupakua na kupakia makasha (Containers) katika "Container terminal" na "Ubungo Container Depot". Katika kipindi cha 1986/87 Sh. 9.0 milioni zimetengwa ili kuendelea na ununuzi na usafirishaji wa zana.

(f) **Dar es Salaam Port Rehabilitation**—Mradi huu una lengo la kuipatia Bandari ya DSM pamoja na zingine zana mpya za kupakua mizigo. Sehemu kubwa ya zana zinazotumika sasa zimechakaa sana, Mradi huu ulianza kutekelezwa 1983/84 na unategemwa kuhamilika mwaka 1986/87 na kiasi cha Shs. 67.6 milioni kimetengwa.

### D. HUDUMA ZA POSTA NA SIMU

17. Shirika la Posta na Simu lina lengo la kueneza huduma za posta na simu katika makao makuu ya wilaya zote nchini na hatimaye vijijini. Katika kueneza huduma za simu, lengo ni kuongeza idadi ya watejea kwa asilimia 12.5 kila mwaka, lakini kwa miaka mingi sasa lengo hili halijafikiwa. Tatizo kubwa limekuwa ni uwezo mdogo kifedha na kiutaalam katika kuwezesha kutekeleza mipango ya shirika kwa ukamilifu.

18. Ili kukabiliana na matatizo ya fedha za hapa, Shirika litajihusisha na matengenezo ya njia mbovu za simu na kuimarisha ukusanyaji wa mapato kwa kupunguza malimbikizo ya madeni ya simu. Jitihada hizi zimekuwa na mafanikio yasiyoridhisha kutokana na mitambo mingi kuwa ya zamani na iliyochakaa kutokana na ukosefu wa spea. Shirika litaendelea na jitihada za kutafuta msaada kutoka nje ya nchi ili kuwezesha kupata vifaa vya kujengea na mitambo na hivyo kurahisisha utekelezaji wa miradi. Kwa matatizo ya kiutaalam, Shirika litaendelea kuendesha mafunzo katika chuo chake na litawatafutia wafanyakazi nafasi za masomo nje ya nchi katika fani za ufundi, huduma za simu, huduma za posta n.k.

19. Ili kuimarisha huduma zitolewazo na shirika, miradi kadhaa itaendelea kutekelezwa katika kipindi cha 1986/87. Miradi hiyo ni pamoja na ya "exchanges" na "microwaves" yenye malengo ya kupanua huduma za simu. Baadhi ya miradi hiyo itakayoendelea kutekelezwa ni:—

(a) **Exchanges for Arusha, Mwanza, Tabora, Dar es Salaam Central, Shinyanga, Mbeya and Kijitonyama (19,000 lines)**:—Mradi huu unahusu uwekaji mitambo ili kuongeza njia za simu. Uwekaji wa exchanges ulikamilika 1984/85 kwa Arusha, Mwanza Mbeya na Dar es Salaam na njia 11,800 zimekwisha wekwa. Vifaa kwa vituo vya Tabora, Shinyanga na Kijitonyama vilifika tangu kipindi cha 1984/85. Ujenzi wa vituo ulikamilika katika kipindi cha 1985/86 na kwa 1986/87 Sh. 4.5 milioni zimetengwa ili kukamilisha uwekaji wa mitambo na hivyo pia kukamilisha mradi wote.

(b) **Exchanges for Bukoba, Kigoma, Musoma, Iringa, Moshi and Songea**:—Mradi huu una madhumuni ya kuweka simu za "automatic" kwa miji ya Kigoma, Bukoba, Musoma na Songea na kupunguza idadi ya watu wanaoongojea kupatiwa simu katika miji ya Iringa na Moshi na unategemea kukamilika katika kipindi cha 1986/87 kwa kiasi cha Sh. 30.0 milioni. Hata hivyo utekelezaji wa mradi unakwama kutokana na kutopatikana mfadhili ili kuwezesha ununuzi wa mitambo.

(c) **Miradi mingine ya uwekaji mitambo inayotegemewa kukamilika katika kipindi cha 1986/87 ni ya Nyololo—Njombe Songea microwave uliotengewa Sh. 2.5 milioni na Mbeya—Sumbawanga—Mpanda UHF link uliotengewa Sh. 11.2 milioni** Mradi wa "Rural and Line Carner systems" ambao una madhumuni ya kuongeza, maunganisho ya simu kati ya "Manual exchanges" zilizopo vijijini na "exchanges" katika makao makuu ya mikoa na pia miji kadhaa ya makao makuu ya wilaya, utakamilika katika kipindi hiki kwa kukamilisha uwekaji mitambo na kiasi cha Sh. 1.0 milioni kimetengwa. Pia mradi wa "cables" wenye madhumuni ya usambazaji simu vijijini ikianzia na makao makuu ya wilaya utaendelea kwa ununuzi na uwekaji wa "cables" na kiasi cha Sh. 25.0 milioni zimetengwa kwa kipindi cha 1986/87.

(d) **Shirika litaendelea na jitihada za kutafuta msaada kutoka nje hasa kwa miradi muhimu ya "Dar es Salaam modernization" ambao unahusu matengenezo ya mitambo iliyochakaa na Dar es Salaam (Earth Station Standard A) ambao unahusu ujenzi wa Kituo kipya cha kupelekea simu nje ya Tanzania, baada ya kituo kilichopo Kijitonyama (Standard B) kujaa.**

## E. UTABIRI WA HALI YA HEWA

20. Umuhimu wa ukusanyaji na utawanyaji wa taarifa mbali mbali zinazohusu hali ya hewa unazidi kujitokeza ili kufanikisha shughuli za uzalishaji mali na kiuchumi (Kilimo, usafiri, ujenzi n.k.). Kutokana na umuhimu mkubwa uliowekwa kwa sekta ya kilimo, matokeo mazuri ya uzalishaji mazao yanategemea kwa kiasi kikubwa jinsi wakulima wanavyoweza kupata taarifa za hali ya hewa. Hivyo Idara ya Hali ya Hewa itaendelea kuimarisha shughuli zake kwa ujenzi wa vituo na ununuzi wa vifaa na mitambo ili vituo hivyo viweze kutoa huduma vizuri.

21. Katika kipindi cha 1986/87, umuhimu umewekwa ili kuwezesha Idara ya Hali ya Hewa kuendelea na shughuli zake kwa hali ya kuridhisha. Ujenzi wa vituo vya "Basic Network" vitakamilishwa kujengwa Mahenge na Sumbawanga na kiasi cha Sh. 5.1 milioni zimetengwa. Pia kituo cha "Upper Air Zonal Office" kilichopo Mtwara kitakamilika kujengwa katika kipindi hiki na Sh. 2.5 milioni zimetengwa. Ujenzi wa vituo hivi unabidi uende sambamba na ununuzi wa vifaa mbali mbali. Hivyo katika kipindi hiki Sh. 3.4 milioni zimetengwa ili kukamilisha ununuzi wa vifaa vya kuchunguza hali ya anga za juu (upper air equipment) kwa ajili ya kituo cha Mbeya ambacho kinakamilika kujengwa; na Sh. 2.0 milioni kwa ununuzi wa vifaa vya mawasiliano (telecommunications equipment) kwa ajili ya vituo vilivyokamilika kujengwa vya Mbeya na Kigoma. Pia ili kuwezesha utunzaji bora wa vifaa mbali mbali, Sh. 4.0 milioni zimetengwa katika kipindi cha 1986/87 ili kukamilisha ujenzi wa bohari. Shughuli nyingine zitakazoendelea kutekelezwa ni ununuzi wa vifaa vya uchunguzi na ujenzi wa Chuo cha Hali ya Hewa huko Kigoma.

## F. USAFIRI WA ANGA

22. Huduma za mawasiliano ni muhimu katika kufanikisha shughuli za usafiri wa anga. Idara ya usafiri wa Anga (Directorate of Civil Aviation) ilikamilisha miradi muhimu katika kipindi cha 1985/86. Mradi wa kwanza wa Flight Calibration Unit unaohusu kufanya "flight testing", upimaji na urekebishaji wa vyombo vyote vya kuongozea ndege ili kufikia viwango vya masharti ya kimataifa kuhusu usafiri wa anga umekamilika kuimarishwa ili uweze kutoa huduma zinazotakiwa. Mradi wa pili ni wa "Transmitting Station" ambao umekamilika baada ya kuweka mitambo mipya ya mawasiliano.

23. Katika kipindi cha 1986/87, Idara itaendelea na shughuli za kuimarisha huduma zake kwa kuendelea na utekelezaji wa mradi wa "Radio and Navigational Aids" unaohusu ufungaji wa mitambo sehemu za Zanzibar na Mwanza na pia ujenzi wa kituo Pemba na Sh. 1.5 milioni zimetengwa. Mradi mwingine ni wa "Aeronautical Fixed Telecommunication Network" (AFTN) unaohusu ununuzi wa mitambo mipya kwa ajili ya kutekeleza mradi wa mawasiliano kati ya Dar es Salaam na nchi nyingine za jirani, na kiasi cha Sh. 1.0 milioni kimetengwa. Idara pia itaendelea na utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa nyumba za wafanyakazi na uimarishaji wa "Civil Aviation Training Centre".

## G. USAFIRI WA NDEGE

24. Shirika la Ndege (ATC) lina shabaha ya kuongeza utoaji huduma kwa kujitahidi kuhakikisha kwamba ndege chache zilizopo zinatunika kikamilifu. Hata hivyo jitihada hizi zinakwama kutokana na matatizo ya matengenezo ya ndege hasa nje ya nchi.

25. Katika kipindi cha 1986/87 Shirika litaendelea na jitihada za kutafuta msaada wa fedha za Kigeni ili kukamilisha uweleaji mitambo na kuwezesha "Kilimanjaro Maintenance Hangar" kuanza kutumika. Pia jitihada zitaendelea kufanywa za kutafti masoko ya nje ili kuwezesha kukodi ndege badala ya kununua mipya ili kuwezesha usafiri wa ndege kuwa mzuri zaidi, miradi ya uimarishaji viwanja vya ndege itaendelea katika sehemu mbali mbali, hasa kiwanja cha Mwanza ili kuwezesha tena huduma za "Boeing 737" na viwanja vya Mafia na Kilwa ili kuwezesha ndege aina ya "fokker" kutua katika viwanja hivyo. Pia mradi wa matengenezo ya taa ili kuwezesha ndege kutua usiku utakamilika katika kipindi hiki kwa viwanja vya Mwanza, Mtwara na Dodoma.

## 11.—MAJI

1. Lengo la taifa kuhusu huduma ya maji ni kumpatia kila mtanzania maji safi na ya kutosha ifikapo mwaka 1991. Utekelezaji wa lengo hili uliendelea katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 1985/86 ambapo jumla ya Shs. 138.9 milioni zilitumiwa kugharamia utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maji mijini na vijijini. Miradi mingi ilihusu uchimbaji wa mabwawa na visima virefu Vijijini na uimarishaji wa huduma za maji mijini. Hata hivyo utekelezaji wa miradi mingi—hasa isiyokuwa na wafadhili uliendelea kukabiliwa na upungufu mkubwa wa fedha za hapa na za kigeni na vifaa mbali mbali vya ujenzi. Kwa sababu hii miradi ambayo ilitegemewa kukamilika katika kipindi hicho haikukamilika.

2. Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 1986/87, Wizara ya Ardhi, Maji, Nyumba na Maendeleo Mijini itaendeleza juhudi za Taifa za kuongeza na kuimarisha huduma ya maji kwa kuendelea kutekeleza miradi yote iliyokuwa ikitekelezwa mwaka jana.

### Maji Vijijini

3. Shughuli za usambazaji maji vijijini zinahusu uchimbaji wa mabwawa, visima virefu, kuziba vijito na kujenga mabwawa na kufunza mafundi stadi wa sekta hii. Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 1986/87 shughuli kubwa zitakuwa ni pamoja na kuendeleza ujenzi wa mabwawa ya Kilimi, Bariadi na Nanga/Bulenyi na kukamilisha ujenzi wa Bwawa la Kyarano. Shughuli nyingine zitahusu ukamilishaji wa miradi ya maji ya East Kilimajaro trunk main, Mwanga, Maji Utaruni na Handeni trunk main.

4. Shughuli za uchimbaji visima zitaendelea katika mikoa ya Mara, Dodoma, Arusha, Tabora, Morogoro, Shinyanga, Lindi na Mtwara. Ujenzi wa matangi ya maji, vituo vya kuchotea maji na ulazaji mabomba utaendelea katika miradi ya maji ya Wang'ombe, Bagamoyo, Mzenga, Nyamazugwa na Bulenyi/Nanga. Shughuli za kuimarisha Karakana ya Wazo na Ujenzi wa uzio huko Kurasini pia zitaendelea. Jumla ya Sh. 299,897 milioni zitatumika kugharamia utekelezaji wa miradi 18 ya maji vijijini. Kati ya fedha hizo Sh. 62.57 milioni ni za hapa na Sh. 67.327 milioni ni kutoka nje.

### Maji Mijini

5. Miradi ya Maji Mijini itakayoendelea kutekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 1986/87 ina lengo la kuongeza kuimarisha huduma za maji katika miji mbali mbali. Miradi mingi inahusu ujenzi wa vianzo vipya vya maji na uimarishaji wa njia za kusambazaji maji.

6. Jumla ya miradi 19 itaendelea kutekelezwa katika kipindi cha mwaka huu wa fedha. Kati ya hiyo miradi 4 inatarajiwa kukamilika katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 1986/87. Miradi hiyo ni ya Maji Mbeya, Lindi, Masasi na Shinyanga.

7. Miradi mingine inahusu uimarishaji wa huduma za maji katika miji ya Mwanza, Arusha, Musoma, Mtwara, Newala, Iringa na Musoma. Miradi hii itaendelea kutekelezwa katika hatua mbali mbali za utekelezaji. Ili kutekeleza miradi ya huduma za maji mijini, Wizara inatarajia kutumia jumla ya Sh. 87,388 milioni. Kati ya fedha hizi, Sh. 54,888 milioni ni za hapa na Sh. 32.5 milioni ni za kutoka nje.

8. Miradi mingine itakayotekelezwa katika mwaka huu wa fedha ni ya kiutafiti. Miradi hiyo ni ya utafiti wa chanzo cha kupanda kwa usawa wa Ziwa Victoria pamoja na matumizi bora ya maji katika sehemu zinazozunguka maziwa hayo. Mradi mwingine ni wa utafiti wa juu ya chanzo cha mafuriko katika ziwa Nyasa. Mradi huu utahusu ujenzi wa vituo vipya vya uchunguzi. Mradi wa uchunguzi wenye lengo la kupunguza madini ya Fluoride katika maji ya kunywa unaoendeshwa katika Kijiji cha Kitefu Mkoani Arusha pia utaendelea kutekelezwa. Vile vile Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya ufundi stadi.

Jumla ya mafundi stadi 100 watafunzwa katika kipindi cha mwaka huu wa fedha. Miradi hii itagharimu jumla ya Sh. 13.4 milioni.

9. Kwa ujumla, Wizara itaendelea juhudi za Taifa za kumpatia kila mtanzania maji safi na ya kutosha. Kwa sababu ya matatizo ya uhaba wa fedha za hapa na nje, miradi itakayotekelezwa katika mwaka huu wa fedha ni ile ambayo utekelezaji wake ulianza katika vipindi vya nyuma. Hivyo mkazo mkubwa utakuwa ni kueniyeleza na kuimarisha huduma zilizopo.

## 12.—ELIMU

1. Katika Kipindi cha Mpango wa Maendeleo wa Mwaka wa fedha 1985/86, juhudi za Serikali za kutaka kuimarisha ubora wa elimu katika ngazi zote za elimu ziliendelea kuathiriwa na uhaba mkubwa wa fedha za hapa na nje unalofikabili taifa. Kwa sababu hii, ngazi zote za elimu ziliendelea kukabiliwa na upungufu wa walimu, vitabu na vifaa mbali mbali vya kufundishia. Vile vile shughuli za ujenzi wa madarasa mpya, mabweni, nyumba za walimu na upanuzi na marekebisho ya majengo ya taasisi mbali mbali katika sekta hii hazikuweza kutekelezwa kwa kiasi kikubwa.

2. Katika mwaka wa fedha wa 1986/87 mkazo mkubwa utawekwa katika uendelezaji na ukamilishaji wa miradi mbali mbali inayoendelea. Juhudi pia zitafanywa kuimarisha ubora wa elimu katika ngazi zote kwa kutoa vifaa vya kufundishia na vitabu vingi zaidi, walimu walio bora zaidi, kusimamia na kutoa ushauri wa kitaalam mikoani katika uanzishaji na ujenzi wa shule za Sekondari za kutwa. Katika kutekeleza shabaha na malengo haya, Wizara ya Elimu inatarajia kutumia jumla ya Sh. 497,969 milioni. Kati ya fedha hizo Sh. 160.5 milioni ni fedha za hapa na Sh. 336,769 ni za nje kutoka Serikali na Mashirika mbali mbali ya Kimataifa.

### Elimu ya Msingi:

3. Utekelezaji wa shughuli nyingi zinazohusu maendeleo ya elimu ya msingi sasa hivi zinafanywa na Serikali za Mita. Hata hivyo Wizara ya Elimu bado itaendelea kusimamia maendeleo na ubora wa elimu ya msingi kwa kutoa sera za jumla kuhusu elimu ya ngazi hiyo, kuwafunza walimu wengi walio bora kutoa vitabu na vifaa vya kufundishia vya kutosha na kutoa mitaala na ushauri wa kitaalam kuhusu uimarishaji elimu. Katika mwaka wa fedha wa 1986/87 Wizara inatarajia kutumia jumla ya Sh. 33.6 milioni kwa ajili ya shughuli mbali mbali zinazohusu maendeleo ya elimu ya msingi. [Kati ya fedha hizo Sh. 0.5 milioni ni za hapa na Sh. 33.1 milioni kutoka nje.

### Elimu ya watu Wazima:

4. Kwa mujibu wa takwimu za elimu ya watu wazima zilizopo asilimia 85 ya Watanzania wote sasa wanaweza kusoma na kuandika. Nia ya Wizara ni kuendelea kuimarisha wote wote wanachua kusoma na kuandika ili wasiye wakarudia tena kutolua kusoma na kuandika na vile vile kuendelea kuwafundisha watu wote ambao mpaka sasa hawajui kusoma na kuandika. Katika mwaka wa fedha wa 1986/87 Wizara itatumia jumla ya Sh. 31,769 milioni kwa ajili ya shughuli mbali mbali za elimu ya watu wazima. Kiasi cha Sh. 2 milioni ni za hapa na Sh. 29,769 ni kutoka nje.

### Elimu ya Sekondari:

5. Lengo la Serikali kuhusu elimu ya Sekondari ni kuongeza nafasi katika shule za Sekondari ili vijana wengi zaidi wanaomaliza darasa la saba waweze kupatiwa elimu hiyo. Kwa kuzingatia madhumuni ya lengo hili, Serikali inatekeleza mpango wa upanuzi na uongezaji wa nafasi katika shule za Sekondari. Mpango huu unatekelezwa katika utaratibu wa aina mbili. Kwanza ni utaratibu wa kuanzisha shule mpya za Serikali na upanuzi wa shule za zamani za Serikali kwa kuongeza mikondo na madarasa katika shule mbali mbali za Sekondari za Serikali. Chini ya utaratibu huu, shule mpya 6 (Kibondo, Kondoa, Mpanda, Mwangaza Mwasa na Kibiti) zinaendelea kujengwa na zingine zaidi ya 6 aidha zimepanuliwa ama kufanyiwa marekebisho. Utekelezaji wa miradi chini ya utaratibu huu unagharimuwa na Serikali. Utaratibu wa pili unahusu uanzishaji wa shule za sekondari za kutwa ambazo hujengwa kwa juhudi za wananchi na Serikali huwajibika kutoa walimu, vitabu na vifaa mbali mbali vya kufundishia.

6. Katika mwaka wa fedha wa 1986/85, shughuli za ujenzi wa shule mpya upanuzi na uongezaji mikondo ziliendelea katika zaidi ya shule 10 za sekondari za serikali. Utekelezaji wa shughuli za ujenzi na upanuzi katika shule za Loleza, Tabora Wavulana na Tabora Wasichana unatarajiwa kukamilika katika kipindi cha mwaka huu wa fedha. Chini ya utaratibu wa pili, shule nne za kutwa zilifunguliwa huko Ifakara, Iramba (Serengeji), Kilwa na Mtwara.

7. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 1986/87 Wizara ya Elimu itaendelea na utekelezaji wa miradi ambayo haikukamilika katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 1985/86. Vile vile Wizara itawajibika kutoa walimu vitabu na vifaa vya kufundishia kwa shule mpya 8 zinazotazamiwa kufunguliwa katika kipindi cha mwaka 1986/87 chini ya utaratibu wa pili, Shule hizo zitafunguliwa katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa, Kagera Pwani, Ruvuma, Shinyanga na Singida. Ili kutekeleza majukumu yake haya, Wizara inatarajiwa kutumia jumla ya Sh. 109.2 milioni. Kati ya fedha hizo Sh. 25.8 milioni ni za hapana shilingi milioni 4 ni, kutoka nje.

### Elimu ya Ualimu:

8. Walimu wa kutosha na walio bora ni kiungo muhimu katika suala zima la kuimarisha ubora wa elimu katika ngazi zote za elimu. Kwa kuzingatia ukweli huu, Wizara ya Elimu imekuwa na bado inaendelea na juhudi zake za kulipatia taifa walimu wa kutosha na walio bora kwa kujenga vyuo vipya, kupanua na kuimarisha vyuo vilivyopo.

9. Katika mwaka wa fedha wa 1985/86, Wizara ya Elimu iliendelea na juhudi zake hizo kwa kutekeleza miradi kadhaa ya ujenzi wa vyuo vipya, upanuzi na uimarishaji vyuo na kutoa mafunzo mbali mbali ndani na nje ya vyuo. Ujenzi wa Chuo cha Bunda umekamilika. Katika mwaka wa fedha 1986/87, Wizara itaendelea kutekeleza na kukamilisha miradi mbali mbali ambayo bado haijakamilika. Vile vile Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa walimu walio nje ya vyuo na kutoa vitabu na vifaa kwa vyuo vya ualimu. Shughuli hizi zitagharimu jumla ya Sh. 44.01 milioni; Sh. 5.7 milioni ni fedha za hapa na Sh. 38.31 milioni ni kutoka nje.

### Elimu ya Ufundi:

10. Umuhimu wa elimu ya ufundi unaendelea kukua kadiri uchumi wetu unavyoendelea kupanuka. Katika mwaka wa 1985/86, Wizara ya elimu iliendelea kutekeleza mpango wa muda mrefu wa kupanua na kuimarisha elimu ya ufundi. Madhumuni ya mpango huo ni kukidhi mahitaji ya taifa ya wataalam wa fani mbali mbali za ufundi. Jumla ya Sh. 145.87 milioni zilitumika kwa ajili ya ujenzi upanuzi na uimarishaji wa vyuo mbali mbali vya ufundi nchini. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara itaendelea kutekeleza miradi mbali mbali inayoendelea. Jumla ya Sh. 126.722 milioni zitahitajika kwa ajili ya kugharamia shughuli hizi.

### Klimu ya Juu:

11. Lengo la taifa kuhusu elimu ya juu ni kupanua na kuimarisha elimu katika ngazi hiyo ili hatimaye taifa tiweze kujitoshesheza kwa mahitaji yake ya wataalam wa ngazi ya juu katika fani mbali mbali za uchumi wetu. Umuhimu mkubwa unawekwa katika kupanua elimu ya sayansi na ufundi. Utekelezaji wa lengo hili unaendelea katika vyuo vyote vikuu vya Dar es Salaam na Sokoine.

12. Katika mwaka wa fedha wa 1985/86, shughuli zilizokuwa zikitekelezwa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam zilihusu upanuzi wa Kitivo cha Uhandisi, uimarishaji vitivo vya Uchumi na Madini kwa kutoa mafuzo ya muda mfupi na mrefu kwa walimu na watumishi wake; nje na ndani ya nchi na kununua vitabu na vifaa mbali mbali vya kufundishia. Vile vile ujenzi wa nyumba mpya na matengenezo ya nyumba za waliu, watumishi wengine na matengenezo ya majengo mengine ya Chuo uliendelea kutekelezwa.

13. Katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, shughuli kubwa zilikuwa ni pamoja na uchoraji wa ramani ya eneo la chuo, ujenzi na ununuzi wa nyumba za walimu, ujenzi wa jengo la utawala na utayarishaji wa michoro ya majengo ya sayansi ya chakula na Maktaba. Shughuli za uchoraji ramani ya eneo la chuo imekamilika.

14. Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 1986/87, shughuli za ujenzi, upanuzi na uimarishaji ambazo bado hazikamilika zitaendelea kutekelezwa katika vyuo vyote viwili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinatarajia kutumia jumla ya Sh. 53.636 milioni Sh. 18.136 milioni ni za hapa na 35.5 milioni ni kutoka nje. Nacho Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kitatumia jumla ya Sh. 36.339 milioni. Sh. 16.239 ni za hapa na Sh. 20.1 Milioni ni kutoka nje.

15. Kwa kifupi, Wizara ya Elimu haitarajii kuanza kutekeleza miradi mipya katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 1986/87. Kazi kubwa ya Wizara katika kipindi hiki itakuwa ni kuendeleza na kukamilisha miradi ambayo utekelezaji wake ulianza katika vipindi vya nyuma. Shughuli nyingi zinahusu ujenzi wa nyumba na majengo mapya na matengenezo ya nyumba na majengo ya taasisi mbali mbali za elimu. Jumla ya miradi 60 itaendelea kutekelezwa. Utekelezaji wa miradi hii utagharimu jumla ya Sh. 497.269 milioni.

## 13.—AFYA NA USTAWI WA JAMII

1. Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii wa mwaka 1986/87 una madhumuni ya kuendeleza maendeleo na shabaha ya mpango wa maendeleo wa muda mrefu: 1980—2000 ambayo ni:—

- (a) Kuongeza uhai wa Mtanzania toka anapozaliwa, toka miaka 50 (1980) na kufikia miaka 60 ifikapo mwaka 2,000;
- (b) Kuongeza afya kwa wote kwa kueneza huduma ya afya ya msingi (Primary Health Care);
- (c) Kuongeza upatikanaji wa wataalam ili kuwa na wataalam wa kutosha katika fani zote za sekta ya afya wakiwemo madaiktari, matabibu, wauguzi, mabwana afya na kadhalika;
- (d) Kuongeza ufanisi katika uendesheji wa huduma za afya katika ngazi mbali mbali kwa kutoa mafunzo ya kuandaa mfumo madhubuti wa ukusanyaji takwimu na upashanaji habari katika sekta ya afya;
- (e) Kuendeleza na kuimarisha hali ya usafama katika makazi na sehemu za kazi na;
- (f) Kuimarisha Huduma kwa wagonjwa, walemavu na watu wengine wasiojiweza.

2. Mpango huu, kama mpango uliopita wa 1985/86 unatilia mkazo uimarishaji wa huduma za afya zinazotolewa katika ngazi zote na unatoa umuhimu zaidi katika ukamilishaji na uendelezaji wa shughuli (miradi) zilizokwisha anza kuliko uanzishaji wa miradi mipya.

### Kinga:

3. Katika mpango huu umuhimu wa kwanza unseendelea kutolewa katika uimarishaji na uendelezaji wa huduma za kinga. Kinga dhidi ya maradhi ya kuambukiza imepewa nafasi ya kwanza. Mradi wa kuzuia malaria utaendelea kutekelezwa. Mradi wa chanjo kwa watoto wadogo na mama wajawazito (EPI) dhidi ya maradhi ya kupooza, surua, kifua kikuu, pepoponda na kadhalika utaendelea kutekelezwa nchini pote. Miradi mingine itakuyotekelezwa chini ya mpango huu kwa maana na lengo la kuimarisha na kuendeleza huduma za kinga dhidi ya maradhi mbali mbali ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza ni Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) na uzulaji wa magonjwa mengineyo, na Mpango wa Afya ya Msingi. Jumla ya sh. 10.38 milioni fedha za hapa na sh. 26.2 milioni fedha za nje zitatumika kwa maendeleo ya huduma za kinga.

### Tiba:

4. Kwa kuzingatia mahitaji ya matibabu dhidi ya maradhi mbali mbali nchini katika wakati uliopo, mpango wa 1986/87 pia umeweka uzito mkubwa katika uimarishaji wa huduma za tiba. Majengo zikiwemo nyumba za watumishi, maabara na wodi za wagonjwa na vifaa mbali mbali katika taasisi mbali mbali zinazohusika na huduma za tiba zitaendelea kufanyiwa matengenezo. Mradi maalum wa matengenezo ya Hospitali za Taifa zikiwemo Mirembe na Kibong'oto itaendelea kutekelezwa. Kadhalika Shirika la Afya Muhimbili litaendelea na matengenezo mbali mbali ya maji, umeme, mifereji ya maji machafu na vifaa vingine.

5. Shirika la Chakula na Lishe litaendelea na utafiti juu ya uhusiano kati ya chakula na lishe na mazingira ya kiuchumi (uzalishaji chakula, mvua) na kijamii (idadi ya watu). Jumla ya sh. 11.0 milioni fedha za hapa na sh. 9.6 milioni fedha za nje zitatumika kwa maendeleo ya sekta ndogo ya huduma za tiba katika kipindi cha 1986/87.

### Mafunzo:

6. Mpango wa 1986/87 unseendelea kuzingatia umuhimu wa mafunzo katika kuongeza upatikanaji wa wataalam wa kada ya afya na ufanisi katika utendaji kazi. Jumla ya sh. 4.45 milioni fedha za hapa na sh. 6.4 milioni fedha za nje zitatumika kwa shughuli za kuimarisha vyuo na mafunzo ya wataalam na watumishi wa fani na daraja mbali mbali. Vyuo vya wauguzi, Matabibu, Wakunga wasaidizi wa vijijini, mabwana Afya na watumishi wengine vitaendelea kufanyiwa matengenezo ya majengo, vifaa na kadhalika.



## 14.—MAENDELEO YA JAMII NA UTAWALA

### A.—MAENDELEO YA JAMII

1. Usimamizi wa shughuli za maendeleo ya Jamii, Utamaduni na Michezo umekuwa ukibadilika mara kwa mara. Katika kipindi cha miaka 23 iliyopita, shughuli hizi zimekuwa chini ya usimamizi wa Wizara na Idara saba (7) tofauti. Hali hii ya mabadiliko ya mara kwa mara imesababisha ukosefu wa usimamizi mzuri na kumbukumbu sahihi za maendeleo ya shughuli mbali mbali katika sekta hizi. Kuanzia mwezi Novemba 1985, kwa mara nyingine, shughuli za maendeleo ya jamii, utamaduni na michezo zimekuwa chini ya usimamizi mpya wa Wizara mpya ya "Maendeleo ya Jamii, Utamaduni, Vijana na Michezo". Kazi kubwa ya Wizara hii mpya itakuwa ni kuendeleza juhudi za taifa za kusaidia kupanga, kuendeleza, kuratibu na kudhibiti maendeleo ya shughuli mbali mbali katika sekta za maendeleo ya Jamii, Utamaduni na Michezo.

2. Mpango wa 1986/87 utaendelea kuzingatia haja ya kupanua na kuimarisha huduma za matunzo kwa wagonjwa, vilemna na watu wengine wasiojiweza. Uimarishaji wa huduma za makazi katika makazi yaliyopo umepewa umuhimu wa kwanza na kupewa uzito zaidi. Ujenzi na matengenezo ya nyumba za watumishi na watumikiwa vitaendelea katika makazi ya Sukamabela (Singida), Kisangara (Kilimanjaro), Nyabange (Mwanza), Magugu na kwingineko. Matengenezo pia yatafanyika kwenye makazi ya watoto wadogo Kurasini mjini Dar es Salaam.

3. Mafunzo yenye lengo la kuwapatia vilemna stadi mbali mbali ili hatimaye waweze kujitegemea japo kwa kiasi fulani tu, nayo yamewekwa mkazo mkubwa kwenye mpango huu. Ujenzi wa karakana ya walemavu Mbeya utanza chini ya mpango huu.

4. Huduma za malezi ya watoto wadogo na marekebisho ya tabia ya watoto watukutu nazo zitaendelea kuimarishwa katika mwaka 1986/87 kwa kuendelea na kutoa mafunzo kwa walezi wa vituo vya kulelea watoto mchana na kuimarisha huduma katika shule ya maadilisho Irambo, Mbeya.

5. Upatikanaji wa wataalam wa kada ya ustawi wa jamii imeendelea kupewa umuhimu unaostahili katika mpango huu. Ujenzi wa nyumba za walimu na mabweni ya wanafunzi katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii mjini Dar es Salaam utaendelea kwa maana hiyo.

6. Jumla ya sh. 12.8 milioni fedha za hapa zitatumika kwa maendeleo ya Ustawi wa Jamii chini ya mpango huu.

7. Kwa pamoja jumla ya Sh. 38.62 milioni fedha za hapa na sh. 42.2 milioni zikiwa ni misaada kutoka nchi na mashirika mbalimbali duniani zimetengwa zitumike kwa shughuli za maendeleo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, katika kipindi cha 1986/87.

### B.—UTAWALA

8. Shughuli za utawala zinazogharamiwa na Serikali husimamiwa na Wizara/Idara za Mambo ya Ndani, Ulinzi, Mahakama, Fedha na Mipango, Sheria n.k. Katika mpango wa mwaka 1986/87 Wizara ya Mambo ya Ndani itatekeleza miradi itakayokuwa na madhumuni makubwa yafuatayo:—

(i) Kuwapatia askari Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto sehemu bora za kuishi.

(ii) Kuwapatia watumishi wa Wizara, ofisi za kutosha.

(iii) Kuwapatia askari wote zana na vifaa vya kutosha vya kufanyia kazi.

(iv) Kulipa Jeshi la Magereza uwezo kubwa zaidi wa kuzalisha chakula hadi kujitosheleza wenyewe, na

(v) Kuendeleza shughuli za kiufundi na kilimo kwa jumla katika magereza ili kuwarekebisha wahalifu.

9. Ili kuweza kufanikisha shabaha hizi, Wizara ya mambo ya Ndani na Idara zake zitatumia jumla sh. 130 milioni kutekeleza miradi mbalimbali. Kati ya miradi ambayo itatekelezwa ni ile ya Ujenzi, Kilimo, Mifugo, Mawasiliano na Viwanda. Shughuli za Ujenzi ndiyo kubwa kuliko zote na zitachukuwa asilimia kubwa ya bajeti ya Wizara. Kazi kubwa ni kujenga nyumba na ofisi na kuyafanyia matengenezo makubwa majengo yaliyochakaa.

10. Shughuli za Kilimo na Mifugo zina miradi kadhaa ambayo itatumia jumla Sh. 20.4 milioni ambayo ni asilimia 15.7 ya bajeti ya Wizara. Malengo ya Idara hii ni kuliwezesha Jeshi la Magereza kujitosheleza kwa chakula. Kazi za viwanda zitatekeleza miradi 6 yenye jumla ya Sh. 1.95 milioni. Miradi hii hutumiwa kama njia mojawapo ya kuwarekebisha wahalifu kwa kuwafunza Kilimo bora na shughuli za viwanda vidogo vidogo, kwa upande wa Mawasiliano itatekelezwa miradi itakayoweza Idara kupata zana na vifaa vya kufanyia kazi. Vifaa hivi ni pamoja na magari, mashua, redio n.k.

11. Wizara ya Sheria impangiwa kutumia Sh. 2.0 milioni ili kuendelea kutekeleza mradi wa uimarishaji na uenezi wa uandikishaji wa vizazi na vifo katika wilaya 12. Mahakama nayo itaendelea na ujenzi wa mahakama ya Magu.

12. Jukumu kubwa mojawapo la Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango utakuwa ni kuendelea na ukusanyaji wa kodi mbali mbali. Ili kutekeleza jukumu hili ipasavyo, wizara itajenga ofisi za forodha na kodi za mauzo katika wilaya mbali mbali kama Singida, Songea, Kyaka, Kiteto, Iringa n.k. Vile vile vituo 12 vya kodi ya njia vitajengwa ili kufanikisha ukusanyaji wa kodi hii Baadhi ya vituo hivyo ni Chalinze, Segera, Makanbaku, Mbozi, Rusumo Falls, Holili na Horohoro.

13. Jukumu lingine kubwa la Wizara hii litakuwa ni kuendelea na upangaji wa mipango ya maendeleo. Ili kutekeleza jukumu hili miradi mbali mbali itatekelezwa kama mradi wa usimamizi wa miradi, utayarishaji wa mpango wa miaka mitano n.k.

## 15.—KAZI

### A. Mafunzo ya Ufundi Stadi:

1. Katika kutilia mkazo mafunzo ya ufundi nchini, Serikali itaendelea kutekeleza miradi mbali mbali katika baadhi ya vyuo vya Ufundi Stadi hapa nchini katika kipindi cha 1986/87.

Katika mpango huu:—

(i) Chuo cha Ufundi Mwanza kitafanywa upanuzi wa mita za mraba 320. Hali kadhalika karakana itapanuliwa na jumla ya nyumba 3 za waalimu zitajengwa.

- (ii) Upanuzi wa mita za mraba 320 utafanywa katika Chuo cha Ufundi cha Tanga na pia nyumba 4 za waalimu zitakamilishwa.
- (iii) Marekebisho ya "welding—Fabrication" pamoja na eneo la karakana yatafanywa katika chuo cha ufundi cha Chang'ombe. Pia ununuzi wa Samani kwa ajili ya karakana, Hosteli ya wanafunzi, madarasa na jikoni utafanywa.
- (iv) Chuo cha Arusha kitafanyiwa marekebisho ya karakana, madarasa, ofisi na mabweni.
- (v) Chuo cha waalimu wa ufundi, Morogoro, kitakamilisha ujenzi wa nyumba zilizoanza kujengwa katika kipindi cha 1985/86 pamoja na kujenga nyumba nyingine tano zaidi.
- (vi) Vyuo vya ufundi vilivyopo katika mikoa ya Mara, Kagera, Iringa, Lindi na Singida vitafanya marekebisho ya majengo yaliyotolewa na uongozi wa mikoa hiyo ili yatamike kama karakana na madarasa kwa ajili ya mafunzo ya ufundi.
- (vii) Ujenzi wa awamu ya kwanza wa Chuo cha Mbeya utaendelezwa.

2. Katika kutekeleza mpango huu katika kipindi cha 1986/87, Serikali itatumia fedha za hapa Sh. 27,115,000/-. Sehemu kubwa ya fedha hizi itatumika kununulia vifaa vya ujenzi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi iliyotajwa hapo juu. Ujenzi wenyewe utafanywa na wanafunzi kama sehemu ya mafunzo yao kwa vitendo.

3. Jumla ya fedha za kigeni Sh. 17,342,000/- zrtahitajika katika kutekeleza mpango huu katika kipindi cha 1986/87. Kati ya fedha hizi Sh. 15,842,000/- ni misaada itakayotolewa na shirika la misaada la Sweden—SIDA (Sh. 13,842,000/-) na Serikali ya Uswiss (Sh. 2,000,000/-) na Sh. 1,500,000/- ni mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB).

Fedha hizi za kigeni zitatumika:

(a) Kununulia vifaa vya mafunzo na spea (b) kulipia mishahara ya waalimu na wataalam wa nje, gharama za wataalam wa muda mfupi (consultants) na kulipia gharama za ukaguzi wa vyuo, (c) kununulia vitabu na vifaa vinavyotumika katika kukuza mitaala (curricula development) pamoja na kugharamia mafunzo ya waalimu wa ufundi na (d) kujenga karakana ya kuchapisha, hosteli ya wanafunzi na nyumba za waalimu.

B. Katika kipindi cha 1986/87, Serikali itatumia fedha za hapa Sh. 6,000,000/- kwa ajili ya kufanya matengenezo ya majengo ya I.D.M. Mzumbe. Vifaa vya kufanyia matengenezo vimeishawasili. Katika kutekeleza mpango huu, Serikali ya Finland itatoa msaada wa fedha za kigeni Sh. 14,000,000/-, kwa ununuzi wa vifaa vya kufanyia matengenezo.

C. Shirika la Akiba ya Taifa ya Wafanyakazi (N.P.F.)

1. Miradi yote itakayotekelezwa na Shirika katika kipindi cha 1986/87 itagharamiwa na fedha za mfuko wa shirika lenyewe. Shirika lina miradi ya aina tatu (3) ambayo itaendelezwa katika kipindi cha 1986/87 kama ifuatavyo:—
2. Shirika litatekeleza miradi ya maendeleo ya shirika ipatayo 29. Miradi ya maendeleo ni pamoja na ujenzi wa ofisi za shirika mikoani na wilayani pamoja na nyumba za kuishi watumishi. Miradi hii italigharimu shirika kiasi cha fedha za hapa Sh. 14,700,000/- katika kipindi cha 1986/87.
3. Hali kadhalika katika kipindi cha 1986/87, Shirika litatekeleza miradi ya vitega Uchumi vya Bodi ya Wadhamini ipatayo 8. Hii ni aina ya miradi ya shirika ambayo ina lengo la kuongeza pato halisi la Bodi ya Wadhamini. Chini ya mpango huu, ujenzi wa ofisi za kupangisha utaendelea huko Dodoma, Ubungo, (DSM), Kibaha, Songea, Iringa, na Shinyanga. Pia nyumba ya kupangisha (Morogoro) na upanuzi wa Makao Makuu (DSM) utaendelezwa katika kipindi cha 1986/87. Miradi ya aina hii italigharimu shirika fedha za hapa Sh. 25,000,000/- katika kipindi cha 1986/87.
4. Aidha shirika litatekeleza kutekeleza miradi ya vitega uchumi vya Akiba vya wanachama ipatayo 4. Miradi ya aina hii ina lengo la kuongeza mapato ya wanachama wa shirika. Katika kipindi cha 1986/87 Shirika litatekeleza ujenzi wa jengo la Wizara ya Kilimo pamoja na Maliasili na Utalii (Dodoma), ujenzi wa hoteli na ofisi ya kupangisha (DSM). Ujenzi wa nyumba za kupangisha Mbezi Beach pamoja na ujenzi wa Maghala utatekelezwa katika kipindi cha 1986/87.

Mpango huu utaligharimu shirika fedha zake za hapa Sh. 130,000,000/- katika kipindi cha 1986/87.

## SURA YA TANO

### MPANGO WA MAENDELEO WA MIKOA MWAKA 1986/87

#### Mapitio ya Mpango wa Mwaka 1985/86:

Katika mpango wa mwaka 1985/86, miradi ya mikoa na Halmashauri za Wilaya ilitengwa Sh. 942.9 milioni. Kati ya fedha hizo, Sh. 549.77 milioni ilitengwa kwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Sh. 393.13 milioni ilikuwa ni ruzuku kwa miradi inayotekelezwa na Halmashauri za Wilaya.

Katika kipindi cha Julai 1985 hadi Machi, 1986, jumla ya Sh. 519.9 milioni zilikuwa zimetolewa kwa mikoa na Halmashauri za Wilaya. Taarifa za utekelezaji zinaonyesha kuwa utekelezaji wa Mpango uliendelea kuathiriwa na ukosefu wa vifaa, mafuta ya petroli, vipuri na kadhalika. Pia upandaji wa bei uliongeza gharama za utekelezaji hasa kwa vifaa vya ujenzi. Hali hiyo imesababisha matumizi makubwa kifedha, lakini utekelezaji halisi (physical-implementation) ulikuwa chini ya malengo yaliyowekwa.

#### Shabaha za Mpango wa 1986/87:

Shabaha za Mpango wa Maendeleo wa mwaka 1986/87 ni hizi zifuatazo:—

- (i) Kuendeleza shughuli za kuimarisha na kukamilisha miradi iliyoanza miaka ya nyuma.
- (ii) Kuweka uratibu wa karibu zaidi kwa miradi inayotekelezwa na Halmashauri za Wilaya na Miji ili kuweza kukabili uzorotaji katika kutekeleza mipango, hali ambayo imejitokeza katika baadhi ya Halmashauri hizo.
- (iii) Kuweka huduma zinazosaidia uzalishaji katika sekta ya kilimo.
- (iv) Kuendeleza utoaji wa huduma za maji, elimu na Afya.

#### Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 1986/87:

Mpango wa Maendeleo ya Mikoa, Wilaya na Miji kwa mwaka 1986/87 umekadiriwa kutumia jumla ya Sh. 1,080.0 milioni, ikiwa ni nyongeza ya Sh. 43.7 milioni au asilimia 4.2 ikilinganishwa na makadirio ya mwaka 1985/86. Kati ya fedha zilizotengwa, Sh. 778.0 ni fedha za hapa na Sh. 302.0 milioni ni fedha za nje. Kati ya fedha za hapa, Sh. 367.16 milioni au asilimia 34.0 ya fedha zote zilizotengwa kwa mikoa na wilaya zimetengwa kama ruzuku kwa miradi inayotekelezwa na Halmashauri za wilaya. Ruzuku kwa miradi ya halmashauri za miji ni Sh. 129.22 milioni au asilimia 12.0 ya bajeti ya mikoa na halmashauri. Pamoja na ruzuku ya Serikali, Halmashauri za Wilaya na Miji zinategemewa kuchangia jumla ya Sh. 323.29 milioni kwenye miradi yao katika mwaka 1986/87. Mgawanyo wa fedha baina ya mikoa, ruzuku kwa halmashauri na mchango wa halmashauri umeonyeshwa katika Majedwali Na. 28 na 29.

Mpango wa mwaka 1986/87, kama ulivyokuwa Mpango wa mwaka 1985/86, umeendelea kutilia mkazo sekta za uzalishaji mali ambazo zimetengwa asilimia 48.5 ya fedha za maendeleo kwa mikoa. Miradi ya uzalishaji mali ni katika sekta kilimo na mifugo viwanda na mafiasili.

Mgawanyo wa fedha za maendeleo umeendelea kuzingatia Agizo la Chama la kutoa umuhimu wa juu kwa Sekta ya Kilimo. Kwa mwaka 1986/87, sekta ya kilimo ikijumuisha uendelezaji mazao na mifugo, hifadhi ya ardhi ambayo ni pamoja na upandaji miti, na barabara vijijini zinazosaidia katika kutoa huduma za usafirishaji kwa sekta ya kilimo kwa jumla zimetengwa Sh. 513.94 milioni au asilimia 47.6 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mikoa, wilaya na miji.

